# BUNGE LA TANZANIA

# MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA SITA

### Kikao cha Nane – Tarehe 8 Februari, 2007

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Wajeshimiwa Wabunge itakumbukwa kuwa aliyekuwa Waziri wetu wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro, aliteuliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuwa Msaidizi wake, yaani Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Kutokana na uteuzi huo, Mheshimiwa Dr. Migiro aliniandikia barua ya kujiuzulu Ubunge tarehe 8 Januari, 2007.

Kutokana na barua hiyo nilimwandikia Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi kumfahamisha kuwepo kwa nafasi wazi ya Ubunge.

Jana,tarehe 7/2/2007 Katibu wa Bunge amepokea barua kutoka kwa Mkurugenzi wa Tme ya Uhaguzi iliyoelezea uteuzi wa jina la Mbunge atakayeziba nafasi ya Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro ambaye ndiye atakayeapishwa hivi punde.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita *Serjeant At Arms* aweze kumwita Mbunge mteule, Florance Kiendesya aje Ukumbini ili kuja kuapa.

*Hapa (Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya) Aliingia Ukumbini tayari Kuapa Kiapo cha Uaminifu*

### KIAPO CHA UAMINIFU

Mjumbe aliyetajwa hapo chini aliapa Kiapo cha Uaminifu na kukaa katika nafasi yake ndani ya Bunge:-

Mheshimiwa Florence Essa Kyendesya.

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (DR.DAVID MATHAYO DAVID)**: Taarifa ya Mwaka ya Kumi na Tisa na Ishirini na Hesabu za Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika kwa Mwaka Ulioishia tarehe 30 Juni, 2004 na

tarehe 30 Juni, 2005. *(The Nineteenth and Twentieth Annual Reports and Accounts of the Co-operative Audit and Supervision Corporation for the years ended 30th June, 2004 and 30th June, 2005)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 98

### Hitaji la Kuigawa Wilaya ya Karagwe kuwa Wilaya Mbili

**MHE. GOSBERT B. BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Karagwe ni kubwa na inavyo vigezo vyote vya kuigawa katika Wilaya mbili, na ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuigawa wilaya ya Karagwe kuwa wilaya mbili?

(b) Je, zoezi hilo litachukua muda gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uundwaji au ugawaji wa maeneo mapya ya kiutawala hapa nchini unatawaliwa na Sheria za Serikali za Mitaa Na. 7 (Mamlaka za Wilaya) na Sheria Na. 8 (Mamlaka za Miji) za mwaka 1982 na Sheria ya taratibu za uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya Na. 12 ya mwaka 1994. Aidha viko vigezo muhimu vinavyotumika kuanzisha maeneo mapya ya utawala.

Mheshimiwa Spika, inawezekana wilaya ya Karagwe ni kubwa lakini kulingana na hali halisi ilivyo sasa Wilaya nyingi hapa nchini zinastahili kugawanywa katika maeneo mawili au zaidi. Hivyo ni vizuri mchakato huu ukaanzia katika ngazi ya Halmashauri na maombi haya yawasilishwe kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za mitaa ili ayashughulikie kwa mujibu wa sheria na vigezo vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ni vema wananchi wote wafahamu kwamba ugawaji wa Wilaya au uanzishwaji wa maeneo mapya ya utawala inawezekana endapo Serikali inalo fungu la kuyajenga. Makao Mkuu ya Wilaya, gharama za uendeshaji na uwekaji miundombinu muhimu pamoja na watumishi wa Wilaya husika. Inakadiriwa kuwa kuanzisha Wilaya moja inaigharimu Serikali bilioni 1 hadi, 2 ambazo ni fedha nyingi na siyo rahisi kwa Serikali kuzipata kwa wakati mmoja kwa maeneo mengi. Hivyo kuanzisha maeneo mapya kunafanyika kulingana na uwezo wa Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la (a) kuanzisha maeneo ya utawala ni mchakato ambao unazingatia mambo mengi. Namshauri Mheshimiwa Mbunge apeleke suala hili katika Halmashauri yake ili lizungumziwe kuanzia kwa wananchi wa eneo hilo.

Aidha, maombi yapitishwe katika vikao halali na baadaye kuawasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikao na Serikali za Mitaa. Hivyo kwa utaratibu huu siyo rahisi kusema suala kama hilo litachukua muda gani.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri na kwa kuwa ameeleza kwamba itabidi Halmashauri ya Karagwe ifuate taratibu ili kuweza kufanya mchakato mzima kuweza kukamilika naomba nimwulize Naibu Waziri sijui kama anajua kwamba taratibu hizi za kuanzia kwenye Halmashauri tayari zilishafanyika na kama anajua hilo ningependa anifahamishe ni kikwazo gani ambacho kimekwamisha Wilaya ya Karagwe isigawanywe mara mbili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi kwamba vigezo ni hatua mojawapo lakini hatua ya pili ni uwezo wa Serikali na la tatu ambalo Mheshimiwa Mbunge ameniuliza ni kwamba; habari nilizopata kutoka Karagwe mpaka jana vikao husika havijakaa katika Halmashauri ya Karagwe.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge arudi ili mchakato huu uanze kwenye vikao vyao vya Halmashauri hatimaye kwenye *RCC* na hatimaye iletwe kwenye Waziri mwenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Lakini hata hivyo inategemeana na uwezo wa Serikali.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya za Mkoa wa Singida, Iramba, Manyoni na Singida Vijijini zinafanana kabisa na maombi ya Wilaya ya Karagwe na kwa kuwa Wilaya hizo tayari zimeshajadili vikao vyote husika katika Mkoa wa Singida na Wilaya zake. Je, Serikali itakuwa tayari kuingiza Wilaya ya Iramba, Wilaya ya Singida na Wilaya ya Manyoni katika orodha ya Wilaya zitakazogawanywa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa Halmashauri, Wilaya ambazo zinakidhi vigezo vya kuanzishwa kuwa Wilaya ziko karibu 42 mpaka sasa hivi. lakini tunachosema ni kwamba uanzishwaji wa Wilaya kuna gharama zake. Kwa hiyo, hatuwezi tukaanzisha Wilaya zote 42 kwa wakati mmoja kama nilivyosema itategemea na uwezo wa Serikali. Maombi yako mengi, vigezo Wilaya nyingi zimekidhi lakini tatizo kubwa ni ufinyu wa Bajeti. Kwa hiyo, tunaangalia pia na hali ya Bajeti ya Serikali.

Na. 99

**Hitaji la Mkoa – Wilaya ya Geita**

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Wilaya ya Geita wako mbali sana na Makao Mkuu ya Mkoa hali inayosababisha wapate shida sana kwa kusafiri safari ndefu kufuata huduma za Kimkoa katika Mkoa wa Mwanza ambapo hulazimika kuvuka ziwa na mara nyingi hulala Kivukoni Busisi au Kamanga; na kwa kuwa, wananchi wa Wilaya za Bukombe na Chato hupata matatizo kama hayo wakifuata huduma Shinyanga au Bukoba; na kwa kuwa, nia nzuri ya Serikali ni kuwapatia wananchi maendeleo na huduma kwa karibu:-

Kwa kuwa, vigezo vya kuunda Mkoa vinatosheleza na vinaruhusu. Je, Serikali haioni kuwa, ni muda muafaka sasa wa kuunda Mkoa kwa kuunganisha Wilaya za Geita, Chato, Bukombe na Sengerema ili kuwaondolea wananchi usumbufu na kuhamasisha maendeleo katika maeneo hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Nne wa Bunge lako Tukufu, tarehe 31/7/2006, Ofisi yangu ilijibu swali Na. 321 lililoulizwa na Mheshimiwa Ernest Mabina, Mbunge wa Geita, linalofanana na swali hili. Katika majibu yangu nilieleza bayana kuwa; utaratibu wa kuunda au kugawa maeneo ya kiutawala unatawaliwa na Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 7 kwa Mamlaka za Wilaya, na Na. 8 kwa Mamalaka za Miji za mwaka 1982 na Sheria ya Taratibu za uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya Na. 12 ya mwaka 1994.

Pamoja na Sheria hizi, vipo vigezo vingine vinavyopaswa kuzingatiwa kabla ya kuanzisha Mkoa. Vigezo hivi ni pamoja na:-

Ukubwa wa eneo usiopungua kilometa za mraba elfu kumi (10,000) NA:-

- Idadi ya watu wasiopungua laki tano (500,000).
- Jiografia ambayo inafanya utoaji wa huduma kwa wananchi kuwa mgumu.
- Rasilimali fedha, watu na miundombinu muhimu.
- Vigezo hivi kwa sasa vimepitwa na wakati na vinapatiwa upya.

Mheshimiwa Spika, vilevile chini ya Ibara ya pili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Rais amepewa mamlaka ya kugawa nchi: “Kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Rais anaweza kuigawa Jamhuri ya Muungano katika Mkoa, Wilaya na maeneo mengineyo kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria zilizotungwa na Bunge, isipokuwa kwamba Rais atashauriana kwanza na Rais wa Zanzibar kabla ya kuigawa Tanzania Zanzibar katika Mikoa, Wilaya au maeneo mengineyo”. Mwisho wa kunukuu.

Kwa kuzingatia vigezo vilivyopo kwa sasa, Wilaya ya Geita inakidhi sifa za kuunda Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hitaji la Mkoa Wilayani Geita, katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Mwanza *(Regional Consultative Committee)* kilichofanyika tarehe 23/11/2006 ambapo Mheshimiwa Mbunge ni mjumbe katika kikao hicho, suala hili la

kuanzisha Mkoa wa Geita lilijitokeza. Katika kikao hicho ilishauriwa kwamba ni vema mchakato uanzie katika Wilaya husika ili kupata maoni ya wananchi kabla ya kuletwa kwenye kikao cha ushauri cha Mkoa. Taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Geita haijawahi kujadili hoja ya kuundwa kwa Mkoa wa Geita katika vikao vyake.

Aidha, baadhi ya Wilaya zilizopendekezwa kujumuishwa na Mheshimiwa Mbunge ni za Mikoa ya Shinyanga na Kagera. Mikoa hiyo pia inatakiwa kukaa na kuridhia uanzishwaji wa Mkoa mpya katika kumega maeneo yake. Suala la uanzishwaji wa Mkoa mpya wa Geita litajadiliwa katika kikao cha Kamati ya ushauri ya Mkoa kinachotarajia kufanywa Februari, 2007 ambapo taarifa ya wilaya ya Geita kuhusu suala hili, itakapokelewa na kujadiliwa. Hivyo namsihi Mheshimiwa Mbunge awe na subiri tupate matokeo ya majadiliano katika Mikao na Wilaya husika.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri yenye matumaini. Kwa kuwa, kuna mabadiliko katika vigezo naamini katika mabadiliko hayo, wilaya ya Geita na wilaya nilizozitaja hata iweje lazima zitakidhi haja na sisi kwa maelekezo tuliyopewa na Serikali kwamba twende tukakae, Kwa kuwa tutaenda kukaa haraka haraka Mheshimiwa anatuahidi kwamba hili suala atalipa kipaumbele kwa sababu wananchi hao wanateseka?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijasema kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo yake mazuri sana. Kimsingi Serikali inachosema ni kwamba uanzishwaji wa maeneo haya, ni jambo ambalo Serikali inaona umuhimu wake, lakini ni lazima tukubali umuhimu wake. Lakini ni lazima tukubali kwamba gharama zake ni kubwa sana. Mara ya mwisho Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa Iringa, alitoa maelezo pale kwamba kuanzisha mkoa mmoja ni karibu bilioni tisa, kwa vyovyote vile si jambo ambalo unaweza ukalifanyia uamuzi wa haraka haraka. Lakini pamoja na hayo alitoa maelezo, kwamba kugawa mkoa mmoja katika mikoa miwili katika mazingira ya gharama kubwa hizi ni jambo ambalo Serikali inasita kwa sasa.

Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu akasema, tunachoweza kwa sasa kujaribu kuangalia ni kuona mikoa ile ambayo inapakana mipaka yake kumega wilaya zile ambazo zikawiana na kuunda mkoa mmoja, nia ni kusogeza madaraka kwa wananchi katika eneo linalohusika, na kwa maana hiyo basi mkoa huu ambao unaombwa, ambao umeunganisha zile wilaya tatu katika mikoa ile mitatu ndio zana ambayo sasa tunajaribu kwenda nayo.

Lakini bado uamuzi lazima uzingatie uwezo wa Serikali, na kwa wakati huo itategemea vilevile mambo mengine ambayo itabidi Serikali iangalie, kwa hiyo hatutaki kuwavunja moyo lakini ni vizuri mkajua kwamba ni jambo ambalo linataka tafakuri kubwa zaidi kidogo.

Na. 100

**Kupandishwa Hadhi Mji wa Kahama**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa, takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa Mji wa Kahama unakuwa kwa kasi kubwa kuliko Miji mingine Mkoani humo kwa takribani asilimia 7 kwa mwaka ukiwa na wakazi

zaidi ya 50,000 na hivyo kukidhi karibu vigezo na masharti yote ya kupandishwa hadhi kuwa Mji Mdogo; na kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama ilishawahi kutuma maombi ya kupandishwa hadhi ya Mji wa Kahama:-

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka kabisa wa kukubali ombi la Halmashauri ya Kahama, hivyo kupandishwa hadhi ya Mji wa Kahama?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Mji wa Kahama unakuwa kwa kasi kubwa na unakidhi vigezo vilivyopo vya kupandisha hadhi eneo hilo kuwa Mji. Vigezo vya eneo kuweza kupandishwa hadhi ya kuwa Mji ni eneo hilo kuwa na idadi ya wakazi wapatao 30,000; kuwepo na kiwango cha juu cha utoaji wa huduma za Afya, Shule ya Sekondari; Maduka 50; Kituo cha Polisi; Makao Makuu ya Tarafa; Uwezo wa kujiendesha kwa asilimia 50 ya Bajeti ya Mamlaka ya Mji Mdogo.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopo, eneo analolitaja Mheshimiwa Mbunge lina jumla ya watu 100,574; Hospitali 2; Vituo vya Afya 2; Zahanati 7; Shule za msingi 21; Sekondari 8; Maduka ya Jumla 86; Maduka ya Rejareja 683; Kituo cha Polisi 1; Mahakama ya Wilaya 1; Mahakama ya Mwanzomoja na Benki 4.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliopo, Halmashauri ya Kahama inatakiwa kupeleka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa maombi ya kupandishwa hadhi eneo la Kahama kuwa Mji. Maombi haya yanatakiwa kwanza yawe yamejadiliwa na kupitishwa katika vikao vya Halmashauri na Uongozi wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, mpaka hivi sasa Ofisi yangu haijapokea maombi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kahama kupandisha hadhi eneo la Kahama kuwa Mji. Maombi yaliyopelekewa ni mapendekezo ya mipaka ya Mji Mdogo wa Kahama ambayo ni hatua mojawapo ya kutekeleza Tangazo la Serikali Namba 137 la tarehe 8 Julai, 1990. Agizo ambalo halijawahi kutekelezwa hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, maombi hayo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kahama yatakapowasilishwa, Ofisi yangu itashughulikia ipasavyo.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaswali moja la nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kwamba ofisi yake imewahi kupokea maombi ya kupandisha hadhi ya mji wa Kahama kuwa Mji mdogo hapana.

Na kwa kuwa Naibu amekiri kwamba ofisi yake imewahi kupokea maombi ya Halmashauri ya Wilayaya Kahama ya kupandishwa kuwa Mji Mdogo ambayo ni hatua moja wapo ya kutekeleza tangazo la Serikali Na. 137 la tarehe 8/7/1990. Je, ni lini Mji wa Kahama utapewa hadhi ya Mji Mdogo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi kwamba kupandishwa hadhi kwa mji mdogo wa Kahama, tangazo la Serikali lilitolewa mwaka 1990 mpaka sasa hivi ndugu zetu wa Kahama hawajaanzisha huo mji mdogo. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wakishirikiana na Halmashauri waanzishe kwanza huo mji mdogo kulingana na hilo tangazo, baadaye ndipo waombe kupandishwa hadhi, hatua ya kwanza hawajaitimiza naomba watimize kwanza hatua ya kwanza, ndipo mji upandishwe hadhi. *(Makofi)*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza, kwa kuwa katika majibu aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri akijibu swali Na. 98, na hivi punde akijibu swali la Mheshimiwa Lembeli, vigezo ambavyo vinahitajika kwa Wilaya ya Kahama kuwa wilaya mbili, imefikiwa, lakini pia sifa zinazotakiwa kwa Kahama kuwa na hadhi ya Mji zimefikiwa. Yanayoendelea sasa ni matatizo ya kiutendaji ambayo wananchi hawahusiki nayo.

Je, Serikali iko tayari sasa kuiangalia wilaya ya Kahama katika sura ambayo ina uzito wa Wilaya mbili katika huduma kwa mfano, polisi, idadi ya polisi, hospitali ukubwa wa vitanda, au wingi wa vitanda kwenye hospitali na huduma za kiserikali, kwa sababu sifa zimefikiwa kilichobaki ni utaratibu tu wakukamilisha kinachotakiwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba ni kweli vigezo vimefikiwa, na kama alivyokiri kwamba tatizo ni la kiutendaji. Sasa Serikali itafanya nini iwapo wenyewe wananchi wa Kahama pamoja na watendaji wao wameshindwa kutekeleza huo mji mdogo kama hatua ya kwanza.

Kwa hiyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na hao watendaji kuhakikisha kwamba wanaanzisha kwanza mji mdogo wa Kahama na hatua zingine zitafuata Maombi mengine yatatekelezwa kulingana na bajeti ya Serikali.

Lakini uanzishaji wa miji midogo utakuta tatizo kubwa linatokana na miji midogo yenyewe kuchelewa jinsi ya kugawana mali na kugawa maeneo husika. Serikali mara nyingi inatoa matangazo mapema sana, kama nilivyosema kwa Kahama, mwaka 1990 wamepewa hilo tangazo na Serikali, Serikali imetimiza wajibu wake. Mpaka sasa hivi hawajatekeleza hilo agizo la Serikali.

Kwa hiyo, nawaomba Wabunge mshirikiane na wananchi wenu katika kutekeleza azma ya Serikali.

Na. 101

**Idadi ya Wahasibu Nchini**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, hadi hivi sasa Tanzania ina uhaba wa Wahasibu wanaotambulika na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu *(NBAA),* kwani hawazidi 1500 kwa nchi nzima, hali

inayosababisha watu wengi wasio Wahasibu kufanya kazi ya kihasibu kinyume na sheria na mara nyingi husababisha upotevu wa fedha nyingi hasa za Serikali:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza idadi ya Wahasibu wenye taaluma na wanaotambuliwa kisheria?

(b) Je, kwa nini Serikali haitoi mikopo kwa wavulana na wasichana waliopata daraja la pili wanaosomea fani hii kama ilivyo kwa walimu na madaktari ili kupunguza uhaba wa wataalamu wa taaluma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuongeza idadi ya wahasibu wenye taaluma na wanaotambuliwa kisheria, Serikali ilianza kudhamini watumishi (*In-service)* wa kada ya uhasibu kuanzia mwaka wa fedha wa 2001/2002, katika kozi za Stashahada ya Juu na Shahada ya Juu ya Uhasibu katika Chuo cha Uhasibu Arusha *(IAA),* Taasisi ya Uhasibu Tanzania *(TIA)* na Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM).*

Katika Chuo cha Uhasibu Arusha watumishi hudhaminiwa katika Stashahada ya Uzamili *(PGDA)* maalumu kuwawezesha kufanya mitihani ya Shahada ya Juu ya Uhasibu *(CPA)* inayosimamiwa na Bodi Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania *(NBAA).*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha hugharamia wanafunzi 1000 wa mwaka wa kwanza kila mwaka katika fani ya Uhasibu kwenye vyuo vyake vitatu (3) kama ifuatavyo:-

*IFM – 350, IAA – 350, TIA – 300,* jumla 1000. Kwa maana hiyo Serikali hugharamia wanafunzi 3000 kila mwaka, yaani kuanzia mwaka wa kwanza hadi mwaka wa tatu gharama, hizo siyo mkopo (*full bursary*).

Vile vile Serikali kupitia Wizara ya Fedha yaani Mhasibu Mkuu wa Serikali, hugharamia wanafunzi katika fani ya *Post Graduate Diploma in Accountancy* na Digrii ya Uzamili (*MBA in Accounting*) kwa ajili ya kuwaandaa wanafunzi hao kufanya mitihani ya Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu *(NBAA)* ili waweze kutambulika kisheria. Pia Serikali ina mkakati kabambe wa kuwagharamia watumishi wanaofanya kazi za kihasibu ambao hawana sifa za fani hiyo, yaani (*In-services*) katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Gharama hizo siyo mikopo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wahasibu wengi wamekuwa wakiacha kazi Serikalini na kufuata maslahi bora zaidi kwingineko Serikali imeanza kuboresha maslahi ya wahasibu na itaendelea kufanya hivyo kadri ya uwezo unavyoongezeka.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dhamana ya utoaji mikopo kwa wanafunzi inatawaliwa na Sheria ya Bodi ya Mikopo, utaratibu wa utoaji mikopo utaendelea kama ulivyo. Juhudi zinazofanywa na Serikali ni kuongeza idadi ya wadhaminiwa kadri uwezo wa kifedha utakavyoruhusu. *(Makofi)*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo ninaamini Wahasibu watarajiwa wameyasikia.

La kwanza, kwa kuwa kwa mujibu wa Sheria namba 33 ya mwaka 1972 iliyoanzisha *NBAA*, kifungu namba 23 ni marufuku kuwa mtu yeyote kumwajiri mtu asiye na sifa kama za kuwa Mhasibu na mtu huyo anayefanya hivyo anaweza kufungwa kwa miaka 2; na kwa kuwa waajiri walio wengi wanaajiri watu wasio na sifa na *NBAA* haijaweza kusimamia Sheria hiyo kutokana na mapungufu mengi yakiwa ni ya kifedha.

Je, Serikali iko tayari sasa kuisaidia Bodi hiyo ili iweze kusimamia utekelezaji wa hiyo Sheria?

La pili, kwa kuwa Serikali imekiri kwamba inatumia fedha nyingi sana kuwasomesha Wahasibu watarajiwa kutoka kwenye Idara na Halmashauri mbalimbali zilizo chini yake. Lakini Naibu Waziri amekiri kwamba Wahasibu wengi wamekuwa wakiondoka kufuata maslahi mazuri. Pamoja na jibu kwamba Serikali inaboresha maslahi ya Wahasibu. Je, Serikali haioni kwamba kutokana na upotevu mkubwa wa mali za Serikali unatokea sasa kutokana na mapungufu ya kihasibu ikafanya hima kubadilisha malipo kwa wahasibu kama ilivyofanywa kwa watumishi wengine kama Polisi ili nao waweze kutulia na kufanya kazi Serikalini badala ya kuhama kwenda kutafuta maslahi bora kwenye sekta binafsi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIB)**: Mheshimiwa Spika, *NBAA* haijashindwa kusimamia Sheria Namba 33 ya mwaka 1972, kifungu cha 23. Inafanya hivyo na itaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maslahi ya Wahasibu kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba tumeyaona hayo na tunajitahidi na tumeanza kama walivyoanza Polisi na sisi tumeanza vilevile kabla ya hapo kuwapa maslahi mazuri Wahasibu ili wasiondoke katika sehemu zetu mbalimbali za Uhasibu.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali ndogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na alivyoeleza nia nzuri ya Serikali inavyosomesha Wahasibu wengi.

Mheshimiwa Spika, moja ya Vyuo ambavyo Wizara ya Fedha ama Serikali inapeleka Wahasibu wake ni Chuo cha Usimamizi wa Fedha na Chuo hicho kimeanza miaka mingi iliyopita. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuki-*promote* Chuo hicho kiwe nacho *Univeristy* ili wale wanaomaliza pale waweze ku-*compete* kwenye soko la ajira?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIB):** Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali iko katika mchakato wa kukifanya Chuo cha *IFM* kiwe Chuo Kikuu lakini bado mchakato huo haujamalizika.

Na. 102

**Mafunzo ya Stashahada ya Juu ya Utabibu Kutolewa**

## Chuo cha Maafisa Tabibu Mtwara

**MHE. JUMA A. NJWAYO** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Afya kilichofanyika Dodoma Juni, 2006 pamoja na mambo mengine ilielezwa kuwa Chuo cha Maafisa Tabibu Mtwara *(COTC)* kina sifa ya kutoa Stashahada ya Juu ya Utabibu (*Advanced Diploma in Clinical Medicine (AMO):-*

(a) Je, ni lini Serikali itaanza kutoa mafunzo hayo *COTC Mtwara?*

(b) Je, Serikali haioni kuwa, kuna haja ya kuanzisha mafunzo hayo kwa haraka ili kupunguza tatizo la wataalam wa tiba nchini, hasa kwa Mikoa ya Mtwara na Lindi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo Mbunge wa Tandahimba, naomba kufanya masahihisho madogo katika swali lake kwa faida ya kumbukumbu kama ifuatavyo:-

Kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kilifanyika Mjini Dodoma mwezi Mei, 2006 na siyo Juni, 2006 kama ilivyoelezwa katika swali lake.

Mheshimiwa Spika, baada ya masahihisho hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Nakiri kwamba suala la kupanua mafunzo ya Stashahada ya Juu ya Utabibu (*Advanced Diploma in Clinical Medicine*) ili kuongeza idadi ya madaktari wasaidizi nchini, hususan, uwezekano wa kuanzisha mafunzo hayo katika Chuo cha Maafisa Tabibu Mtwara *(COTC),* ni miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa katika Kikao cha Baraza la Wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, kuanzisha mafunzo ya Stashahada ya Juu Utabibu (*Advanced Diploma in Clinical Medicine*) katika Chuo hicho kunahitaji kupanua nafasi ya majengo kwa ajili ya madarasa, mabweni na maktaba. Aidha, mafunzo haya yanahitaji kuwapo kwa Madaktari Bingwa wa kutosha katika hospitali, kwani sehemu kubwa ya walimu katika mafunzo haya ni Madaktari Bingwa.

Wizara imekwishafanya makubaliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank*) ili kupata mkopo kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Vituo vya Afya katika Mkoa wa Mtwara ikiwa ni pamoja na upanuzi wa Chuo cha Maafisa Tabibu Mtwara *(COTX)* ili kiweze kutoa mafunzo ya Stashahada ya Juu ya Utabibu sanjari na mafunzo ya Stashahada ya Utabibu.

Mradi huu utakaogharamiwa na fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika ni kwa miaka mitano na unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2007/2008 baada ya kukamilika kwa michoro, mipango ya utekelezaji na taratibu za kumpata mkandarasi. Hata hivyo, mafunzo ya Stashahada ya Juu ya Utabibu yanatarajiwa kuanza katikati ya kipindi cha mradi huu kwani lengo ni kuwa na wataalam kabla ya ujenzi na ukarabati wa Vituo kukamilika.

Baadhi ya Madaktari Bingwa watakakohitimu katika Vyuo Vikuu watapangiwa kufanya kazi katika Hospitali ya Mkoa wa Mtwara na kufundisha katika Chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na upungufu mkubwa wa Madaktari Wasaidizi walipo nchini ikiwa ni pamoja na Mikoa ya Lindi na Mtwara. Wizara itaendelea kuendesha mafunzo ya tabibu kujiendeleza kuwa Madaktari Wasaidizi katika Vyuo vya Madaktari Wasaidizi vilivyopo vya Bugando, Ifakara, *KCMC,* Mbeya na Tanga.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake ya kutia moyo. *(Makofi)*

(a) Kwa kuwa kuwepo kwa kozi ya Stashahada ya Juu ya Utabibu kutaondoa tatizo la wafanyakazi wenye sifa liliko kwenye Mikoa ya Mtwara na Lindi; na kwa kuwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri yamesema Mpango huo unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika utachukua miaka mitano, na kwa sababu katika hali iliyopo sasa katika Mikoa ya Kusini Mtwara na Lindi kuna matatizo makubwa ya wafanyakazi wenye sifa. Je, Serikali ina mpango gani wa kidharura wa kupunguza tatizo lililoko? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa tatizo la ukosefu wa wataalam lililoko katika Mikoa ya Mtwara na Lindi ni pamoja na ukosefu wa vifaa kama vile magari ya magonjwa hasa kwenye Vituo vya Afya vya Liteu, Namikupa na Mahuta kiasi kinachosababisha akinamama wajawazito hujifungulia njiani wakienda Newala au Tandahimba ambako pia hakuna wataalam wa kutosha. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi wa Tandahimba? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kabla sijamjibu napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, kwa kufuatilia sana masuala ya wananchi wake wa Mkoa wa Mtwara na Lindi, hususan katika Jimbo lake la Tandahimba.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba mradi huo wa *ADB* utachukua miaka mitano. Ni kweli kwamba hakuna wafanyakazi wa kutosha kama anavyofikiri, lakini kama mnavyofahamu katika majibu ya maswali yaliyopita nilisema kwamba kwa sasa hivi Serikali inajitahidi kupeleka wafanyakazi katika yale maeneo yaliyoko pembezoni.

Lakini ili kukabiliana na tatizo hilo sasa hivi tunao mpango wa *emergence hiring* ambao unafadhiliwa na *Global Fund* na sasa hivi katika magazeti yamewekwa matangazo ili watu waweze kuomba kazi za ajira na waweze kuajiriwa na watapelekwa katika sehemu hizo za pembezoni.

Mheshimiwa Spika, ninatoa wito kwa wale wenye sifa ambao hawana ajira waandike maombi kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Katibu Mkuu ili waweze kupangiwa Vituo vya kazi na katika magazeti wameweka *deadline* ni tarehe 15 Machi, 2007. Kwa hiyo, ni taarifa naomba muipokee Waheshimiwa Wabunge na muwahamasishe.

Mheshimiwa Spika, ni kweli amesema kwamba kuna upungufu mkubwa wa vifaa yakiwemo magari. Naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba kitendea kazi kama gari inayotakiwa kununuliwa ni Halmashauri husika. Kwa maana hiyo, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge wakae na Halmashauri yake ili watoe kipaumbele ili aweze kuwapatiwa *ambulance.*

Aidha, sisi Wizara ya Afya na Ustawi Jamii tukipata magari sehemu nyingine basi tutaichukulia Tandahimba kama sehemu mojawapo ambayo iko pembezoni na tutaweza kuipatia gari kama itawezekana.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, napenda niungane na Mheshimiwa Juma Njwayo, kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, katika swali la msingi la muuliza swali amezungumzia juu ya tatizo la uhaba wa watumishi hasa Madaktari na Madaktari Wasaidizi. Wilaya ya Tandahimba ni Wilaya mpya, hospitali ya Wilaya inakosa huduma kama za Daktari wapasuaji, Darubini na kadhalika. Kwa hiyo, wananchi wanapata huduma hizo katika hospitali ya jirani ya Newala. Hospitali ya Newala pamoja na kwamba inahudumia Wilaya hizo, mbili ina tatizo la Madaktari na mwaka jana wakati wa Kikao cha Bajeti Mheshimiwa Mbunge wa Tandahimba alieleza hilo nami nilieleza hilo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge uliza swali tafadhali.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu Serikali iliahidi kuongeza Madaktari katika Wilaya ya Newala ili iweze kuhudumia vizuri Wilaya hizo mbili wakati wa kikao cha Bajeti kilichopita. Je, Serikali imefikia hatua gani mpaka sasa katika kutekeleza ahadi hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba kuna uhaba wa wafanyakazi na kwamba Tandahimba kama Wilaya mpya inapata huduma katika Wilaya ya jirani ya Newala.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya awali na wakati huo, sasa hivi siyo Newala tu wala siyo Tandahimba, lakini nchini kote kuna tatizo la wataalam hususan Madaktari na Madaktari Wasaidizi.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni kwamba sasa hivi Madaktari wengi wameishafuzu na wako katika hatua za kupangiwa Vituo vya kazi. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka Mikoa ya Mtwara na Lindi kwamba tutaiangalia hiyo Mikoa kwa jicho la karibu zaidi ili tuhakikishe kwamba wataalam wengi hususan Madaktari na Madaktari Wasaidizi tunawapeleka katika maeneo husika. *(Makofi)*

Na. 103

**Huduma ya Wazee Nchini**

**MHE. LUCY F. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu Serikali imejitahidi kuhudumia makundi mbalimbali kama wanawake, watoto na watu wenye ulemavu kwa kuyapa kipaumbele katika mikakati mbalimbali ya kuondoa umaskini na kuboresha hali zao:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kundi la wazee ambao ni hazina ya Taifa?

(b) Je, Serikali iko tayari kuunda Taasisi Maalum au Idara kwenye Wizara husika ili kushughulikia wazee?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu, swali la Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, kwanza naomba kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuwepo kwa Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2002 na Mikakati ya Utekelezaji wake ni kielelezo cha dhamira ya dhati ya Serikali katika kuboresha maisha ya wazee. Utekelezaji wa Sera unahusisha wadau mbalimbali zikiwemo Halmshauri za Wilaya, Miji, Manispaa, Wakala na Asasi zisizo za Kiserikali. Aidha, utekelezaji unapaswa kuanzia katika ngazi ya familia na jamii ambayo Mheshimiwa Mbunge anaiwakilisha.

Baada ya maelezo hayo sasa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Sera imeanza kutekelezwa na baadhi ya masuala yanayohusu wazee yamezingatiwa katika mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini MKUKUTA. Aidha, kwa mujibu wa sera hiyo Serikali inakusudia kuanzisha mfuko *Revolving Loan Fund* ambao utawawezesha wazee kuendesha miradi ya uzalishaji mali. Mchakato wa kuanzisha mfuko huu utaanza mwaka huu wa fedha kwa lengo la kuanza utekelezaji mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa sera na mipango mbalimbali inayohusu wazee, Wizara inaendesha makazi 17 ya wazee na inaratibu na kusimamia makazi 24 yanayoendeshwa na wakala za hiari. Huduma kwa wazee hutolewa pia katika jamii na mwelekeo wa sasa ni kuimarisha zaidi eneo hili la huduma ili jamii ziwajibike kuwatunza wazee. Wizara itaendelea kutekeleza masuala yanayowahusu wazee na kuhamasisha ushiriki wa wadau katika utekelezaji wa mikakati mbalimballi inayolenga kuboresha maisha ya wazee.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa huduma kwa wazee zinatolewa kikamilifu kabisa na Wizara yangu kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii. Hata hivyo, pale itakapothibitika kuwa kuna mahitaji ya lazima ya kuwa na Idara/Taasisi maalum kwa ajili ya kushughulikia wazee ni dhahiri kuwa Serikali haitasita kutekeleza uamuzi huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Owenya, kabla hujauliza swali lako la nyongeza. Ningependa kwa niaba ya Wazee kukushukuru kuona kwamba unatujali sisi wazee. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ametueleza kwamba ipo sera ya wazee ili hiyo sera ya wazee iweze kutekelezeka vizuri. Je, Serikali iko tayari kutunga sheria ambayo itasimamia sera hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, napenda na mimi nimpongeza Mheshimiwa Lucy Owenya, kwa kuzungumzia sana masuala ya wazee hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, wazo alilosema ni nzuri, Wizara yangu itakaa na kuona kama itabidi kuwe na sheria maalum ambayo inawahusu wazee basi itakuja hapa ili iweze kushughulikiwa. Lakini sasa bado tunaendelea kusisitiza kwamba Mpango uliopo bado ni mzuri na wazee wana mipango mizuri tu ambayo wanashirikiana, na sera iliyopo inatosheleza kabisa. Lakini nalichukua wazo lake tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Na. 104

**Uharibifu wa Mazalio ya Samaki na Mazingira**

**MHE. DR. ALI TARAB ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa, tafiti za kisayansi za hivi karibuni ulimwenguni zinathibitisha kupungua sana kwa samaki na viumbe wa bahari (*marine biodiversity*) vikiwemo vinavyotumika kama chakula *(Sea Food*) kwa kipindi cha miaka miwili sasa; na kwa kuwa tafiti hizo zinatabiri pia kuzidi kupungua kwa kiasi kikubwa au kutoweka kabisa kwa viumbe hao ifikapo katikati ya karne hii ya ishirini na moja iwapo kasi ya uharibifu wa mazalio ya samaki na viumbe bahari wengine pamoja na uvuvi wa zaidi ya kiwango (*overfishing)* kama utaendelea kama ilivyo sasa:-

(a) Je, ni jitihada gani zinafanyika ili kuhakikisha ya kuwa, mazalio ya samaki kwenye bahari yetu hayaharibiki?

(b) Je, isingekuwa bora kwa Taasisi zetu husika za bahari zikiwafunza wavuvi na vikundi vya wananchi waishio kwenye mwambao namna ya kufuga na kuzalisha viumbe wa bahari kama vile ngisi, pweza, kamba, kaa na chaza ili kupunguza uvunaji wa viumbe hivyo baharini?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua tatizo la uharibifu wa mazingira baharini hususan mazalio ya samaki. Serikali yetu imeweka mikakati mbalimbali ikiwemo usimamizi wa Sheria zinazohusika. Katika Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2005 na Kanuni zake za 2005 zinasisitza kwamba ni marufuku kutumia zana ambazo haziruhusiwi kisheria katika uvuvi endelevu. Zana hizo ni pamoja na nyavu zenye macho madogo, makokoro, uvuvi wa kutumia mabomu na kadhalika.

Katika kutekeleza hili, Wizara yangu inashirikiana na Taasisi mbalimbali za Serikali kama vile Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Kikosi cha Wanamaji katika kudhibiti uvuvi haramu baharini. Aidha, wananchi wanashirikishwa katika ulinzi wa

maliasili ya uvuvi kwa kutumia vikundi vya ulinzi wa rasilimali (*Beach Management Units, BMU's*).

Njia nyingine ni kupunguza uvuvi unaozidi kiwango kwa kufunga shughuli za uvuvi kwa mfano, shughuli za uvuvi wa kamba miti hufungwa kuanzia tarehe 1 Novemba, na ufunguliwa tarehe 1 Machi, kila mwaka. Kutokana na ukame wa takriban miaka mitatu (3), mwaka huu shughuli za uvuvi wa kamba zitafunguliwa tarehe 1 Juni. Mkakati mwingine ni kutenga maeneo ya mazalio ya samaki kama hifadhi au maeneo tengefu.

Mheshimiwa Spika, kwa kujua tatizo kubwa la uharibifu wa mazingira katika mazalio ya samaki, Nchi yetu imeridhia Mikataba ya Kimataifa kama vile: "*Biodiversity Convention*" wa mwaka 1992, *"International Law of the Sea "* ambayo iliridhiwa tarehe 30/09/1985, *"SADC Fisheries Protocol"* ambao ulisainiwa tarehe 14/8/2001, *"Convention on International Trade in Endagered Species of Wild Fauna and Flora (CITES)"* ambao uliridhiwa mwaka 1973 na kadhalika.

Aidha, nchi yetu inahakikisha kwamba samaki na viumbe wengine wa bahari wanalindwa, wanahifadhiwa na kutumiwa kwa busara kwa faida ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, aina kuna kadhaa za samaki wa maji baridi na maji chumvi wana uwezekano wa kufugwa na kukuzwa. Hii ni njia ya kuongeza uzalishaji wa samaki. Hata hivyo, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba siyo aina zote za samaki wanaweza kustahimili kutaga na kukua kwenye mazingira ya kufugwa. Kwa mfano, samaki aina ya Pweza na Ngisi hawawezi kutaga katika mazingira ya kufugwa. Kaa wameanza kufugwa kwa ajili ya biashara katika Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Muheza na kamba miti Mkoa wa Pwani Wilaya ya Mafia. Pia ifahamike kuwa teknolojia ya kukuza viumbe katika maji ya bahari siyo rahisi na gharama yake ni kubwa ukilinganisha na teknolojia ya kukuza viumbe wa maji baridi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inao mpango wa kutoa mafunzo ya ufugaji na ukuzaji wa samaki kwa wavuvi wa Ukanda wa Pwani katika Mradi wa *MACEMP. (Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba kuuliza swali ndogo la nyongeza. Kwa vile uharibifu unaotokea kwenye baharini unafanana sana na uharibifu unatokea kwenye maziwa yetu makuu hususan Ziwa Nyasa. Katika Vikao vilivyopita tuliambiwa kwamba wenzetu wa Malawi walikuwa wanamwaga chakula na kulisha samaki ili kuongeza uzalishaji wa samaki ambacho ni kitendo cha kiharamia. Je, kitendo hicho sasa kimesitishwa au bado kwa vile Wizara ilisema kwamba inashughulikia suala hilo? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kuhusu nchi ya jirani ya Malawi kuweka chakula kwenye Ziwa Nyasa ili kuongeza samaki ni suala ambalo kwa kweli linaleta uchafuzi katika Ziwa na Wizara inaendelea kufanya mawasiliano na wenzetu wa Malawi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Swali langu la nyongeza ni dogo sana. Kwa kuwa katika Bajeti iliyopita Serikali ilithubutu kutenga karibu

shilingi milioni 250 kwa ajili ya kuwatunza vyura wa Kihansi. Sasa je, Serikali haioni ni kipindi muafaka kwa sasa hivi kutenga kiasi cha fedha kwa matunzo ya samaki ambao mbali na kwamba ni chakula, lakini vilevile ni biashara nzuri kwa ajili ya *exportation?*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika**,** Wizara yangu iko katika mchakato wa kuandaa mradi wa kuwawezesha wananchi katika Wilaya za Ukanda wa Pwani na ukanda wa Ziwa Victoria kufuga samaki.

Aidha, katika Ukanda wa Pwani na Mikoa ya Visiwa vya Zanzibar na Pemba uko Mradi mkubwa wa *MACEMP* ambao nao unalenga kuwafunza wananchi katika kufuga samaki, na kuna mipango mingi pamoja na kuwawezesha wananchi kununua vifaa vya kisasa ili waweze kufuga na kutunza maliasili ambayo wanayo katika maeneo yao.

Na. 105

**"Survey" ya Kuweka Lami Barabara ya Uchumi ya Soni- Bumbuli – Dindira**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi ilipokuwa ikijibu swali na 47 mwaka 2004 iliahidi kuifanyia *Survey* barabara ya Soni – Dindira kwa kutegemea uwezo wake kifehda ili kuweza kugundua gharama ya kuijenga kwa kiwango cha lami kwa sababu barabara hiyo inahusisha pia kuendeleza zao la chai; na kwa kuwa, Serikali ilitenga shilingi milioni 30 kwa ajili ya ya kufanya *survey* hiyo:-

Je, Serikali inaweza kutoa taarifa ya *survey* hiyo na mwelekeo wake kitaalam, kiuchumi na kimazingira?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Hezekiah Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS* imeifanyia upembuzi yakinifu *feasibility study* barabara ya Mkoa wa Soni – Bumbuli hadi Dindira yenye urefu wa kilometa 47 na kazi hiyo ilikamilika mwaka wa fedha 2004/2005 na ilitekelezwa na kampuni ya Mhandisi Mshauri *Crown Tech Consult Limited* ya Dar es Salaam.

Taarifa ya tathmini iliyofanyika kwa kuzingatia vigezo vya kitaalum, kiuchumi, na kimazingira ilionekana dhahiri kuwa barabara ya Soni – Bumbuli - Dindira inakidhi vigezo vya kujengwa kwa kiwango cha changarawe na siyo kiwango cha lami.

Aidha, ilionekana kuwa kiwango cha changarawe kingetosheleza wananchi kufikia maeneo ya huduma muhimu kama shule na hospitali na kufika haraka katika masoko ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia mapendekezo ya Mhandisi Mshauri, Serikali ilikubaliana nayo hasa kwa kuzingatia kuwa idadi ya magari yanayotumia barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira ingeongezeka baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kiwango cha changarawe kutoka magari 41 kwa siku kwa mwaka 2004 hadi zaidi ya magari 106 kwa siku kwa mwaka 2010 ambapo sasa ingekidhi vigezo vya kujengwa kwa kiwango cha lami.

Aidha, faida zitokanazo na kupungua kwa gharama za matengenezo ya barabara, gharama za usafiri na usafirishaji na kupungua kwa muda wa usafiri zingekuwa kidogo katika miaka mitano ya mwanzo ikilinganishwa na gharama za ujenzi wa lami.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira inajengwa kwa kiwango cha changarawe chini ya mradi wa *STABEX* unaofadhiliwa na Jumuiya ya Ulaya *(EU)* ambapo jumla ya shilingi bilioni 1.66 zimetengwa kwa kazi hizo kama ifuatavyo:-

Kilometa 24 kutoka Soni hadi Bumbuli zitakarabatiwa kwa gharama ya shilingi milioni 769.49 na jumla ya shilingi milioni 886.11 zitatumika kwa ajili ya kukarabati sehemu ya Bumbuli hadi Dindira ambayo ni kilometa 23.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza lingine nitamwachia mwenzangu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali napenda tu kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba kwa sababu vigezo vilivyotumika ni vigezo vya kompyuta na kwamba Mheshimiwa Waziri alitembelea eneo hilo aliona mazingira yalivyo na bado nadhani Serikali ina haja ya kuangalia mazingira yaliyopo pale, kwa sababu changarawe ikinyesha mvua zitasogea. Kompyuta ina vigezo vya jumla lakini kuna hali halisi. Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kufanya *review* hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA**): Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba ni kompyuta ambayo ilitumika, lakini wataalamu walipitia maeneo hayo. Naweza nikasema kwamba kwa sababu ndio utaalamu huo na ndio maana tunatumia wataalamu katika kufanya hizi *feasibility studies*. Hatuwezi tukasema kwamba basi kwa sababu utaalamu wenu umetumia kompyuta ambayo ndiyo teknolojia ya kisasa haifai labda tuangalie tu mambo ambayo yapo kwa kuangalia kwa macho na watu ambao sisi wengine ni *layman.*

Lakini ni kweli kwamba nilipotembelea maeneo hayo niliona hali halisi niseme tu kwamba hizi tathmini ambazo zimefanywa kisayansi lazima tuendelee kuziheshimu. Lakini nieleze kwamba katika sheria mpya ya barabara ambayo nadhani mwaka huu italetwa ndani ya Bunge hili kwa ajili ya kupitishwa vigezo vya kuangalia ni namna gani barabara zinapandishwa hadhi na namna gani barabara zinajengwa kwa kiwango cha changarawe au kwa lami zitaainishwa upya na bila shaka labda mawazo hayo ya Mheshimiwa Mbunge ya kuangalia hata maeneo ya milimani kama yale ya Lushoto kama nilivyoona yanaweza yakaingizwa sasa katika vigezo vipya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Wangwe, swali la nyongeza. Lakini kabla hujauliza swali nataka nikukumbushe kwamba una deni kwangu la kutoa sahihisho na matamko yako uliyoyatoa katika Mkutano wa Nne kama nilivyoamua hivi juzi hapa Bungeni. Siku iliyobaki ni kesho baada ya

hapo ninakuwa sina njia nafungwa na Kanuni nitalipeleka suala lako kwa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kuhusiana na hilo nitaliwasilisha ofisini kwako leo.

Kuhusu swali la nyongeza. Napenda kumpongeza Naibu Waziri wa Miundombinu kwa kuitikia wito wa wananchi wa Tarime na kuja kuikagua barabara ya Nyamwaga/Arusha na akatumia muda wake wa Krismas pale tukiwa na yeye. Ningependa Serikali itoe tamko rasmi kwa wananchi wa Tarime. Je, ina mpango gani wa kuitengeneza ile barabara kwa kiwango cha lami hivi karibuni?

**SPIKA:** Sijui kama umesikia Mheshimiwa Naibu Waziri hiyo barabara iliyotajwa?

Mheshimiwa Naibu Waziri hakusikia ni barabara ya kutoka wapi kwenda wapi?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Barabara ninayoizungumzia ni barabara ya kutoka Tarime/Nyamwaga/Arusha ambayo ni barabara ya Serikali.

**SPIKA:** Hili ni swali kama jipya lakini naona Naibu Waziri yupo tayari kulijibu. Kwa ufahamu wa Bunge basi umetusaidia.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo anayoizungumzia ya kutoka Tarime/Nyamwaga/Mugumu kuelekea Arusha haijakidhi viwango vya kujengwa kwa kiwango cha lami.

Na. 106

**Uhaba wa Magari Shule za Sekondari Katika Kata za Ikuwo, Iniho na Upepo**

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Makete kiutawala ina Kata 17 ambazo kijiografia zinatenganishwa na milima na mabonde makubwa; na kwa kuwa, katika Kata za Ikuwo, Iniho na Ipepo hakuna vituo vya afya hali inayosababisha wanafunzi wa Shule za Sekondari Katani humo kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za matibabu kwenye Kata nyingine:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka magari katika shule hizo zilizo kwenye mazingira magumu ili kuwasaidia wanafunzi hao, hasa wa kike?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua kuwepo kwa tatizo la wanafunzi wa Shule za Sekondari za Kata za Ikuwo, Iniho na Ipepo kusafiri umbali mrefu kufuata huduma za

matibabu. Hii ni hali iliyopo katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo ni ukweli pia kwamba, Wizara yangu ina uhaba mkubwa wa magari hasa katika Shule za Sekondari. Nia ya Serikali ni kuona kuwa kila Shule ya Sekondari inakuwa na gari ili kurahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma muhimu katika shule. Lakini tatizo ni ufinyu wa Bajeti wa kuweza kuzipatia magari shule zote za Sekondari za Serikali ambazo kufikia mwezi wa Januari 2007 zilikuwa 1805. *(Makofi)*

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa ni kweli kabisa kwamba kwa uwezo wa Serikali hivi sasa si rahisi kununua gari kwa kila shule kwa wakati mmoja. Je, kwa nini basi Serikali isiweke utaratibu wa kusambaza *Medical Kits* kwa kila shule ambayo gharama yake ni ndogo na hii itakuwa imesaidia sana matibabu madogo madogo. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote namshukuru sana kwa mchango wake wa mawazo.

Naomba kumwarifu kwamba zoezi hilo tumelianza na *First Aid Kits* zimesambazwa na hivi sasa tunajaribu pia kuangalia namna ya kufungua vizahanati vidogo vidogo kwenye shule ili huduma za msingi ziweze kutolewa. *(Makofi)*

Na. 107

**Upungufu wa Walimu Shule za Sekondari na za Msingi Kigoma Kaskazini**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA( K.N.Y. MHE. KABWE ZUBERI ZITTO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Shule za Sekondari na za Msingi katika Jimbo la Kigoma Kaskazini hazina walimu wa kutosha na baadhi ya Shule za Sekondari zina mwalimu mmoja tu:-

(a) Je, tutatimiza malengo ya milenia kwa kufungua shule bila walimu?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka walimu wa kutosha katika shule hizo?

(c) Je, Serikali ina mpango wowote wa kutoa motisha kwa walimu wanaofundisha Shule za Mwambao wa Ziwa Tanganyika kwani zenyewe ndizo zinazoathirika zaidi na upungufu huo wa walimu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa malengo ya Milenia kwa upande wa Elimu ya Msingi na Sekondari yanafikiwa na walimu wamepatikana. Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kukabiliana na upungufu wa walimu unaotokana na ongezeko kubwa la Shule za Msingi na Sekondari. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuajiri walimu na kuwapanga katika mikoa yote kadri wanavyohitimu mafunzo ya ualimu;

(ii) Kuongeza nafasi katika vyuo vinavyotoa Stashahada na Shahada za Ualimu;

(iii) Kuajiri wahitimu wa Kidato cha Sita na Vyuo Vikuu wasio na Ualimu na kisha kuwapatia mafunzo ya ualimu;

(iv) Kuajiri walimu wastaafu kwa mkataba; na

(v) Kuongeza nafasi za Vyuo Vikuu kwa wanafunzi wanaosomea Shahada za Ualimu.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 jumla ya walimu 346 wa Shule za Msingi na 195 wa Shule za Sekondari wamepangwa katika Mkoa wa Kigoma. Ni matarajio ya Wizara kuwa wananchi na viongozi wa Mkoa wa Kigoma watajipanga kuwapokea walimu hao na kuwapanga vizuri katika Shule za Mkoa huo kulingana na upungufu uliopo katika kila shule. Wizara itaendelea kuwapanga walimu zaidi katika Mkoa wa Kigoma, likiwemo Jimbo la Kigoma Kaskazini, kadri wanavyopatikana.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inalifanyia kazi suala la kutoa motisha kwa walimu katika shule zilizoko kwenye maeneo yenye mazingira magumu katika sehemu mbalimbali nchini. Hata hivyo motisha ya kwanza ni wananchi wa Kigoma kwa kushirikiana na Serikali kujenga nyumba za walimu, maeneo ya vijiji ambako hata nyumba za kupanga hakuna. Aidha, ukarimu wa viongozi wa Kigoma kwa walimu wapya utasaidia sana walimu kutokimbia Mkoa wa Kigoma.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala moja la nyongeza.

Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yako mazuri. Jimbo la Kigoma Kaskazini liko katika Wilaya ya Kigoma Vijijini, ambako kuna matatizo mengi sana. Miundombinu hairidhishi, huduma za jamii nazo haziridhishi kama maji na afya. Vile vile maeneo mengi pia hayana umeme nahisi ni kati ya sababu ambazo zinawafanya watumishi wengi pia wakiwemo walimu wasiweze kuripoti katika vituo vyao vya kazi. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuboresha huduma hizo ili watumishi wanapopangiwa katika maeneo yenye mazingira magumu waweze kwenda? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge huduma za maji, afya na umeme hazipatikani katika Mkoa wa Kigoma hasa Kigoma Vijijini. Lakini sio Mkoa wa Kigoma peke yake, mikoa mingi sana ya pembezoni kama vile Mkoa wa Lindi, Mtwara, Ruvuma, Tabora, Singida, Shinyanga nayo ina matatizo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, tunaloomba ni wananchi kushirikiana na Serikali kuona ni jinsi gani ya kuweza kuboresha mazingira ya walimu. Kwa sababu Serikali haipati fedha za kutosha kuweza kutoa huduma hizi tunaomba wananchi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wawe na uvumilivu mpaka pale Serikali itakapokuwa na uwezo wa kuweza kutoa huduma hizi katika shule zetu.

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa sehemu ya tatu ya swali inazungumzia motisha kwa eneo la Mwambao wa Ziwa Tanganyika. Na kwa kuwa mwaka jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotembelea Mkoa wa Kigoma wakati anapewa taarifa ya Mkoa binafsi nilimweleza matatizo wanayopata watumishi wa Mwambao mwa Ziwa Tanganyika na hasa jimbo la Kigoma Kusini. Nikamweleza juhudi zinazofanywa na wananchi za kutengeneza barabara kutoka kijiji cha Ilagala mpaka Kalia.

Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu akatoa maelekezo kwa Meneja wa *TANROAD* namna ya kusaidia kukamilisha barabara hiyo. Mheshimiwa Naibu Waziri ametuambia hapa wananchi wa Mkoa wa Kigoma waonyeshe ukarimu. Wananchi hawaonyeshi tu ukarimu ila vile vile wameonyesha juhudi zao za kusimamia kutengeneza barabara hiyo. Lakini maelezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu bado hayajashughulikiwa. Je, Serikali haioni kwamba inachangia katika kutoa elimu duni Mkoa wa Kigoma kwa kutosaidia kujenga miundombinu katika mkoa ule? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua sana umuhimu wa kujenga miundombinu hasa katika mikoa ambayo iko pembezoni ukiwemo Mkoa wa Kigoma, ili kwa kweli adha ambayo inapatikana na uchumi walionao uweze kutumika vizuri kwa Watanzania wote. Ndiyo maana katika mikakati yetu tumeweka umuhimu sana hasa katika miaka mitano hii ijayo ya Ilani hii kuhakikisha kwamba mikoa ya pembezoni ukiwepo na Mkoa wa Kigoma, inajengewa miundombinu na hasa barabara kwa kiwango kinachotakiwa. Nina hakika Mheshimiwa Mbunge anaelewa mipango hiyo. Suala hapa ni lini tutakamilisha lakini kwa kweli miaka mitano ijayo Mkoa wa Kigoma, pamoja na mikoa mingine kama Rukwa, tutaendeleza mikakati hii ya kuijengea miundombinu ya barabara na miundombinu mingine muhimu. (*Makofi)*

**MHE. RAMADHANI A. MANENO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri napenda niulize swali moja la nyongeza kuhusu suala la walimu.

Kwa kuwa shule nyingi za Sekondari na walimu wengi wamepelekwa kwenye hayo mashule. Lakini mwaka jana na mwaka juzi kulitokea tatizo la mishahara kwa walimu kupelekwa wakati usio muafaka kwa maana walichelewa kuingizwa kwenye *payro*ll. Je, katika kipindi hiki Serikali ina mpango gani au ina mikakati gani ya kurahisisha kuwapelekea mishahara walimu mapema ili waweze kufanikisha kazi zao kwa ufanisi katika awamu hii ya nne ya Serikali?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naamini kabisa Waheshimiwa Wabunge wote wameona kumekuwa na mabadiliko kidogo katika kuhudumia walimu. Kwa hiyo, walimu watarajali tayari wameshakwenda mashuleni mwezi

Januari naamini hamjaona kwenye gazeti yeyote aliyesema sijapata fedha kwa sababu tulishatanguliza fedha kabla hawajakwenda. (*Makofi)*

Pili, tulishaweka *Task force* Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya kuhakikisha kwamba haipiti miezi miwili kabla mwalimu yoyote ambaye ameanza kazi awe hajaingizwa kwenye *payroll.* Kwa hiyo, kuanzia sasa naomba muamini Waheshimiwa Wabunge kwamba itakuwa si rahisi mwalimu kukaa miezi miwili kabla hajaanza kupata mshahara wake. Hata hivyo atakuwa ameshapata posho ya siku saba (7) kabla hajafika shuleni. (*Makofi)*

Atazikuta posho za siku 7 kwa Mkuu wake wa Shule. Kwa hiyo, naomba muwe na imani hiyo. *(Makofi)*

Tuna mikakati mingi tu ipo inaandaliwa walimu watapata furaha tu wavute subira. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge Mama akishasema sio ndio basi tena. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 108

**Ukosefu wa Vituo vya Polisi**

**MHE. FATMA OTHMAN ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika Kijiji cha Fumba kuna watalii wengi wanaokwenda kuangalia samaki aina ya pomboo na kwa kuwa kuna Vijiji karibu vitano kutoka Kiembesamaki mpaka Fumba ambavyo havina vituo vya Polisi:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapatia wananchi wa Vijiji hivyo vituo vya Polisi hasa ikizingatia wimbi la ujambazi na kwamba, Vijiji hivyo vingi vipo kandokando ya bahari?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kijiji cha Fumba kuna watalii wanaokwenda kuangalia samaki aina ya Pomboo. Eneo hilo pamoja na maeneo ya Vijiji vya karibu vya Kiembesamaki mpaka Fumba hakuna kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa vijiji hivyo vinatembelewa na watalii na viko kandokando ya bahari, hali ya usalama katika eneo hilo ni shwari. Wananchi na wageni wanaendelea na shughuli zao bila bughudha yoyote. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi inaendelea kufanya tathmini ya kujua mahitaji halisi ya vituo vya Polisi nchini ili iweze kutatua tatizo la kukosekana kwa vituo vya Polisi kulingana na vigezo vya Kipolisi.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa vijiji hivyo vitaendelea kuhudumiwa na Kituo cha Polisi cha Mazizini ambacho ndicho kituo kikubwa katika eneo hilo. Aidha, Jeshi la Polisi litaendelea kuimarisha doria za kawaida, na misako ya kushtukiza kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola pamoja na kuwashirikisha wananchi wa vijiji hivyo katika mpango wa Polisi Jamii ili kuhakikisha usalama katika eneo hilo.

**MHE. FATMA OTHMAN ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa kumejitokeza matokeo mengi ya ujambazi hasa kwa watalii walipofika Visiwa vya Zanzibar. Je, Jeshi la Polisi linachukua hatua gani kwa vitendo hivyo?

**NAIBU WAZIRI USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limejipanga vizuri sana pale Zanzibar kupambana na ujambazi wowote unaotokea au unaokusudia kutokea. Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba matukio yote yale yaliyotokea ya ujambazi kwa hivi sasa yamedhibitiwa vizuri katika Kisiwa kizima cha Zanzibar. Aidha, Jeshi la Polisi lina mpango maalum wa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii kule Zanzibar kuhakikisha kwamba inapambana na wimbi la uhalifu wa aina zote hasa kwa watalii.

**MHE. HAROUB S. MASOUD:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa kituo cha Polisi cha Mazizini mpaka Fumba kinazidi kilomita 15 na naelewa juhudi kubwa ambazo Wizara ya Usalama wa Raia inachukua. Lakini kuna mambo ambayo yanahitaji yarekebishwe ambayo wameyarithi katika awamu ya tatu. Kwa mfano, Kituo cha Polisi cha Mwera ambacho ni Makao Makuu ya Mkoa wa Kusini, kilomita moja tu hapo katika awamu ya tatu palijengwa Kituo cha Polisi ambacho si zaidi ya kilomita moja.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Naibu Waziri anakubaliana na mimi kwamba hapa atakaporekebisha hali hiyo aangalie mahali muhimu kusiwe na utitiri wa vituo vya Polisi mahali pamoja bila sababu za msingi?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA**: Mheshimiwa Spika, katika suala langu la msingi nilisema kwamba Serikali kupitia Jeshi la Polisi inafanya tathmini ya kina kuweza kuelewa maeneo muhimu ambayo yanahitaji kuwepo vituo vya Polisi kwa kufuata vigezo vya Kipolisi.

Nataka kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba makosa yaliyopita huko nyuma hayatatokea na sasa vituo vya Polisi vitajengwa mle tu pahali ambapo pana mahitaji halisi ya kufanya shughuli hizo.

Na. 109

**Kutofautiana Kwa Pensheni za Wanajeshi Wastaafu**

**MHE. ISSA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, askari waliostaafu mwezi Juni mwaka 2002 pensheni zao za miezi 6 ni kubwa ikilinganishwa na wale waliostaafu mwezi Juni, 2004; na kwa kuwa, utumishi wa askari hao ni sawa wa miaka 31 – 32 pamoja na vyeo vyao ni sawa:-

(a) Je, ni kigezo gani kilichotumika hata kufikia kutofautiana huko?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, hali hiyo inavunja moyo wastaafu ambao vigezo vyao ni sawa kisha wakazidiana vipato?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mbunge wa Jimbo la Mpendae, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuwalipa pensheni maafisa na askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania upo kisheria na unafuatwa. Wastaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania wanaweza kutofautiana katika malipo yao ya pensheni kutokana na sababu za msingi zifuatazo:-

(i) Muda wao wa utumishi;

(ii) Cheo alichostaafia;

(iii) Umbele wa Kupandishwa cheo (*seniority);*
(iv) Mshahara aliostaafia; na

(v) Sera inayotawala malipo ya pensheni kwa wakati likiwemo na suala la ukadiriaji wa viwango.

Mheshimiwa Spika, pamoja na sababu hizo za msingi zipo pia sababu nyingine zinazoleta tofauti ya malipo ya pensheni baina ya wastaafu. Sababu hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Muda wake ambao mstaafu alikaa kizuizini hautahesabiwa katika miaka yake ya utumishi;

(ii) Muda ambao mstaafu alitoroka kazini hautohesabiwa katika utumishi wake;

(iii) Muda ambao mstaafu alisimamishwa kazi hautahesabiwa katika miaka yake ya utumishi; na

(iv) Likizo bila ya malipo muda huo pia hautahesabiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Kassim Issa, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, vigezo vilivyotumika kuandaa pensheni za askari hao aliowaelezea ni kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya awali. Wizara ya Ulinzi ilitegemea kwamba kama hakuna tatizo lolote kwa askari waliotolewa mfano na Mheshimiwa Mbunge

linalowahusu wao wenyewe na wanalingana kwa sifa zote, basi aliyestaafu mwezi Juni, 2004 angepaswa kuwa na pensheni kubwa ikiwa kulikuwepo na kuongezeka kwa mshahara.

Hata hivyo, iwapo kuna maafisa au askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ambaye anayeona analipwa pensheni pungufu ukulinganisha na mwenzake ambaye ana sifa sawa na yeye, anaweza kumwandikia lalamiko lake Katibu Mkuu Hazina, ambaye ndie mwenye dhamana ili tatizo hilo liweze kuchunguzwa na kufanyiwa marekebisho haraka iwezekanavyo..

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haina nia ya kuwavunja moyo maafisa na askari waliotumikia nchi hii kwa uadilifu. Serikali itaendelea kufuata sheria na taratibu zilizopo na kuhakikisha kwamba kila mtumishi anatendewa haki na bila ubaguzi wa aina yoyote ile. *(Makofi)*

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ulinzi. Lakini nina swali la nyongeza.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anakubaliana nami katika maelezo yake marefu aliyotueleza hapa Bungeni kwamba sio sahihi kuhusu habari za vijana waliostaafu Jeshi na wao vyeo vyao ni sawa sawa kwamba malipo yao hayalingani hayatokani na uzito unaonyeshwa katika ulipaji?

La pili, atakubaliana na mimi katika suala hili zima la kuwalipa pensheni ya miezi sita wakairekebisha ili kuondoa uzito wa maisha ya Askari hao ikawa wanawalipa kila baada ya miezi miliwi?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba Wastaafu wanaweza kutofautiana pensheni zao ikiwa mmojawapo anatofautiana na maelezo au na vigezo nilivyoeleza. Kama vigezo ni sawasawa na hakuna nyongeza ya mshahara iliyotokea, wastaafu hawa wanapaswa kuwa na pensheni sawa sawa. Ikiwa Mheshimiwa Mbunge ana watu au Maafisa au Askari ambao wana kero hizo, basi nadhani tuonane ili tuwaone hawa Maafisa ili tuweze kulitatua tatizo hili kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni suala la pensheni kulipwa kila baada ya miezi sita. Suala hili mtakumbuka lilijadiliwa katika hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na nakumbuka kwamba wenzetu wa Wizara ya Fedha ambao ndio wenye dhamana ya kupanga miezi mingapi mingapi pensheni hiyo itoke walitoa ahadi kwamba wanalitafakari hilo suala na wanalifanyia kazi. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuvute subira ili wenzetu wa Wizara ya Fedha watakapokamilisha hiyo kazi watatupa taarifa. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumwuliza: Kwa kuwa Askari wengi hukabiliwa na hali ngumu ya kimaisha baada ya kustaafu: Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatayarisha kimaisha kabla ya kustaafu?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, katika wafanyakazi au watumishi wa Serikali nataka nilitaarifu Bunge lako Tukufu, Maafisa na Askari wa Jeshi ni miongoni mwa watumishi ambao wanapata mshahara mkubwa.

Katika matembezi yangu kwa Kambi mbalimbali nimekuwa nikiwaelezea kwamba wanajeshi hawa wajitayarishe kustaafu kwa kujijengea nyumba na wajitayarishe kwa kujiendeleza kielimu ili watakapostaafu wawe na makazi bora wao yao wenyewe pamoja na Elimu ambayo itawasaidia kupata ajira katika maeneo mengine. Sisi kama Wizara ya Ulinzi bado tunaendelea kuwasaidia wanajeshi hawa, tunaendelea kuwasomesha ili waweze kustaafu vizuri.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na sasa ni matangazo. Kwanza niseme kwamba, baada ya matangazo haya nitatoa maamuzi yangu kuhusu suala la Mwongozo na Utaratibu nilioletewa na Bwana Mengi wa *IPP* na Mheshimiwa Malima Mbunge wa Mkuranga.

Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, ameniomba niwatambulishe Waheshimiwa Madiwani na Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana (CCM) Mkoa wa Mtwara, Mheshimiwa Rashid Mwamatika. Nawaomba wageni wasimame ili Wabunge waweze kuwatambua. *(Makofi)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Madiwani na watumishi. Kwa hakika mnapendeza hata nguo zenu. Kwa tangazo hili, pia namwomba Mkurugenzi wa Halmashauri ya Urambo aige mfano mzuri wa Tandahimba. *(Kicheko)*

Wageni wengine ni Waheshimiwa Madiwani na Makatibu wa *UWT* kutoka Mkoa wa Mbeya waliomsindikiza Mheshimiwa Florence Kyendesya. Wageni hao ni Mheshimiwa Tuli Mwang'amba, Mheshimiwa Thabita Mwakabaka, Lucy Singela, Shiza Mwakatundu, Joyce Bilali na Amina Kango. Nawaomba wasimame, wale pale. Ahsanteni sana na tunawashukuru kwa kuweza kumpa moyo na nguvu Mbunge mpya. *(Makofi).*

Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko Naibu Waziri wa Habari ameniomba niwatambulishe wageni wake ambao ni wanafunzi 14 na Walimu wawili wa Shule ya Sekondari Mwilavya. Hili jina linaonyesha ni zile Sekondari mpya mpya kutoka Jimbo la Kasulu Mashariki, ahsante sana. Karibuni sana hapa Dodoma na poleni kwa safari ndefu sana kutoka Kasulu. Sijui mlipita njia gani, lakini tunashukuru mpo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Thomas Abson Mwang'onda, Mbunge wa kuteuliwa, anaomba nimtambulishe wafuatao:- Mke wake Sophia Abson Mwang'onda, yule pale. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Madiwani kutoka Mkoa wa Mbeya, Katibu Mkuu wa *UWT* Mkoa wa Mbeya na Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya Mbeya Mjini *UWT*. Ahsante sana karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lubeleje, ameniomba nitangaze kuwepo kwa wageni wake, Bwana Stanley Noha na Bwana Edward Maghuku na Thimoth Mwaja. Anasema hapa wote ni shemeji zake. Kwa majina haya Mheshimiwa Lubeleje una mke mmoja maana majina haya pengine na wao wameoa kwako hatujui. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Juma Killimbah na Diana Chilolo, wameniomba nitangaze kuwepo kwa wageni wao ambao ni akina mama wajasiriamali kutoka Wilaya ya Iramba kikundi cha

*(MWAMAKI)*. Mwanamke na Maendeleo Kiomboi wamekuja kwenye maonyesho ya *SIDO* hapa Dodoma. Naomba msimame tafadhali, wale pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rosemary Kirigini ameniomba nitangaze kuwepo kwa mgeni wake ambaye pia ni mdogo wake na ni Kamanda wa Vijana CCM Kata ya Kimara, Bwana Paul Kirigini. Yule pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Dr. Cyril Chami na Mbunge wa Moshi Vijijini anao wageni wake, Mama Clara Mandara na Mama Flora Walilo. Hawa ni wakazi wa Jimboni kwake, lakini pia amenifahamisha kwamba akinamama hawa ni machachari na walihusika sana na ushindi wa Mheshimiwa Chami. Hongera sana.

Wapo pia wanafunzi 19 na Walimu wanne wa *Dar es Salaam Independent School.* Wale pale! Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mikutano ya Kamati kukutana, Semina ya Maboresho ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Lubeleje ameomba kwamba Wajumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, kutakuwa na Semina hiyo itakayofanyika leo tarehe 8 Februari 2007 katika Ukumbi Na. 428 Ghorofa ya nne saa 7.00 Mchana.

Mheshimiwa Castro Ligalama ameniomba nitangaze kwamba Wajumbe wote wa Bodi ya Mfuko wa Uwezeshaji wakutane leo katika Jengo la Utawala saa 7.00 mchana.

Mwenyekiti wa Manaibu Mawaziri wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. Maua Daftari, anaomba Manaibu Waziri wenzake wakutane leo saa 2.00 Usiku pale *Nam Hotel*. Hawa wenzetu wana utaratibu mzuri kweli. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, ameniomba niwatangazie Wajumbe wa *TAPAC* kuhusu kwenda kula chakula cha mchana na watoto yatima wa Kijiji cha Matumaini Dodoma leo saa 7.00 mchana. Usafiri umeandaliwa na Wajumbe wakutane mbele ya Jengo la Utawala.

Mheshimiwa Gedion Cheyo - Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi anaomba Wajumbe wakutane saa 5.30 asubuhi hii Ukumbi Na. 227.

Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii anaomba niwatangazie kuwa kutakuwa na Kikao cha pamoja cha Kamati ya Maendeleo ya Jamii na Kamati ya Huduma za Jamii saa 5.00 Asubuhi katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa William Kusila, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama anaomba Wajumbe wote wa Kamati hiyo wakutane leo tarehe nane kuanzia saa 5.00 asubuhi katika Ukumbi Na. 219 Jengo la Utawala.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika - Mheshimiwa Chiza, anaomba niwatangazie Waheshimiwa kuwa fomu za maombi ya Mikopo kutoka katika Mfuko wa Pembejeo zinapatikana katika Ofisi za Kilimo za Wilaya zote. Hata hivyo amewaandalia Waheshimiwa Wabunge nakala zao ili iwe rahisi kufuatilia. Fomu watakazogawiwa leo ni zifuatazo:-

Maombi ya Mkopo wa kununua na kukarabati trekta na Maombi ya Mkopo wa kununulia pembejeo. Ahsante na hongera sana Wizara ya Kilimo kwa kurahisisha upatikanaji wa vitu muhimu kama hivyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nikishamaliza kusoma maamuzi yangu kuhusu suala hili la Bwana Reginald Mengi na Mheshimiwa Adam Malima, itanibidi nitoke nitamwachia Naibu Spika.

Kwa hiyo, nadhani tutafanya utaratibu kwa sababu nadhani itachukua dakika 20 hivi, ili Kanuni itenguliwe kuongeza muda kidogo kama wa nusu saa kutoa nafasi kwa shughuli zile nyingine zilizopangwa ziweze kufanyika bila kuwazuia watu kuweza kuchangia kama ilivyopangwa na ilivyoahidiwa na Naibu Spika jana.

**MAAMUZI YA SPIKA KUHUSU MALALAMIKO YA BWANA REGINALD A. MENGI NA MHESHIMIWA ADAM K. A. MALIMA KUHUSIANA NA MATUKIO YA AGOSTI, 2006 WAKATI WA MKUTANO WA NNE WA BUNGE**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Maelezo (*facts*) Maamuzi yangu ya leo yanatokana na malalamiko yaliyowasilishwa kwangu na Bwana Reginald A. Mengi tarehe 6 Agosti, 2006 akilalamika kwamba, tarehe 2 Agosti, 2006 wakati akichangia hoja ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo Bungeni, Mheshimiwa Adam K. A. Malima, Mbunge wa Jimbo la Mkuranga, pamoja na mambo mengine, alishutumu matumizi mabaya ya televisheni ya '*Independent Television (ITV)'* pamoja na mmiliki wake kwa kuwa siku hiyo Mheshimiwa Malima siku hiyo alitamka Bungeni kwamba: Nanukuu *Hansard*:

"Nimewahi kushuhudia Mimi Rais wa Jamhuri ya Muungano ana habari nzito kwenye Taarifa ya Habari ya saa mbili anapewa dakika moja Na nusu, Waziri Mkuu anataka kuzungumzia njaa anapewa dakika moja na nusu, watoto wa *'Primary'* wanakuja kutoka Zanzibar kutembelea Kiwanda cha *Coca-Cola* wanapewa dakika kumi. Mmiliki wa *TV* anakwenda kuongea na watoto wa Madrasa Msasani kwa ajili ya kugombana na Sheikh mmoja anapewa dakika kumi." (*Hansard* ya tarehe 2 Agosti, 2006).

Katika barua yake hiyo ya tarehe 6 Agosti 2006 Bwana Mengi alidai kuwa, alikuwa ameshutumiwa mahali ambapo hawezi kujitetea, na kwamba, shutuma hizo zilizotolewa na Mheshimiwa Adam K. A. Malima (Mb.) dhidi yake na *ITV* hazikuwa na ukweli wala msingi wowote. Katika malalamiko yake, Bwana Mengi alifafanua kwamba:-
" Japokuwa Mheshimiwa Malima hakutaja Ni kituo gani cha televisheni, Ni wazi kwamba, Kwa taathira yake, *(by implication)* ni dhahiri kwamba, kauli ya Mhe. Malima ilikuwa inaishutumu *ITV* na Mmiliki wake Kwa sababu, *ITV* ndiyo iliyorusha hewani vipindi vya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusiana na suala la njaa, watoto wa shule kutoka Zanzibar kutembelea Kiwanda cha *Coca-Cola* na watoto wa Madrasa Msasani." Mwisho wa kunukuu.

Katika barua yake, hiyo Bwana Mengi aliendelea kulalamika kwamba: "Kama Mheshimiwa Malima alivyotarajia, uongo huo umewafikia wanajamii na kwa vyovyote vile tunaonekana mbele yao kama wadharau wakubwa wa viongozi wa Kitaifa na kama watumiaji wa chombo cha habari kwa manufaa binafsi badala ya Manufaa ya Umma. Mimi na *ITV* tumefadhaishwa sana na uongo huo." Mwisho wa kunukuu.

Pamoja na kuwasilisha malalamiko hayo kwangu, tarehe hiyo hiyo, Bw. Mengi alitoa taarifa kwa vyombo vya habari *(Press Release)* hususan katika vile vya *IPP* kukanusha tuhuma za Mheshimiwa Malima alizozitoa Bungeni. Katika taarifa hiyo, pamoja na mambo mengine, ilidaiwa kwamba:
"Shutuma hizo zilikuwa ni za uongo uliotungwa na Mheshimiwa Malima, kwa maslahi yake binafsi ya Mheshimiwa Malima." Mwisho wa kunukuu.

Baada ya Taarifa ya Bwana Mengi kwa vyombo vya habari kurushwa hewani na *ITV*, Mheshimiwa Malima naye aliwasilisha kwangu malalamiko yake tarehe 7 Agosti, 2006, akidai kuwa matangazo hayo ya Bwana Mengi yamemdhalilisha, na akaendelea kusema hivi:

"Ni wajibu wetu kama Wabunge kuhoji mwenendo wa masuala yote ya Kitaifa, ya Mkoa, ya Wilaya hadi Kijiji, masuala ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kadhalika, kwa manufaa ya maendeleo ya Watanzania wote bila kubagua na mimi niliamini kwamba, nilifanya hivyo kwa kuzingatia haki, maadili na taratibu kama zilivyoainishwa kwa ajili ya Wabunge wa Bunge hili." Mwisho wa kunukuu.

Katika barua yake ya malalamiko, Mheshimiwa Malima aliendelea kudai kwamba:- Nanukuu: "Katika utekelezaji wa majukumu haya, Katiba, Kanuni za Bunge na Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge ya Mwaka 1988, zimeweka mwongozo wa wazi kuhusu majukumu ya Mbunge na nafasi ya utekelezaji wa majukumu yake." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Malima alihitimisha malalamiko yake kwa kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu hatua stahili anazopaswa kuchukua yeye binafsi kama Mbunge kuhusu matangazo ya *IPP Media* dhidi yake au hatua zinazoweza kuchukuliwa na Bunge, kwa niaba yake.

Baada ya kupokea malalamiko hayo na kubaini kuwa yanahusu Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, niliamua kuyapeleka kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, ili Kamati hiyo ifanye uchunguzi na kunipa ushauri wa jinsi ya kuyashughulikia. Baada ya Kamati hiyo kukamilisha kazi na kukabidhi taarifa hiyo yake ya ushauri kwangu, leo nimeona ni wakati muafaka wa kutoa maamuzi yangu kuhusu malalamiko hayo mawili.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijatoa maamuzi yangu, napenda kuwashukuru kwa dhati Mheshimiwa Mwenyekiti Juma S. Nh'unga na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa umakini wao na kwa kutumia utaratibu wa haki katika kuchunguza na hatimaye kukamilisha kazi yao na kutoa ushauri wao kwangu. Muda waliotumia na gharama zake visingeweza kuepukwa. Umma wa Watanzania unapaswa kuelewa kwamba, katika kushughulikia suala lolote kama hili linalolenga kuweka misingi ya utawala bora katika nchi yetu, gharama haiepukiki. *(Makofi)*

Kwa kuwa, malalamiko yote mawili yanahusu Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge (*Parliamentary Privilege*); na kwa kuwa, suala hilo halijaeleweka sana kwa wananchi walio wengi hapa nchini, na pia kwa ajili kuweka uelewa mzuri wa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla, nimeona ni vyema katika uamuzi wangu, nianze kwa kutoa maelezo na ufafanuzi kuhusu maana na madhumuni ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nizungumzie maana na madhumuni ya Kinga Haki na Madaraka ya Bunge *(Parliamentary Privilege).* Katika Mabunge kadhaa bado upo mkanganyiko kuhusu maana halisi ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge *(Parliamentary Privilege)*.

Katika maamuzi yangu, kwa ujumla wake, nitaziita haki hizo "Haki za Bunge". Haki hizo aghalabu hupewa maana na tafsiri ambayo ni potofu. Kamati Teule ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge la Makabwela la Uingereza *(House of Commons)* ilitoa tamko lifuatalo kuhususiana na *Parlimentary Privilege:*- Nanukuu:

*"The word "privilege" has in modern times acquired a meaning wholly different from its traditional parliamentary connotation. In consequence, its use could convey to the Public generally the false impression that, Members are, and desire to be, a "privileged class". It is out of keeping with modern ideas of Parliament as a place of wok and of the status of its Members as citizens who have been elected to do within that place of work their duty as representatives of those who elected them".* Linanukuliwa kutoka kwenye *House of Commons Selected Committee on Parliamentary Privilege ya mwaka 1967.*

Mwandishi maarufu na mtaalam aliyebobea na anayenukuliwa sana kuhusiana na Sheria, Kanuni na taratibu za masuala ya Bunge Bw. *Erskine May* wa Uingereza anaeleza kwamba, tafsiri ya "*Haki za Bunge"* katika ujumla wake *(Parliamentary Privilege),* ni majumuisho ya haki zote za kipekee za Bunge lenyewe na za kila Mbunge binafsi, ambazo bila hizo, Bunge lenyewe au Wabunge, hawataweza kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Kwa ajili ya ufasaha zaidi, napenda kunukuu tafrisi hiyo katika lugha iliyotumika na Mwandishi huyo ifuatavyo kwa lugha ya Kiingereza:- Nanukuu:*"Parliamentary privilege is the sum total of the peculiar rights enjoyed by each House collectively and by Members of each House individually, without which they could not discharge their functions, and which exceed those possessed by other bodies or individuals".*

Waheshimiwa Wabunge, Haki hizi zinatambuliwa pia katika Sheria za Mambo ya Katiba (*Constitutional law*) kwamba, kila Bunge linatekeleza haki ambazo zinahesabiwa kuwa ni za muhimu kwa hadhi na kwa kuliwezesha Bunge kufanya kazi (*Each House exercises certain powers and privileges which are regarded as essential to the dignity and proper functioning of Parliament).*

**MBUNGE FULANI:** *That is interested.*

**SPIKA:** Malengo na madhumuni ya msingi ya haki za Bunge (*Parliamentary privilege*) ni kuliwezesha Bunge na Wabunge kutekeleza majukumu yao ya Kikatiba. Nimnukuu tena Bwana *Erskine May* huyu mtaalamu wa mambo hayo, anatoa ufafanuzi zaidi kuhusu umuhimu, malengo na madhumuni ya haki za Bunge kwa maneno yafuatayo:-

*"Certain rights and immunities such as freedom from arrest or freedom of speech belong primarily to individual Members of the House and exist because the House cannot perform its functions without unimpended use of the services of its Members. Other such rights and immunities such as the power to punish for contempt and the power to regulate its own constitution belong primarily to the House as a collective body, for the protection of its members and the vindication of its own authority and dignity. Fundamentally, however, it is only as a*

*means to the effective discharge of the collective functions of the House the individual privileges are enjoyed by Members.*

*The term "privilege" is therefore used to mean those fundamental rights absolutely necessary for the exercise and due execution of constitutional powers and functions of the House".*

Waheshimiwa Wabunge, Kwa tafsiri hii ni kwamba, "Haki za Bunge" ni zile haki ambazo ni za lazima kabisa kwa hadhi na heshima ya Bunge, kwa ajili ya kutekeleza majukumu na madaraka yake ya Kikatiba ipasavyo. Kwa maneno mengine, haki za Bunge ni nyenzo muhimu za kuliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake na Bunge linaweza kutekeleza wajibu wake wa kikatiba ipasavyo, pale tu ambapo haki hizo za Bunge zinahifadhi mamlaka, hadhi na heshima inayolistahili Bunge.

Aidha, haki hizo zinawalinda Wabunge wanapotekeleza majukumu yao ya Kibunge, ndani ya Bunge na Kamati zake, dhidi ya kubanwa kwa namna yoyote ile na Mihimili mingine ya Dola, yaani Utawala *(Executive)* na Mahakama *(Legislature)* na hata dhidi ya vyombo vingine na watu binafsi. Kwa uhuru huo Wabunge wanawezeshwa kutekeleza kazi zao ndani ya Bunge bila vikwazo *(in order that they may be able to perform their duties in Parliament without let or hindrance).*

Kitabu cha *House of Representatives Practice6* cha Australia kinafafanua zaidi kuhusu maana ya "*Haki za Bunge*" kule Australia kwa maneno yafuatayo:- Nitanukuu tena kwa Kiingereza:

*"Parliamentary Privilege relates to the rights and immunities which belong to the Parliament, its Members and Others, which are essential for the operation of the Parliament. These rights and immunities allow the Parliament to meet and carry out its proper constitutional role, for Members to discharge their responsibilities to their constituents and for others properly involved in the parliamentary process to carry out their duties and responsibilities without obstruction or fear of prosecution".*

Aidha, Bunge la Makabwela la Uingereza *(House of Commons) limetoa* ufafanuzi wa ziada kuhusu maana ya *"Haki za Bunge*" kwa maneno yafuatayo: *"Privileges are not the prerogative of Members in their personal capacities. In so far as the House claims and members enjoy those rights and immunities which are grouped under the general description of "privileges", they are claimed and enjoyed by the House in its corporate capacity and by its members on behalf of the citizens whom they represent"*

Waheshimiwa Wabunge, ili haki za Bunge ziwe na maana, ni lazima zihifadhiwe na kutiliwa nguvu iwapo zitavunjwa au kupuuzwa. Kwa ajili hiyo, kuvunja au kupuuza haki za Bunge huchukuliwa kuwa ni kosa la kuvunja haki za Bunge *(breach of privilege)* au mara nyingine huitwa kosa la kudharau *(contempt)*; makosa ambayo hustahili adhabu kwa mujibu wa sheria.

Bwana Erskine May anatoa ufafanuzi kuhusu dhana hiyo kama ifuatavyo: *"When any of these rights and immunities, both of the Members, individually and of the Assembly, in its collective capacity, are disregarded or breached by any individual or authority, the offence is*

*called a breach, and is punishable under the law of Parliament. The House also have the right to punish actions, which, while not breaches of any specific privilege, are offences against its authority or dignity, such as disobedience to its legitimate commands or libels upon itself, its officers or its Members. Such actions, though often called "breach of privilege" are more properly distinguished as contempts."*

Kihistoria, chimbuko la haki za Bunge ni harakati za mapambano kati ya Bunge la Makabwela la Uingereza *(House of Commons)* wakati wa enzi ya Malkia Elizabeth wa Kwanza katika karne ya 16 ya kudai uhuru wa Bunge kama chombo cha uwakilishi, wa kutoingiliwa madaraka yake na Mihimili ya utawala *(Executive)* au na Mahakama *(Judiciary)* katika kutekeleza majukumu yake.

Harakati hizo zilitokana na kuwepo kwa dhana ya mgawanyo wa madaraka *(separation of powers)* ambapo, kama ilivyo kwa Mihimili hiyo miwili ya Dola, Bunge nalo lilitakiwa liwe huru kikamilifu, na lisiingiliwe madaraka yake kwa namna yoyote ile, katika utekelezaji wa madaraka na majukumu yake.

Harakati za mapambano hayo zilitokana pia na Watawala, hususan Mfalme/Malkia wa Uingereza kutaka kulifanya Bunge kuwa kama ni chombo cha kutekeleza amri na malengo yake binafsi.

Haki za msingi za kwanza ambazo Bunge la Makabwela la Uingereza *(House of Commons)* lilizidai na hatimaye zikakubaliwa, ni haki ya Wabunge kutokukamatwa na kuwekwa korokoroni kutokana na matamshi yaliyotolewa na Mbunge husika ndani ya Bunge *(freedom from arrest)*. *(Makofi)*

Haki nyingine muhimu iliyodaiwa na Bunge hilo na kukubaliwa ni uhuru wa majadiliano Bungeni *(freedom of speech)*. Haki hizi muhimu kwa sasa zimetambuliwa na kuheshimiwa na Mahakama *(Judiciary)* na utawala *(Executive)*.

Waheshimiwa Wabunge, haki hizi ni muhimu kwa sababu bila hizo, Bunge lingeweza kuzuiliwa lisikutane kwa Wabunge kukamatwa, na pia Bunge lingezuiliwa na kushindwa kujadili masuala mbalimbali, hususan yale ya kuikosoa na kuisimamia Serikali, kwa sababu, katika kipindi kirefu cha mapambano ya kudai haki hizo, kulikuwepo na matukio mengi ya Wabunge kukamatwa na kuweka korokoroni, kwa amri ya Mfalme/Malkia, kutokana na kauli walizozitoa Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, napenda nizungumzie Sheria ya Haki *(Bill of Rights)* ya Uingereza ya mwaka 1689. Mapambano kati ya Bunge na Watawala kwa upande mmoja na kati ya Bunge na Mahakama kwa upande mwingine nchini Uingereza, yalisababisha itungwe sheria ya Haki *(Bill of Rights)* mnamo mwaka 1689.

Ibara ya IX ya Sheria hiyo iliweka na kuhifadhi uhuru wa majadiliano na haki ya kutokukamatwa na kuwekwa korokoroni, katika Bunge la Uingereza. Ibara hiyo inatamka ifuatavyo:- Nanukuu:

*"The freedom of speech and debates or proceedings in Parliament ought not to be impeached or questioned in any court or place outside of Parliament."* Mwisho wa kunukuu.

*Rafiki yetu Erskine May* amefafanua kwamba maneno "*freedom of speech* yana maana kwamba, kauli zinazotolewa na Wabunge Bungeni zinalindwa kisheria *(legal immunity)*, hususan

kwa yale ambayo Mbunge anayatamka akiamini kuwa ni sahihi, hata kama anachotamka Mbunge kitamwathiri mtu mwingine yeyote. *(Makofi)*

Kwa mujibu wa kinga hiyo, Mbunge hawezi baada ya kuongea Bungeni akafunguliwa mashtaka Mahakamani kwa kosa lolote la kukashifu *(libel)*

Katika kusisitiza umuhimu wa uhuru wa majadiliano Bungeni, Kamati Teule ya Haki za Bunge ya Bunge la Uingereza, ilitamka yafuatayo katika taarifa yake: *"Parliament is a legislative and deliberative assembly. Its main constitutional role is to enact law and to grant supply. Parliament is also 'the grand inquest of the nation'; it is the forum where any grievance may be aired, however small or great. It is the place where the government is called to account by representatives of the whole Nation. Freedom of speech is central to Parliament's role. Members must be able to speak and criticize without fear of penalty. This is fundamental to the effective working of Parliament, and is achieved by the primary parliamentary privilege: the absolute protection of 'proceedings in parliament' guaranteed by article 9 of the Bill of Rights 1689. Members are not exposed to any civil or criminal liabilities in respect of what they say or do in the course of proceedings in Parliament."*

Waheshimiwa Wabunge, sambamba na kudai na kutetea haki hizo, Bunge la Uingereza lilidai pia haki ya Bunge ya kuzilinda haki hizo lenyewe kwa kuzifanyia maamuzi na kutoa adhabu pale zinapokiukwa au kupuuzwa, bila kupitia chombo kingine kama vile Serikali au Mahakama. Kutilia nguvu haki za Bunge kwa kuwachukulia hatua watu wanaozikiuka au kuzipuuza haki hizi, kunafanana na mamlaka ya Mahakama ya kuwaadhibu wale wanaofanya kosa kudharau amri za Mahakama *(contempt of court)*.

Waheshimiwa Wabunge, napenda nizungumzie Haki za Bunge katika Bunge la Tanzania sasa. Kutokana na sababu za kihistoria nilizozielezea kwa kirefu hapo juu, Bunge la Jamhuri ya Muungano, kama yalivyo mabunge mengi ya Nchi za Jumuiya ya Madola, linafuata misingi ya Bunge la Uingereza *(Westminster model)*. *(Makofi)*

Kutokana na historia hiyo, mfumo wa utawala na hususan wa Bunge la Tanzania na taratibu za uendeshaji wa shughuli zake unafuata misingi ya mfumo wa Bunge la Uingereza.

Haki za Bunge zilizotumiwa na kutambuliwa na chombo cha kwanza cha kutunga sheria wakati wa utawala wa Uingereza nchini *[The Legislative Council (LEGCO)]* ziliwekwa na sheria iliyoitwa, *' The Legislative Council (Powers and Privileges) Ordinance, (Cap.359)'* ya mwaka 1955.

Sheria hiyo iliendelea kutumika hadi mwaka 1988 ilipotungwa sheria nyingine ambayo inatumika hivi sasa yaani, *The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, 1988 (No.3 of 1988)*."

Nchini Tanzania, haki za Bunge ziliwekwa rasmi katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano, 1977 kupitia marekebisho ya Katiba ya mwaka 1984 chini ya Ibara ya 100. Aidha, Ibara ya 101 ya Katiba hiyo iliweka msingi wa kuweka sheria ya kuhifadhi haki za Bunge. Ibara hizo mbili zinatamka ifuatavyo:-

"100.-(1) Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano, au katika Mahakama au mahali penginepo nje ya Bunge.

(2) Bila ya kuathiri Katiba hii au masharti ya sheria nyingine yoyote inayohusika, Mbunge yeyote hatashitakiwa au kufunguliwa shauri la madai Mahakamani kutokana na jambo lolote alilolisema au kulifanya ndani ya Bunge au aliloleta Bungeni kwa njia ya maombi, Muswada, hoja au vinginevyo.

101.-(1) Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya kuwezesha Mahakama na sheria kuhifadhi na kutilia nguvu uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu wa shughuli katika Bunge ambao kwa mujibu wa ibara ya 100 umedhaminiwa na Katiba hii.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nizungumzie Haki za Bunge kwa mujibu wa Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge ya Mwaka 1988 (*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, 1988)*

Waheshimiwa Wabunge, Sheria hii ilitungwa kwa madhumuni ya kutekeleza Ibara ya 101 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, 1977. Haki za Bunge zinazotambuliwa na Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, kimsingi ni haki zile zile na madaraka yale yale yanayotambuliwa kama ni haki na madaraka ya Bunge katika Mabunge mengi ya nchi za Jumuiya ya Madola. Sheria hii, pamoja na mambo mengine, inatamka chini ya kifungu cha Tatu na cha Tano kama ifuatavyo:-

"*3. There shall be freedom of speech and debate in the Assembly and such freedom of speech and debate shall not be liable to be questioned in any Court or place outside the Assembly."*

*'5. No civil or criminal proceedings may be instituted against any member for words spoken before or written in a report to the Assembly or a committee or by reason of any matter or thing brought by him therein by petition, bill or motion or otherwise or for words spoken or act done bona fide in pursuance of a decision or proceedings of the Assembly or a committee."*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuelezea misingi na kutoa ufafanuzi muhimu kuhusu haki za Bunge, sasa napenda kuwarudisha kwenye suala husika lililopo mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ufafanuzi kuhusu malalamiko husika. Napenda ieleweke wazi kuwa, kilichowasilishwa kwangu na Bwana. Mengi na Mheshimiwa Malima siyo 'kesi' kama wengi wanavyofikiria. Mawazo hayo ni potofu, kwa sababu, wahusika hao wawili walileta malalamiko kwangu, kila mmoja akimlalamikia mwenzake, kama nilivyokwisha kuelezea kwenye sehemu ya kwanza hapo juu.

Waheshimiwa Wabunge, malalamiko hayo sio 'kesi' kama ambavyo watu wengi wamekuwa wakipotosha; na tafsiri hiyo potofu imewafanya watu wengi, kukaa mkao wa kungojea 'ushindi', au uamuzi unaotamka kuwa Bwana Mengi au Mheshimiwa Malima kashinda au kashindwa, kitu hicho hakipo. *(Makofi)*

Msimamo wa sheria kuhusiana na suala hili umewekwa na tafsiri ya Ibara ya 100(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, ikisomwa pamoja na Kifungu cha 3 na cha 5 cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ya mwaka 1988 na Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Bunge (Toleo la 2004). Ibara ya 100(1) ya Katiba inatamka ifuatavyo:-

*"Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano au katika Mahakama au mahali penginepo nje ya Bunge."*

Kifungu cha Tatu cha sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, 1988 (*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, 1988*) kinatamka kwamba:- "*There shall be freedom of speech and debate in the Assembly and such freedom of speech and debate shall not be liable to be questioned in any court or place outside the Assembly."*

Kifungu cha Tano cha sheria hiyo kinatamka kwamba:- "*No civil or criminal proceeding shall be instituted against any member for words spoken before or written in a report to the Assembly or a Committee or by reason of any matter or thing brought by him therein by petition, bill or motion or otherwise or for words spoken or act done in bona fide pursuance of a decision or proceeding of the Assembly or a Committee."*

Waheshimiwa Wabunge, ili kutoa uamuzi sahihi na wa haki kuhusu suala hili, hoja za msingi (*issue*s) za kujiuliza nilizozibaini na kuzijibu ni zifuatazo:-

(a) Hoja ya kwanza ni je, uhuru unaohakikishwa na Ibara ya 100(1) ya Katiba na Kifungu cha 3 cha sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, 1988 unayo au hauna mipaka (*absolute freedom)*;? na kama una mipaka, mipaka hiyo ni ipi?

(b) Hoja ya pili ni je, matamshi aliyoyatoa Mhe. Malima, Bungeni, yamepewa kinga na Ibara ya 100(1) ya Katiba na Kifungu cha 3 cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, 1988?

(c) Hoja ya tatu ni je, Bwana Mengi alikuwa na haki ya kuhoji juu ya matamshi ya Mhe. Malima aliyoyatoa Bungeni? Kama alikuwa na haki hiyo alitakiwa ahoji kwa utaratibu upi?

(d) Hoja ya nne na mwisho ni je, utaratibu wa Bunge, kwa mujibu wa sheria na Kanuni za Bunge, unatoa au hautoi, haki na utaratibu wa mtu asiye Mbunge, kujitetea au kujibu shutuma zinazotolewa na Mbunge dhidi yake ndani ya Bunge?

Waheshimiwa Wabunge, sasa nataka nizungumzie kuhusu Taarifa na ushauri wa Kamati ya Kinga, Maadili na Madaraka ya Bunge. Baada ya Kamati ya Kinga, Maadili na Madaraka ya Bunge kukamilisha uchunguzi wake, iliwasilisha taarifa yake kwangu pamoja na taarifa ya maoni tofauti (*dissenting views*) za wajumbe wake wawili.

Katika taarifa hiyo na niseme tu na mmoja kajiuzulu, Kamati ya Kinga, Maadili na Madaraka ya Bunge Kamati iliridhika kuwa Mheshimiwa Adam K.A. Malima (Mb.), hakusema uongo ndani ya Bunge, na kwamba hakukuwa na uthibitisho wowote kuwa ana maslahi binafsi na kile alichokisema Bungeni. *(Makofi)*

Kwa matokeo hayo, Kamati ilishauri Bwana Reginald Mengi aarifiwe kuhusu matokeo hayo ya uchunguzi wa Kamati, na pia Bwana Mengi ashauriwe kuwa makini katika matumizi ya vyombo vya habari, hasa vile anavyovimiliki. *(Makofi)*

Aidha, Kamati ilishauri kuwa, Mheshimiwa Malima ajibiwe maombi yake ya Mwongozo wa Spika kuwa, alipokuwa anachangia Bungeni tarehe 2 Agosti, 2006, alikuwa sahihi kulingana na misingi ya Katiba, Sheria na Kanuni za Bunge na kwamba, akipenda afuate taratibu zaidi za kisheria, kudadi haki yake kwa kuwa, kushambulia mchango wa Mbunge mmoja mmoja wakati anatekeleza majukumu yake ya kikatiba si halali na mhusika wa kutenda kosa hilo anaweza kushtakiwa Mahakamani.

Pamoja na ushauri huo wa Kamati, ushauri tofauti (*dissenting views*) uliotolewa na Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka (Mb.) na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela (Mb.) ambao ulibainisha kwamba, kutokana na Wabunge wote waliochangia hoja pamoja na Mheshimiwa Waziri, kuhoji utendaji kazi wa vyombo vya habari vya *IPP* katika kulishupalia suala la *NSSF* na *Quality Group*, madai ya Mheshimiwa Malima dhidi ya *ITV* na mmiliki wake, Bwana Mengi yalikuwa tofauti.

Mheshimwia Malima katika mchango wake alilinganisha muda wanaopewa viongozi na anaojipa mmiliki. Kwa suala hilo Waheshimiwa Ole-Sendeka na Anne Malecela waliona kuwa Bwana Mengi alikuwa sahihi kulalamika dhidi ya shutuma zilizotolewa na Mheshimiwa Malima.

Taarifa ya Wabunge hao inaendelea kubainisha kwamba, madai yaliyotolewa na Mheshimiwa Malima kwamba, *"ameshuhudia Rais na Waziri Mkuu wanapewa dakika moja na nusu kila mmoja na mmiliki wa ITV anapewa dakika kumi"* kwa kila tukio alilolitaja hayakuwa na ukweli wowote, kwa sababu pia Mheshimiwa Malima hakuweza kuyathibitisha hata kwa kanda za televisheni alizozileta mwenyewe kwenye Kamati. *(Makofi)*

Waheshimiwa hao wanabainisha pia kuwa, uchunguzi wa Kamati ya Kinga, Maadili na Madaraka ya Bunge umebaini kwamba, si kweli kuwa Mheshimiwa Malima amewahi kushuhudia Rais na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanapewa dakika moja na nusu kila mmoja na mmiliki wa *ITV* anapewa dakika kumi wakati wa taarifa ya habari ya *ITV* ya saa mbili usiku.

Katika kuthibitisha hilo, Waheshimiwa hao wanasema, katika maelezo yake wakati wa uchunguzi wa Kamati, Mheshimiwa Malima alipoulizwa alitamka kwamba hakupata hata wakati mmoja, kuangalia saa kuthibitisha muda aliopewa Rais, Waziri Mkuu na mmiliki wa *ITV*.

Waheshimiwa hao wawili yaani Ole-Sendeka na Mama Malecela wanaendelea kusema kwamba, kwa kuwa Mheshimiwa Malima hakuweza kuthibitisha ukweli wa madai yake kuhusu muda *(air time)* aliokuwa anauzungumzia Bungeni na kwa kuwa kwa matamshi kuwa *"nimeshuhudia",* Mheshimiwa Malima alikuwa na nia ya kulifanya Bunge liamini maneno aliyokuwa anasema Bungeni, huku akijua wazi kuwa hakuwa na uhakika wa ukweli wa anachokisema, ni dhahiri Mheshimiwa Malima alikiuka Kanuni ya 50(1) inayokataza kusema uwongo Bungeni na inayomtaka Mbunge kuwa na hakika kwamba maelezo anayoyatoa Bungeni ni sahihi na siyo mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu. *(Makofi)*

Waheshimiwa hao wanahitimisha taarifa zao za maoni tofauti kwa kutoa ushauri kwamba, kwa ukiukaji huo wa Kanuni ya 50(1) ya Bunge, Spika amshauri Mheshimiwa Malima kuwa makini kila anapotoa maelezo Bungeni ili kuhakikisha kuwa maelezo hayo ni sahihi.

Aidha, Waheshimiwa hao pia wamesema kwamba, kuhusu malalamiko ya Mheshimiwa Malima kwamba alikashifiwa na Bwana Mengi na kushushiwa heshima mbele ya Jamii,

wanashauri kwamba Mheshimiwa Malima alipeleke suala hilo kwenye vyombo husika vya kisheria ili liamuliwe kwa sababu si jukumu la Bunge kuamua kuhusu kashfa. Kwa msimamo huu wanaungana na hitimisho la Kamati nzima kuhusu namna ya kushughulikia madai ya kukashifiana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa uchambuzi wa hoja za msingi. Uchambuzi wa Hoja ya Kwanza, ni dhahiri kwamba, kwa mujibu wa tafsiri ya Ibara ya 100(1) ya Katiba, ikisomwa pamoja na kifungu cha 3 cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, 1988, kauli na matamshi yanayotolewa na Wabunge wanapokuwa kwenye vikao au mikutano ya Bunge au Kamati za Bunge, yanalindwa na Ibara hiyo ya Katiba na kifungu hicho cha sheria, hata kama kauli au matamshi hayo yanamwathiri mtu mwingine. *(Makofi)*

*Erskine May* anaeleza kwamba: Namnukuu*: "Subject to the rules of order in debate, a Member may state whatever he thinks fit in debate, however offensive it may be to the feelings, or injurious to the character, of individuals; and he is protected by his privilege from any action for libel as well as from any other question or molestation." Mwisho wa kunukuu.*

Waheshimiwa Wabunge, lakini Tafsiri ya maneno "*Subject to the rules of order in debate"* ni kwamba, kauli na matamshi yanayotolewa na Wabunge wanapokuwa kwenye vikao au mikutano ya Bunge au Kamati za Bunge, yanalindwa na kupewa kinga *(legal immunity),* pale tu ambapo yatakuwa hayakiuki Kanuni na taratibu za majadiliano Bungeni, kwa mfano kutokutenda vitendo au kutozungumza mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. *(Makofi)*

Kwa hiyo, taratibu za kibunge zimeweka ukomo wa uhuru wa kutoa mawazo Bungeni. Ni dhahiri basi kuwa hakuna uhuru usio na mipaka *(absolute freedom)* ndani ya Bunge la Tanzania. Kwa wanaoamini kuwa kuna Mungu, wanaamini kuwa, ni Mungu Muweza wa yote pekee, ndiye mwenye uhuru huo usio na mipaka. Uhuru unaotolewa kwa Bunge na kwa Wabunge na kuhakikishwa na Ibara ya 100(1) ya Katiba, umewekewa mipaka na Ibara ya 100(2) ya Katiba inayotamka kwa maneno yafuatayo:-

"Bila ya kuathiri Katiba hii au masharti ya sheria nyingine" Hiki ndicho kikwazo, huwezi kuwa Na uhuru, narudia tena "bila ya kuathiri Katiba hii au masharti ya sheria nyingine *yoyote inayohusika, Mbunge yoyote hatashtakiwa au kufunguliwa shauri la madai Mahakamani* kutokana na jambo lolote alilolisema au kulifanya ndani ya Bunge au alilolileta Bungeni kwa njia ya maombi, muswada, hoja au vinginevyo."

Tafsiri ya Ibara hii ni kwamba, Mbunge yeyote ambaye matamshi yake Bungeni yatadhihirika kwenda kinyume na masharti na matakwa ya Katiba au masharti ya sheria nyingine yoyote inayohusika, anaweza kuchukuliwa hatua ndani au nje ya Bunge.

Vilevile tafsiri ya maneno: "Kuathiri Katiba hii au masharti ya sheria nyingine yoyote inayohusika," inajumuisha kwenda kinyume na Katiba na pia kwenda kinyume na masharti na matakwa ya Kanuni za Bunge zilizotungwa na Bunge chini ya Ibara ya 89(1) ya Katiba, kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kutekeleza kwa ubora wa shughuli zake.

Waheshimiwa Wabunge, maana ya maneneo ya Ibara hii ndogo ya (2) ya Ibara ya 100 ya katiba ni kwamba, uhuru wa majadiliano ulioelezwa katika ibara ndogo ya (1) utatumika kwa kutambua kuwa kuna ibara nyingine za Katiba zinazopaswa kufuatwa na kuzingatiwa, na

kwamba, uhuru huo haupaswi kutumika kwa kuvunja au kukiuka masharti na matakwa ya Ibara hizo nyingine za Katiba au sheria nyinginezo. *(Makofi)*

Katika kuunga mkono msimamo huu, Bw. *Erskine May* yule mtaalam wetu tena anasema chini ya kichwa cha habari "*Modern Application of Privilege law"*, anasema kwamba:

*"Throughout the long history of parliamentary privilege, the need to balance two potentially conflicting principles – both first enunciated in the seventeenth century – has become clear. On the one hand, the privileges of Parliament are rights 'absolutely necessary for the due execution of its powers'; and on the other, the privilege of Parliament granted in regard of public service 'must not be used for the danger of the Commonwealth."* Mwisho wa kunukuu.

Aidha, "kwenda kinyume na masharti na matakwa ya Kanuni za Bunge," ni pamoja na kufanya au kutenda tendo lolote ambalo limekatazwa na Kanuni hizo, mojawapo likiwa ni kufanya lolote kati ya mambo yasiyoruhusiwa Bungeni, ambayo yameainishwa na Kanuni ya 50 ya Kanuni za Bunge (Toleo la 2004).

Mathalani Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Bunge, inaweka mipaka kwa uhuru uliotolewa kwa Bunge na Wabunge chini ya na Ibara ya 100(1) ya Katiba, kwa maneno yafuatayo: "Ni marufuku kabisa kusema uwongo Bungeni. Kwa sababu hiyo, Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni, atawajibika kuwa na hakika kwamba, maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu."

Hivyo basi, ni dhahiri kwamba Mbunge anayesema uwongo Bungeni, au Mbunge anayesema mambo ya kubuni au kubahatisha tu, hawezi akadai au kustahili kinga ya kutokuchukuliwa hatua.

Ufafanuzi uliotolewa na maelezo ya hapo juu unajibu, bila mashaka yoyote, hoja ya kwanza ya msingi kwa kudhihirisha kwamba, uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu unaotolewa na Ibara ya 100(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Kifungu cha 3 cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, 1988 una mipaka.

Kama nilivyopata kutamka humu Bungeni siku za nyuma, dhana ya kinga isiyo na mipaka kwa Wabunge, ina athari ya kuwaweka Wabunge kuwa ni juu ya wananchi. Dhana hiyo, si tu kwamba inapingana na misingi ya demokrasi ambapo Wabunge wanawajibika kwa wananchi, bali pia inaathiri ibara ya 8(1) a ya Katiba ya nchi yetu inayotamka bayana kwamba: "Wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote…." *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Majibu ya Hoja ya Pili. Kwa mujibu wa ufafanuzi nilioutoa hapo juu, ni kwamba, ili matamshi yoyote yanayotolewa na Mbunge Bungeni yapewe kinga chini ya ibara ya 100(1) ya Katiba na Kifungu cha 3 cha sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, 1988, ni lazima yakidhi matakwa na kutimiza masharti yafuatayo:-

(a) Yasiathiri Katiba au masharti ya sheria nyingine yoyote inayohusika kulingana na fasili ya ibara ya 100(2) ya Katiba;

(b) Yasiwe ni juu ya mambo yasiyoruhusiwa kusemwa Bungeni kama vile kutumia jina la Mheshimiwa Rais kwa dhihaki [Kanuni 50(5)] au kuzungumzia mwenendo wa Rais, Spika na kadhalika [50(6)];

(c) Yasivunje au kukiuka masharti na matakwa ya Kanuni za Bunge, mojawapo likiwa ni kwenda kinyume na masharti ya Kanuni ya 50 ya Kanuni za Bunge (Toleo la 2004).

Ili kujibu, kwa usahihi hoja ya pili ya msingi hatuna budi tupime na kujiridhisha iwapo matamshi au kauli aliyoitoa Mheshimiwa Malima Bungeni, kama ilivyonukuliwa hapo juu, inakidhi na kutimiza masharti hayo, na hivyo kuwa na kinga chini ya Ibara ya 100(1) ya Katiba na Kifungu cha 3 cha sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, 1988.

Kauli ya Mheshimiwa Malima kwamba:- Nanukuu tena. "Nimewahi kushuhudia mimi Rais wa Jamhuri ya Muungano ana habari nzito kwenye taarifa ya habari ya saa mbili anapewa dakika moja na nusu, Waziri Mkuu anataka kuzungumzia njaa anapewa dakika moja na nusu, watoto wa *'Primary'* wanakuja kutoka Zanzibar kutembelea Kiwanda cha *Coca-Cola* wanapewa dakika kumi. Mmiliki wa *TV* anakwenda kuongea na watoto wa Madrasa Msasani kwa ajili ya kugombana na Sheikh mmoja anapewa dakika kumi." Mwisho wa kunukuu.

Hii inadhihirisha wazi na kushawishi kuwa Mheshimiwa Malima alikuwa anatoa taarifa ya jambo alilolishuhudia yeye mwenyewe. Katika kauli yake, Mheshimiwa Malima alikuwa anazungumzia kitu cha kitaalam, yaani muda wa kurusha matangazo hewani *(Air time)*, ambapo muda huo hupimwa kwa sekunde.

Kamati ilifanya uchunguzi kwa kuangalia kanda za televisheni za matukio yote yaliyokuwa yametajwa Bungeni na Mheshimiwa Malima. Imedhihirika kwamba, kanda za pande zote mbili yaani za Bwana Mengi na alizoziwasilisha Mhe Malima. Imebainika kuwa, si kweli kwamba, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipewa dakika moja na nusu, watoto wa *Primary* kutoka Zanzibar waliotembelea Kiwanda cha *Coca-Cola* walipewa dakika kumi na Mmiliki wa *ITV* alipokuwa anaongea na watoto wa Madrasa Msasani alipewa dakika kumi.

Katika ushahidi wa kanda zilizowasilishwa na Bwana Mengi, tukio la Bwana Mengi kutembelea Madrasa ya Msasani lilirushwa hewani kwa dakika 4.21, tukio la ziara ya watoto wa *Laurent International* ya Zanzibar kutembelea *ITV* Mikocheni lilirushwa hewani kwa dakika 3.17, tukio la Waziri Mkuu akizungumzia njaa lilirushwa hewani kwa dakika 5.04 na tukio la ziara ya Rais Msumbiji lilirushwa hewani kwa dakika 3.31.

Katika ushahidi wa kanda zilizowasilishwa na Mheshimiwa Malima, tukio la ziara ya Rais Msumbiji lilirushwa hewani kwa dakika 3.20, tukio la Waziri Mkuu akizungumzia suala la njaa lilirushwa hewani kwa dakia 4.28, na matukio ya Bwana Mengi kutembelea Madrasa ya Msasani na lile la watoto wa *'Primary'* ya Zanzibar kutembelea *ITV* na *Coca-Cola* yalirushwa hewani kwa dakika 5.50 kwa ujumla wake.

Waheshimiwa Wabunge, matokeo hayo ya uchunguzi wa Kamati hiyo ya Bunge yanaonesha wazi kuwa, matamshi ya Mheshimiwa Malima hayakutimiza masharti niliyoyataja kwenye aya ya 5.4.2.1 hapo juu, yaani kwamba, yamevunja na kukiuka masharti na matakwa ya Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Bunge (Toleo la 2004) ambayo, pamoja na mambo mengine, inapiga marufuku Mbunge yeyote kusema Uwongo Bungeni. *(Makofi)*

Kwa uelewa mzuri, Kanuni hiyo inatamka kwamba: "Ni marufuku kabisa kusema uwongo Bungeni. Kwa sababu hiyo, Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni, atawajibika kuwa na hakika kwamba, maelezo anayoyatoa ni sahihi, na siyo mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu."

Ukweli huo unatusaidia kujibu hoja ya pili kwamba, kutokana na kukiuka masharti ya Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Bunge, matamshi ya Mheshimiwa Malima aliyoyatoa Bungeni hayana kinga inayotolewa na Ibara ya 100(1) ya Katiba na Kifungu cha 3 cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, 1988. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, uzito wa shutuma zilizotolewa na Mheshimiwa Malima. Kabla ya kutoa majibu ya hoja ya msingi ya tatu, ni muhimu tukapima na kufafanua uzito wa shutuma alizozitoa Mheshimiwa Malima Bungeni dhidi ya chombo cha habari cha *ITV* pamoja na mmiliki wake Bwana Mengi. Ni muhimu kwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuelewa uzito wa shutuma husika na athari zinazoweza kutokea kutokana na shutuma kama hizo, ili kuweza kubaini iwapo '*reaction'* ya Bwana Mengi kuhusiana na shutuma husika ilikuwa halali kwa vyovyote vile.

Tujiulize tu kuwa, je tuhuma husika kwamba Bwana Mengi amejikweza na kuwafunika Rais na Waziri Mkuu ina uzito gani, na je, tuhuma kama hizo zinaweza kuwa na athari gani kwa mtu anayelengwa?

Ni wazi kabisa kwamba, shutuma hii, kwa taathira yake *(by its implication)* inakishtaki na kukigombanisha chombo cha habari cha *ITV* na mmiliki wake Bwana Mengi, kwa upande mmoja dhidi ya Viongozi wakuu wa nchi, kwa upande mwingine. *(Makofi)*

Tuhuma hizo za mtu kujiweka juu ya Rais na Waziri Mkuu, zina uzito mkubwa sana, na kwa hali yoyote ile. Aidha, zingeweza kuwa na athari kubwa sana kwa chombo hicho cha habari kilichoshutumiwa, pamoja na mmiliki wake, hususan katika nchi kama yetu ambayo Rais wetu ni Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amri Jeshi Mkuu *(Executive President)* na Waziri Mkuu ana madaraka juu ya udhibiti, usimamiaji, utekelezaji wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hiyo, kuweka katika hali ya kuonekana kwamba Bwana Mengi anajikweza katika vyombo vyake vya habari na kujijengea umaarufu unaompita Rais na Waziri Mkuu ni jambo la hatari sana kwa mfanyabiashara na kwa raia yeyote ndio maana unaweza kuelewa kwamba Bwana Mengi alilalamikia kauli hiyo kuliko zile za Waheshimiwa wengine ambao walitamka kwamba anajipendelea na anawasakama wengine kama vile *Quality Group*. *(Makofi)*

Ni muhimu vilevile Wabunge na wananchi kwa jumla, tukaelewa kwamba, vyombo vya habari hapa nchini vimeanzishwa kwa mujibu wa sheria na kwa malengo maaalum. *(Makofi)*

Kwa jinsi hiyo, kuna vyombo vya habari vinavyoanzishwa kwa ajili ya kutangaza na kueneza masuala ya dini za madhehebu mbalimbali, na vingine kwa ajili ya kutangaza biashara na kadhalika.

Kwa mfano, *Radio Tumaini* imeanzishwa kwa ajili ya kutangaza masuala ya dini kwa madhehebu ya Kikatoliki, *WAPO Radio* kwa ajili ya kutangaza masuala ya dini kwa madhehebu ya Kipentekoste, *Radio Uhuru* kwa ajili ya kutangaza masuala ya Chama cha Mapinduzi na kadhalika. Ni jambo la kawaida kabisa, na sio kosa kwa chombo cha habari kama *Radio Tumaini*, kutumia muda wake mwingi wa matangazo kutangaza masuala ya dhehebu la Katoliki kwa sababu, hayo ndiyo masuala na malengo ya msingi ya kuanzishwa kwake; na kwa kiwango fulani viongozi wa dhehebu hilo watasikika zaidi wakitangazwa kuliko watu wengine wowote. *(Makofi)*

Aidha, si kosa pia kwa chombo cha habari kutangaza masuala yanayohusu mmiliki wake. Katika hali hiyo, haitegemewi mtu yeyote kushangaa au kuishutumu Radio au *TV* iliyoanzishwa na *BAKWATA* kwa lengo la kutangaza masuala ya dini ya Kiislamu, kwa kutumia muda wake kiasi fulani kutangaza masuala ya *BAKWATA* na viongozi wake. Hali kadhalika, kwa wamiliki binafsi wa vyombo vya habari, wataonekana wakitoa ujumbe kuhusu mambo ya msingi wanayoyashughulikia katika jamii kwa mfano mambo ya watoto yatima au walemavu na kadhalika. *(Makofi)*

Cha muhimu kuelewa hapa ni kwamba, mmiliki yeyote wa chombo cha habari, anapokitumia kutimiza malengo ya kuanzishwa kwake, hana budi kuzingatia mipaka iliyowekwa na sheria ya *TCRA*.

Ni dhahiri pia kwamba kutokana na Bwana Mengi kuwa kiongozi katika vyombo mbalimbali hapa nchini, kama vile, Mwenyekiti wa *Media Owners Confederation;* Mwenyekiti wa *Coca-Cola Kwanza;* Mwenyekiti wa *SCULT*; Mwenyekiti wa Makampuni ya *IPP*; Mlezi wa Chama cha Walemavu Tanzania, ni wazi kabisa kuwa, Bwana Mengi ni *'Public figure'* na mfanyabiashara maarufu ambaye ataonekana mara nyingi zaidi kuliko mtu mwingine wa kawaida ambaye hana wingi wa shughuli za umma hata kama Bwana Mengi asingemiliki vyombo vya habari angeonekana kwa kiasi kikubwa kuliko mtu wa kawaida. *(Makofi)*

Sasa baada ya maelezo hayo, napenda kutoa majibu ya hoja ya tatu za msingi kama ifuatavyo:-

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuzungumzia kuhusu uzito wa malalamiko ya Mheshimiwa Malima. Ni muhimu vile vile, kupima na kuona uzito wa malalamiko ya Mheshimiwa Malima dhidi ya Bwana Mengi ili kuweza kujibu hoja za msingi zinazofuata kikamilifu.

Malalamiko ya Mheshimiwa Malima dhidi ya Bwana Reginald Mengi ni kwamba, kwa maneneo kuwa "*shutuma zilizotolewa na Mheshimiwa Malima Bungeni tarehe 2 Agosti, 2006 zilikuwa ni uongo uliotungwa na yeye mwenyewe (Mheshimiwa Malima) kwa maslahi yake binafsi,"* alivyosema Bwana Mengi kwenye taarifa yake kwa vyombo vya habari, yalimkashifu yeye kama Mbunge na kumshushia heshima yake katika jamii.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa nimekwishatoa ufafanuzi wa maana ya uhuru wa majadiliano kwa mujibu wa Ibara ya 100(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, 1977 na Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, 1988, pamoja na mipaka iliyowekwa katika matumizi ya uhuru huo, katika kupima uzito wa malalamiko ya Mhe. Malima dhidi ya Bwana Mengi tutafakari na kujihoji sisi wenyewe kuhusu masuala muhimu yafuatayo:-

(a) Iwapo uhuru wa majadiliano Bungeni unaruhusu wabunge kusema maneno ambayo si ya kweli, au kuwashutumu watu wengine ambao si wabunge, na iwapo uhuru huo unaruhsu au hauruhusu watu wasio wabunge kuzijibu shutuma pale wanaposhutumiwa na Wabunge ndani ya Bunge.

(b) Iwapo kutokana na uhuru huo mwananchi wa kawaida anayo au hana haki ya kurekebisha usemi au ukweli wa jambo lililozungumzwa ndani ya Bunge.

Kabla sijatoa ufafanuzi kuhusu masuala haya mawili muhimu napenda kuuliza swali moja ambalo naamini litatufanya sisi sote na wananchi wote kwa ujumla tuelewe vizuri masuala haya ambayo yanatugusa. Swali lenyewe ni:-

Waheshimiwa Wabunge, iwapo itatokea, kwa mfano, Mheshimiwa Mbunge mmoja akatamka Bungeni kuwa, Imamu au Padri au Mchungaji wake wa Kijijini, katika Kijiji fulani katika Jimbo lake ni jambazi Kijijini kwake: Je, yule aliyeguswa na matamshi hayo ambayo ni ya uwongo kweli hana haki ya kusahihisha matamshi au usemi huo?

Nimetamka hapo awali kwamba, hakuna uhuru usio na mipaka, na kwamba, uhuru wa majadiliano Bungeni halikadhalika nao pia una mipaka iliyowekwa na Katiba na Sheria nyingine za nchi.

Waheshimiwa, hebu tutafakari hali ya kuwa na kinga isiyo na mipaka. Je, tungeweza kwenda kwenye Kampeni za uchaguzi, tukawaambia wapiga kura kwamba, tuchagueni, ila tukishafika Bungeni tuna kinga dhidi yenu isiyo na mipaka kwa matamshi yetu yoyote yale, yawe ya uwongo, uchochezi, au ya kudhalilisha, na mtu yeyote hataruhusiwa kutuhoji? tutaonana baada ya miaka mitano. Lakini je, taarifa iliyochapishwa na *ITV* dhidi ya Mheshimiwa Malima hata kama inatokana na kuchokozwa haikuvuka mipaka na kumuathiri Mheshimiwa Mbunge huyo?

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu majibu ya hoja ya tatu na ya nne, mtu binafsi asiye Mbunge anayo haki ya kuhoji au kujibu shutuma zozote zinazotolewa na Mbunge dhidi yake ndani ya Bunge. Haki hii (*right of reply*) inatokana na matakwa ya haki ya asili (*natural justice*) yanayohitaji kwamba, mtu asituhumiwe na kuhukumiwa bila ya kusikilizwa (a *person should not be condemned unheard*).

Katika Bunge letu hili haki hiyo imetolewa kwa utaratibu uliowekwa na Kanuni ya 28 na 40 ya Kanuni za Bunge, kwa kuwasilisha maombi au maelezo binafsi, kupitia kwa Mbunge yeyote. Majibu ya *ITV* na Bwana Mengi dhidi ya Mheshimiwa Malima yalikuwa na lugha ya kuudhi na kwa hiyo hayakumtendea haki Mheshimiwa Malima. *(Makofi)*

Katika mabunge ya nchi zingine za Jumuiya ya Madola, upo utaratibu wa mtu asiye Mbunge kujibu shutuma zinazotolewa na Mbunge dhidi yake ndani ya Bunge. Mfano mzuri ni Bunge la '*New South Wales'* nchini Australia, ambalo limeweka utaratibu unaoitwa *"Right of Reply Scheme*", ambao kwa mapitio mepesi na uelewa, nimeunukuu hapa chini:

*Citizen's Right of Reply, Resolution in the New South Wales Legislative Council*. Inasema hivi: *" Any person who has been referred to in the House by name, or in such a way as to be readily identified, may make a submission in writing to the President(speaker),"* kule Spika anaitwa President, nashukuru hapa sio hivyo, maana yake lah! Ingeleta migongano *"on any one or more of the following grounds, claiming:*

*(a) that they have been adversely affected:*

*(i) in reputation;*

*(ii) in respect of dealings or associations with others;*

*(b)* *that they have been injured in occupation, trade, office or financial credit; or*

*(c)* *that their privacy has been unreasonably invaded, and requesting that they should be able to include an appropriate response in the parliamentary record* yaani raia anaruhusiwa ku-*apply* kwa Spika matamshi yaletwe Bungeni anayaandika anayaleta, ndio Australia hawa.

*(1)* *Where a person makes a submission to the President (speaker), the President (speaker) must, as soon as practicable",* ni lazima hakuna hiari hapa, raia kalalamika leta Bungeni *"as practibale consider the submission and decide whether:*

*(a)* *To refer the submission to the Standing Committee on Parliamentary Privileges and Ethics (referred to as "the Committee") for inquiry and report; or*

*(b)* *It is inappropriate to be considered by the Committee on the grounds that the subject matter of the submission is trivial, frivolous, vexatious or offensive in character.*

*(2)* *The President (speaker) must inform the person in writing of the decision."*
Waheshimiwa Wabunge, pengine itakuwa vema tukaiga mfano huu wa Australia ili kuweka hali hii wazi zaidi katika taratibu zetu.

Kabla sijahitimisha suala hili kwa kutoa maamuzi yangu naomba nizungumzie suala la Mheshimiwa Ndesamburo, kuhusu tuhuma kwa Wabunge kupewa rushwa.

Waheshimiwa Wabunge, kabla ya Kamati kuwasilisha taarifa yake kwangu, Mjumbe wa Kamati Mheshimiwa Ndesamburo alielezea mkasa ambao ulihusisha suala la rushwa. Kwa bahati mbaya, katika suala hilo, Mheshimiwa Ndesamburo katika nyakati mbalimbali, amelitolea kauli ambazo zinakinzana. Kwanza aliieleza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuwa Bwana Mengi alimlalamikia kwa njia ya simu kwamba:-

"Anaamini Bwana Mengi Kamati hiyo haingemtendea haki Bwana Mengi, kwa kuwa kulikuwa na vitendo vilivyoashiria maamuzi ya Kamati kuingiliwa na Serikali, na pia alikuwa na taarifa na ushahidi kuwa Bwana Mengi aliitwa na Waziri Mkuu ambaye alimshauri ajitoe katika 'kesi' hiyo, kwa kuwa Wabunge wamehongwa na Bwana Manji, hivyo hatashinda."

Alipokuja kuniona Ofisini Dar es Salaam, Mheshimiwa Ndesamburo akiwa pamoja na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Nh'unga na Makamu Mheshimiwa. Masilingi, tarehe 10 Januari, 2007 akiambatana pamoja na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Nh'unga na Makamu Mheshimiwa Mheshimiwa Masilinga, mimi nikiwa na Naibu Spika, alitueleza nia yake ya kujiuzulu ujumbe wa Kamati ikiwa Kamati haitawahoji Bwana Mengi na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nilimjibu kuwa, ikiwa tuhuma ni dhidi ya Wabunge wengi au dhidi ya Kamati, isingewezekana Wabunge waitwe na kuwahoji, kama mashahidi wakati wao wenyewe Wabunge ndiyo watuhumiwa. Isitoshe kwa nini aamini mazungumzo ya simu kwa jambo zito kama hili?

Hata hivyo siku hiyo hiyo akaniletea barua yake ya kujiuzulu ujumbe wa Kamati ambamo alidai umetokana na: nanukuu:

*"(a)* *kuwepo kwa madai kwamba Wabunge wamepewa rushwa na Manji na Kamati kutofuatilia suala hilo kujua ukweli wa mambo kabla ya kesi ya msigni kuamuliwa;*

*"(b)* kuwepo kwa mazingira ya Mhimili wa Utawala *(Executive)* kuingilia" sasa hii ni maneno yake kwa hiyo lazima niyanukuu hivyo hivyo *"kuingilia mhimili wa Bunge (Legislature)* ambayo ni kinyume na utawala bora na mgawanyo wa madaraka." Mwisho wa kunukuu.

Lakini taarifa za vyombo vya habari tarehe 11 Januari, 2007 vikinukuu aliyoyasema kwenye mkutano wa waandishi wa habari jana yake zilidai kuwa, Mheshimiwa Ndesamburo alieleza kuwa, wenye kutiliwa mashaka ya kula rushwa ni wanakamati wenzie na siyo Wabunge "wengi" kama alivyonieleza Ofisini au "Wabunge" bila kubainisha kama alivyoniandikia. Kwa kuwa kuna Wanakamati ambao ni Wabunge, Wabunge wengi ambao ni takribani sisi sote na Wabunge tu ambao idadi yake haijulikani.; pia alielekea kusema kuwa alikutana na Bwana Mengi, kinyume alivyoniambia ofisini kwamba ilikuwa ni kwa simu, sasa anasema walikuwa wanakutana na siyo kwa simu kama alivyotamka awali.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ili kuondoa utata, nilimwandikia barua aweke bayana zaidi tuhuma zake, ili niweze kuamua hatua za kuchukua. Ikiwa ni wajumbe wa Kamati ndiyo watuhumiwa wa rushwa nilikuwa na uwezo wa kuagiza kwa taratibu wa Kibunge zitumike katika kuchunguza. Lakini ikiwa ni "Wabunge wengi" pamoja na Spika pengine au "Wabunge" kwa idadi isiyo wazi isingewezekana kutumia taratibu wa Bunge. Hii ni kwa sababu ya msingi kwamba, Bunge/Wabunge wasingeweza, wao wenyewe wakiwa ni watuhumiwa, kujichunguza na ama kujisafisha ama kujihukumu.

Barua ya Mheshimiwa Ndesamburo aliyonijibu tarehe 24 Januari, 2007 bado imeendeleza utata kwa kudai kwamba, wanaohisiwa kula rushwa ni Wabunge kwa ujumla. Habainishi kwamba, ni Wajumbe wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, au Wabunge wengineo nje ya Kamati hiyo.

Wakati wote huu suala hili la tuhuma za Mheshimiwa Ndesamburo kuhusu rushwa limeendelea kuchukuliwa kisiasa na chama chake cha *CHADEMA* ambao wamenukuliwa na vyombo vya habari wakisema kwamba wamepeleka barua kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Aidha, wamekuwa wakizungumzia uvumi huu kwenye mikutano mbalimbali ya wananchi.

Taarifa za karibuni zinaelezea kwamba, Mheshimiwa Ndesamburo sasa anachapisha kitabu kuelezea jinsi suala la Bwana Mengi na Mheshimiwa Malima lilivyoshughulikiwa vibaya na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

Katika hali inayozidi kukanganya katika barua yake kwangu ya tarehe 24/1/2007, Mheshimiwa Ndesamburo akinijibu kuainisha tuhuma amedai kwamba, nanukuu: "Na hata katika barua yangu sijamtaja Yusufu Maji aliyenitukana magazetini. Mimi nilimtaja *Manji* tu ambaye anamjua Bwana Mengi na huenda siyo Yusufu Manji." Mwisho wa kunukuu. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tuhuma za "*Wabunge kupewa rushwa"* ni nzito na ukizingatia kuwa zimetolewa na Mbunge ambaye ni mtu mzima na mzoefu, haziwezi kupuuzwa hata kidogo. Kutokana na sababu hiyo, na kwa kuzingatia ukweli kuwa, kupokea au kutoa rushwa ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria za nchi; *(Makofi)*

Kwa kuwa, kwa kosa la jinai Wabunge hatuna kinga yoyote, na kwa kuwa kuna chombo mahsusi cha kisheria cha kushughulikia uchunguzi wa rushwa, niliamua kumwagiza Katibu wa

Bunge awasiliane kwa maandishi, na Mkurugenzi wa Tume ya Kudhibiti Rushwa *(TAKURU)* ili uchunguzi ufanywe kubaini ukweli, na hatimaye kuachia sheria ichukue mkondo wake. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge aliandika barua tarehe 26 Januari, 2007 kukabidhi suala hili kwa *TAKURU*. Aidha, kwa nakala ya barua hiyo, ambayo ilinakiriwa kwa Mheshimiwa Ndesamburo amehimizwa kutoa ushirikiano kwa *TAKURU*, ili ukweli kamili ufahamike.

Aidha, nimemwagiza Katibu wa Bunge anipatie ushauri kamili wa uhalali au vinginevyo, wa Mheshimiwa Ndesamburo akiwa Mjumbe wa Kamati ya Bunge, kufanya mawasiliano yasiyo rasmi na mmoja wa wanaochunguzwa wakati uchunguzi unaendelea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ingewezekana kuiagiza Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kufuatilia jambo hili, lakini nimeona si hekima kufanya hivyo kwa sasa.

Waheshimiwa Wabunge, nachelea kuchukua hatua zozote ambazo zitaonekana kumwekea vipingamizi Mheshimiwa Ndesamburo, hasa kwa sababau tuhuma za rushwa anazielekeza kwa Waheshimiwa Wabunge wenzake ni nzito.

Waheshimiwa Wabunge, sasa Maamuzi ya Spika. Kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi na ushauri wa Kamati ya Kinga, Maadili na Madaraka ya Bunge, na pia kwa kuzingatia ushauri wa Wajumbe wawili wa Kamati hiyo waliotoa mawazo tofauti na pia uchambuzi na ufafanuzi nilioutoa hapo juu na vile vile na kwa kuzingatia mwenendo wa suala lenyewe na yote yaliyojitokeza wakati Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ikifanya uchunguzi wake;

Na kwa kuzingatia uzito wa tuhuma za Mheshimiwa Malima dhidi ya Bwana Mengi kuwa zimemuathiri Bwana Mengi zenye athari ya kumgonganisha na viongozi wakuu wa nchi;

Na kwa kuwa, kitendo cha Bwana Mengi cha kukosea utaratibu kwa kutumia lugha ya kuudhi kukanusha matamshi ya Mheshimiwa Malima kupitia vyombo vya habari na kuwa pia imemuathiri Mheshimiwa Malima;

Na kwa kuwa, itakuwa ni kwa manufaa ya wahusika, ambao ni watu maarufu kwamba, suala hili limalizwe na kufikia mwisho wake;

Na kwa kuwa, linapotokea suala lolote Bungeni au kwenye Kamati ya Bunge, suala hilo linapaswa liamuliwe kwa mujibu wa utaratibu za Kibunge *(Parliamentary usage and practice);* Katibu naomba ugawe uamuzi sasa. *(Makofi)*

Na kwa kuzingatia kuwa, malalamiko husika hayakuwa ni 'kesi' kati ya Mheshimiwa Malima na Bwana Mengi, bali ni malalamiko ya wote wawili, kila mmoja akimlalamikia mwenzake, kama yaliyowasilishwa kwangu kwa ufumbuzi;

Na kwa kuwa, busara zangu zinanituma kwamba, njia nzuri na iliyo bora ya kuyashughulikia na kuyamaliza malalamiko ya watu hawa wawili, ni kwa usuluhishi (*reconciliation*) kati yao; kwa hiyo basi, Mimi Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuleta suluhu hiyo, naelekeza kwamba:

(i) Katibu wa Bunge awasiliane na wahusika yaani Bwana Mengi na Mheshimiwa Malima, ili tukutane ofisini kwangu Dar es Salaam, kwa siku nitakayopanga na iliyo muafaka

kwao tuweze kuongea pamoja kwa madhumuni ya kukubaliana nami, utaratibu muafaka, utakaojenga suluhu endelevu baina yao na kuepuka hatari ya suala hili kushamirisha makundi yaliyoanza kuchomoza ambayo yameanza kuibua masuala ya udini, rangi na tofauti za vipato katika jamii. *(Makofi)*

Uamuzi huu nimeutoa Dodoma leo tarehe 08 Februari, 2007, ahsante. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijatoka ndani ya ukumbi naomba niwashukuru sana wote walionisaidia Katibu wa Bunge, Watafiti ndugu Oscar Mtenda, lakini pia vijana wa *Hansard* ambao leo walikesha, saa nane usiku ndiyo niliwakabidhi haya na asubuhi hii waliweza kuchapisha vijitabu ambavyo kwa subira kidogo mtagawiwa hayo maamuzi na ninaomba sasa niachie kiti kazi hii niliyoifanya nadhani si ndogo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, namuomba sasa Naibu Spika, aweze kuja ili aongoze kikao ahsante sana. *(Makofi)*

**Taarifa ya Kamatiya Hesabu za Serikali *(PAC)* na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. GEORGE B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja kama ifuatavyo:- *Medical Store Department (MSD),* imepewa dhamana ya kusambaza madawa, kwenye Mahospitali yetu katika Halmashauri za Wilaya. Tatizo kubwa tulilolikuta katika Halmashauri tulizozitembelea ni kuhusu kutopatikana kwa madawa katika Bohari ya Madawa ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko hayo yanadai kuwa, kuna tatizo la uorodheshaji wa mahitaji ya madawa yanayohitajika katika Halmashauri zetu. Kwa kuwa fedha za madawa za Halmashauri zimewekwa *MSD* hivyo, Halmashauri zetu zinabanwa kuchukua madawa kutoka *MSD* tu na wala siyo sehemu nyingine. Mara nyingi Halmashauri zetu zimekuwa zikipewa pungufu na wakati mwingine nusu ya mahitaji yao. Halmashauri zetu hushindwa kutoa huduma iliyokusudiwa kwa sababu ya ukosefu wa madawa toka *MSD.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza Halmashauri zetu, zipewe uhuru wa kununua madawa kwenye maduka mengine ya madawa, ambayo hayapatikani *MSD.* Haileti maana yoyote, kwa *MSD* kuendelea kukumbatia fedha za Halmashauri wakati hawawezi kuwapatia madawa. Kuna tatizo la watumishi wa Hospitali ya Nyakahanga, Wilayani Karagwe, kutolipwa mishahara yao mapema na kutolipwa nyongeza ya mishahara hadi sasa. Wafanyakazi wa Hospitali ya Nyakahanga, iliyoko Wilayani Karagwe, hawajapewa nyongeza ya mishahara ya mwaka 2006 hadi sasa. Tatizo hilo linakera sana na linavunja moyo watendaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kilio cha watumishi wa Hospitali ya Nyakahanga, kuhusu ucheleweshaji wa mishahara yao. Tarehe za kupokea mishahara hutofautiana kila mwezi. Napendekeza watumishi wa Hospitali ya Nyakahanga, Wilayani Karagwe, walipwe nyongeza ya mishahara yao na malimbikizo. Pia mishahara yao iwe inapelekwa kwa wakati unaotakiwa, mshahara uende ndani ya mwezi husika na tarehe iwe ni moja, isiwe tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawo wa fedha za ujenzi wa madarasa Sh. 3.1 milioni na mgawo wa Sh. 3.6 milioni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mwalimu, hazitoshi hasa kwa kuzingatia kuwa, kiwango hicho kilitolewa tangu mwaka 2002. Ninashauri fedha hizo ziongezwe. Pia fedha hizi hutolewa sawa bila ya kujali umbali wa maeneo.

Mfano, Shule ya Msingi Wazo, ambayo iko kilometa kati ya 2 – 5 toka kiwanda cha saruji kilipo, inapewa fedha sawa na Shule ya Msingi Chamuchuzi, iliyoko Wilayani Karagwe, zaidi ya kilometa 3,000 kutoka Kiwanda cha Saruji cha Wazo, Dar es Salaam. Tafiti zimeonesha kuwa, mfuko wa saruji Wilayani Karagwe ni Sh. 18,000 – 20,000. Wakati mfuko huo huo wa saruji kwa Dar es Salaam ni Sh. 11,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba, kwa hali yoyote ile, ujenzi wa chumba cha darasa chenye vipimo sawa na viwango sawa kwa Wilaya ya Karagwe na Wilaya ya Kinondoni, lazima watu wa Karagwe watajenga kwa taabu sana na wakati mwingine kushindwa kumaliza ujenzi huo. Ninapendekeza mgazo wa fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa na nyumba za walimu, ulenge umbali kutoka vifaa vya ujenzi vinakozalishwa. Kwa wale wa mbali, wapewe kiasi kikubwa ili kufidia gharama za usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wetu katika Halmashauri zetu, wana ukosefu wa magari na mafuta kwa ajili ya kusimamia miradi. Kwa mfano, wahandisi wetu, wanahitaji usafiri na mafuta ili kuweza kusimamia ujenzi wa sekondari za kata katika wilaya nzima.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mambo haya yananikumbusha siku hukumu ya kesi ya uchaguzi wangu ilipotolewa. Lakini hakuna marefu yasiyokuwa na ncha. Tunashukuru. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge, jana tulikubaliana ya kwamba tungekuwa na Wazungumzaji wanne katika wale walioomba. Lakini sasa muda umekwisha. Nami ningeomba sasa tuwaite Mawaziri waanze kutoa maelezo juu ya hoja mbalimbali halafu baadaye Watoa hoja watapewa robo saa kila mmoja na Mawaziri wote watapewa saa moja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja na kujibu baadhi ya maswali ya Kamati ya *PAC* pamoja na Kamati ya *LAAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, jana nilifikiria kwamba tungeweza kusema kwamba tumesikia na kwamba tutayafanyia kazi na kwamba kipindi kijacho tutaleta kwa maandishi.

Lakini baada ya majadiliano ya Waheshimiwa Wabunge, tumeona kwamba pamoja na kufanya hivyo basi ni vizuri nijibu au nichangie baadhi ya hoja ambazo zilikwishaletwa mbele yetu. Kwa sababu ya muda, kwa kweli nitachukua hoja chache na kwa sababu Waheshimiwa Mawaziri wenzangu pia watafanya hivyo, basi watachangia hoja nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo ningependa kuchangia kwanza ni suala hili ambalo Waheshimiwa Wabunge, wameelezwa kusikitishwa kwamba kwa Halmashauri zile ambazo hati zao ni chafu, basi fedha zinakuwa hazipelekwi na kwa maana hiyo, tatizo kubwa ni

lile ambalo linawapata wananchi. Niseme kwamba sehemu kubwa ya bajeti yetu ya maendeleo inatoka kwa Wahisani mpaka hivi. Mara nyingine Wahisani wana masharti yao mbalimbali. Lakini Serikali nayo pia imetafakari na imeliona kwamba kunakuwa na matatizo ya maendeleo katika Halmashauri hizo.

Tumeamua kwamba tutalifanyia kazi pamoja na kuzungumza na Wahisani ambao wanahusika. Lakini niseme kwamba Serikali ndiyo maana inazungumzia kwamba upande wa fedha ambazo tunapata misaada, tungependa sana fedha hizi Wahisani wapeleke moja kwa moja kwenye Bajeti ya Serikali *(General Budget Support)*. Inapopeleka moja kwa moja kwenye *General Budget Support* ni Serikali ambayo inaamua sasa kuona matatizo katika sehemu mbalimbali inaamua shughuli fulani iende mahali fulani na kadhalika.

Kwa upande wa *project* ni kwamba, mara nyingi Wahisani wanasema *project* ziende maeneo fulani na ndiyo maana kunakuwa na matatizo pale, unaona kwamba miradi mingi inakwenda sehemu moja ya nchi na siyo sehemu nyingine, pamoja na suala zima la *basket*.

Kwa hiyo, ni tatizo ambalo tunaloliona, mpaka hivi sasa hasa pale ambapo fedha kama Waheshimiwa Wabunge, walivyoeleza kwa maana nyingine fedha zinafika mwisho kabisa kwa sababu tunategemea fedha za Wahisani. Kukitokea matatizo nchini kwao kwa mfano mwaka 2006 kuna nchi moja ambapo kulikuwa na uchaguzi fedha zikachelewa nakadhalika, lakini nasema kitu muhimu nafikiri ni kuongeza mapato ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia na hili nalo limezungumzwa ni kuhusu kodi kutoka Makampuni ya Madini pamoja na ripoti ya *Alex Stewart*. Kwanza niseme kwamba *issue* hii ya *Alex Stewart* haikutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, kwa maana hiyo, haijawa *audit query* kutoka *Control and Audit General*. Sasa hatuelewi jinsi suala hili limetumbukia *PAC* kwa sababu *PAC* mara nyingi inazungumza masuala ambayo yanatoka kwa *CAG*. Sasa *CAG* haikupelekwa kwamba ni kweli kwamba *Alex Stewart* ana Mkataba wa Ukaguzi na kuna *issues* mbalimbali ambazo zinakuwa *raised* pia na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa katika hili labda niseme kwamba, kuna haja ya kujiuliza wakati huu ni nini makubaliano yetu kama Serikali na Makampuni ya Madini, tumekubaliana nini kwa upande wa kodi na kadhalika, nini makubaliano yetu ya makampuni haya ya madini? Kwa sababu kutokana na makubaliano kama makampuni haya hayakwenda kinyume na makubaliano yetu ambayo yaliyokuwa *raised* na *Alex Stewart* yanakuwa maeneo ya kufanyia kazi ambapo kama tulivyoeleza kwamba Serikali imeunda Kamati ya kufanyia kazi maeneo haya mbalimbali, masuala ya kodi, masuala ya sheria na kadhalika.

Tukisema tu tutekeleze kwa wakati huu yale ambayo ambayo yameandikwa na *Alex Stewart* na ambayo kwa kweli bila kuangalia makubaliano yetu sisi Serikali na haya makampuni tutaingia matatizo ya kisheria, kwa kweli. Lakini pia kusema kuwa Serikali imepoteza shilingi trilioni 1.3, trilioni 1.3 ni hela nyingi sana. Trilioni 1.3 ni kama asilimia 25 ya bajeti yetu nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nasema kwamba sio sahihi kwa sasa kusema kwamba Serikali imepoteza Shilingi trilioni 1.3 kwa sababu hili ripoti au *audit* ya *Alex Stewart* na kama nilivyoeleza lazima tuangalie makubaliano yetu kati yetu Serikali na makampuni ya madini haijazungumzwa kwa utaratibu wa *audit* ambapo katika utaratibu wa *auditing* kuwa na *auditor* na *audit*.

Kwa hiyo, kama *report* ya *audit* imefanyika na kunakuwa na matatizo, ndiyo utaratibu. Hata utaratibu wetu wa kawaida huu tunasema kwamba fedha zimepotea kwa mfano, lakini baada ya mazungumzo na yule muhusika, anasema aaa! Hii ni risiti ambayo ilikuwa haikutolewa, sasa nasema kwamba hili halikufanyika.

Kwa maana hiyo, ripoti ya *audit* ya Alex Stuart itabidi kutoa taarifa kwa wale ambao wameyapata katika Makampuni haya na ambayo yanakwenda kinyume na makubaliano yetu kama Serikali katika masuala mbalimbali ya kodi na kadhalika, kukaa kwa mfano na *BOT*, kukaa na Serikali, kukaa na *TRA*, kukaa na Makampuni na kuzungumza haya. Kikao kama hicho hakijafanyika na kwa maana hiyo kwa upande wa *auditing* wanasema kulikuwa hakuna *exit meeting.* Kwa hiyo, kwa sasa hivi hatuwezi kusema kwamba Serikali imepoteza *trillion* 1.4 kwa sababu ya makubaliano.

Nasema kuna mambo mengine ambayo yameletwa kama mawazo ambayo yataongezea na Kamati inayofanya kazi ile, kwa sababu tunajua kwamba kuna baadhi ya Makampuni ambayo tayari yameshaanza kulipa, kwa mfano *Cooperate Tax*. Mfano mmojawapo ni Bulyanhulu imelipa mwaka 2006 *Cooperate Tax* ya Sh.1,120,000,000/=. *North Mara Gold Mine* nayo pia imeshalipa bilioni tisa. *Tanzanite One* pia nayo imeshawahi kulipa Shilingi bilioni 1.2 na kadhalika pamoja na *Geita Gold Mine* ambayo ililipa mwaka 2006 Shilingi bilioni 1. Kwa hiyo, kuna makubaliano haya ya kikodi ambapo Makampuni haya yanasema kwamba yanaanza kulipa baada ya kuwa hawapati hasara.

Sasa Alex Stuwart anasema kwamba wamedanganya. Kwa hiyo, tunasema kwamba hiyo ni *preliminary,* ni *report* ambayo wameeleza. Lakini kwa sababu kulikuwa hakuna *exit meeting,* hakuna mkutano huo. Hatuwezi kusema kwa hivi sasa kwamba Serikali imepoteza Shilingi trilioni 1.4.

Nimesema hilo nililizungumze, natumaini limeeleweka, lakini nasema kwamba mawazo mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia, yatasaidia sana katika kuhakikisha kwamba masuala haya yanaangaliwa pamoja na kushirikiana na wale wawekezaji.

Nchi hii inahitaji wawekezaji na tunaposema kwamba tunahitaji, hatusemi kwamba aah, basi tutafunga macho, kama kutatokea matatizo, hapana. Lakini tunahitaji wawekezaji na tuna sheria na taratibu ambazo tumezipitisha za kodi ambazo Bunge lako Tukufu limepitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kwamba Serikali inatumia fedha nje ya bajeti iliyopitishwa na Bunge. *Figure* ambayo imetolewa ni Shilingi bilioni 31. Sasa niseme kwanza nataka kuweka wazi kabisa na hasa kwa Waandishi wa Habari kwamba hili lilizungumzwa kwa mwaka 2003/2004 na *PAC* inazungumzia, 2003/2004 iko nyuma kidogo. Kwa hiyo, hizi Hesabu za 2003/2004 ninasema kwamba, kwanza kabisa inawezekana kabisa kwamba Serikali inaweza ikapata matatizo ya ukame, mafuriko, hivi sasa miundombinu imeharibika, wakaja wahisani, wakasema kwamba sisi tunataka kuchangia, fedha hizi zinakuwa ni zaidi hazijapitishwa Bungeni.

Mimi kama Waziri wa Fedha nitakuwa kichekesho nikisema hapana hatutaki fedha zenu. Chukueni fedha zenu. Sasa zikitumika pale kwanza Sheria inampa mamlaka ya Waziri wa Fedha kufanya hivyo. Lakini baada ya kufanya hivi, Waziri wa Fedha analeta Bungeni *Bill Suppliment*, sasa Shilingi bilioni 31 ambazo zilitumika mwaka 2003/2004 tayari Waziri wa Fedha ameleta *Bill Suppliment* Na. 2 iko pale Mheshimiwa Cheyo anayo mkononi ambayo itajadiliwa katika Bunge lijalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sio sahihi kwamba Serikali hii inatumia fedha bila kufuata taratibu na Sheria zilizowekwa na Bunge hili. Nasema hilo nalo pia niliweke sawa. *(Makofi)*

Lingine lililozungumziwa ni kuhusu suala zima la Wahasibu kupelekwa katika Halmashauri. Serikali imefanya utaratibu kwamba kila Halmashauri iwe na Mhasibu ambaye ni *trained* na ambaye amepelekwa na Serikali. Lakini niseme Waheshimiwa Wabunge mtusaidie, hata hivi sasa kuna nafasi 600 ambazo zimetangazwa kwa ajili ya Wahasibu kwenda kwenye Halmashauri. Lakini naomba mtusaidie. Vijana hawa wanapata *frustrations* wakifika kule na hatutaki kutaja Wilaya gani, hawapewi kazi. Wale waliokuwepo ndiyo wanazunguka huku na kule lakini wao wanakuwa hawapewi kazi zozote. Naomba mtusaidie, Wahasibu wamepelekwa kwenye Halmashauri na hivi sasa tumetangaza nafasi 600.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda wenyewe ni mfupi na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu pia watachangia, napenda kuchukua nafasi hii tena kukushukuru. Napenda pia kushukuru kwa dhati kabisa Kamati zote mbili kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. Nafikiri utaratibu mzuri huu kwamba tunayazungumza haya hapa Bungeni. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali. Katika Wizara yangu, napenda kutambua mchango uliotolewa na Mheshimiwa John M. Cheyo, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti na Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu. *(Makofi)*

Waheshimiwa wote waliochangia nataka kuwapongeza sana kwa sababu moja kuu. Kwa sababu mawazo yao yote ambayo wameyatoa kwa njia moja ama nyingine yanalenga katika kuhakikisha kwamba Taifa letu linanufaika na madini yanayotokana na hapa nchini. Mawazo namna gani tutafanya yanaweza kuwa tofauti lakini lengo ni lile lile na ndilo ninaloshukuru.

Mheshimiwa Rais alipoingia madarakani alilitambua hilo na alisema kwamba ataanza kulifanyia kazi na kweli ameanza kulifanyia kazi. Kwa hili lina pembe mbili. Pembe ya kwanza ni ile ya Makampuni ambayo tayari tuna mikataba nayo ambayo kisheria huwezi ukavunja hiyo mikataba bila kuzungumza nao. Lakini la pili, ni yale Makampuni ambayo migodi itakuwa inaanzishwa kwa upya. Yote yameangaliwa kwa ujumla wake. Kwanza nijielekeze kwa michango iliyotoka kwa Wabunge wenyewe.

Kwanza kuna hili la kitaalam kwa nini Sheria ya Madini inaruhusu *depreciation* baada ya mwaka mmoja. Hii *depreciation allowance* ya mwaka mmoja iko chini ya Sheria ya Kodi *Financial Laws and Miscellaneous Amendment, 1997* na imewekwa ndani ya Mikataba ya Madini lakini lengo kubwa la hili ilikuwa ni kuwavutia wawekezaji ili waweze kuokoa hela yao ambayo wanawekeza kwa mara moja. Inategemea na uzalishaji wake huenda hata ile *capital* aliyoiweka hawezi akaimaliza kwa mwaka mmoja, inatokea kwamba kuna masalia yanayobaki. Masalio yaliyobaki yalikuwa yanawekwa chini ya Mikataba iliyokuwa na madini ambayo ilikuwa inaitwa mabaki ya asilimia 15 ambayo ilikuwa yanaongezewa tena kama *capital allowance*.

Tunamshukuru Mheshimiwa Rais, katika mazungumzo anayoyaongoza Makampuni ambayo yalikuwa na hii asilimia 15 ya mabaki ya mitambo *capital allowance.* Kuna Makampuni mawili tayari yamekwishakubali kuiondoa na Makampuni mengine tunayoendelea kuzungumza nayo na yenyewe yanaendelea kuiondoa. Tuna uhakika kwamba hapo baadaye na hii Sheria ambayo inaruhusiwa sasa hivi haitakuwa na hayo mabaki. Kwa hili, tunapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwamba nguvu zake alizoziweka sasa hivi zinaanza kutoa matunda. *(Makofi)*

Kuna hoja iliyotokea juu ya maelewano kati ya wananchi na migodi mbalimbali, kuna matatizo mbalimbali hususan kati ya migodi mikubwa na wachimbaji wadogo wadogo ama wachimbaji wadogo wadogo na wananchi wanaoishi katika maeneo ya machimbo hayo madogo madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutangazia Bunge lako Tukufu kwamba sisi toka tumeingia Wizarani, tumekwishaanza ziara za kutembelea migodi yote na kutaka kuoanisha matatizo yaliyopo. Mheshimiwa aliyekuwa Naibu Waziri wangu ambaye ni Mheshimiwa Membe, alikuwa katika ziara hizo za kutembelea hiyo migodi na alikuwa Shinyanga alipoteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje. Sasa hivi Naibu wangu aliyeingia madarakani siyo zamani sana, lakini alipoingia tu wiki iliyofuata na mwenyewe akaenda Mara kuanza kutembelea migodi. *(Makofi)*

Ni nia yangu sasa hivi nilipoingia kwenye Wizara hii nilikuwa nimebanwa sana na nishati. Lakini sasa hivi kwa sababu pamekuwepo ahuweni kidogo, nawahakikishieni Waheshimiwa Wabunge wote kwamba baada ya Bunge hili nina nia ya kutembelea hususan maeneo ya Geita, nimesikia kuna matatizo na maeneo ya Mara kuna matatizo makubwa. Lakini lengo la sasa hivi tunazungumza na wenye migodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tumetoka *South Africa* nilikuwa nimeandamana na Mheshimiwa Rais, amekutana na wenye migodi wote ambao wapo hapa Tanzania. Lengo ni kujaribu kuwaunganisha wawekezaji hao na kwenye maeneo wanayokaa ili wakae kiurafiki. Wawekezaji wanakuja na mitaji na wanakuja na teknolojia, lakini wananchi ambao wanaishi kwa kuzunguika ile migodi ndiyo wanayoilinda hiyo migodi.

Kwa hiyo, wote wawili wanahitajiana, wanategemeana. Kwa kutambua hilo, tumeanza kuzungumza nao. Nitakwenda nizungumze na wananchi na wenyewe wenye migodi nitazungumza nao vile vile ili kuhakikisha kwamba huu uhasama ambao ulikuwa unataka kujitokeza haupo tena na hauna sababu ya kuwepo. Njia moja ya kuuondoa huu uhasama ni wananchi waliozunguka kwa namna moja ama nyingine, hoja imetolewa humu wanafaidikaje na wenyewe kuwepo pale? *(Makofi)*

Moja, ni mapato ambayo yameoanishwa, tumeoanisha katika Mikataba. Lakini la pili ni kuweza kuona wanapata mahitaji yao kutoka kwenye maeneo waliyoyazunguka. Hiyo itafanya yale maeneo waliyoyazunguka na wenyewe kifedha wataweza kuboreka.

Lakini yale mahitaji yanayohitajika na ile migodi kama yanatoka mbali na maeneo hayo mwananchi wa kawaida anaweza asione moja kwa moja hiyo pesa inayokwenda kwenye *Council* ikajenga Shule ama barabara, lakini anachoweza kuona moja kwa moja ni kama amelima mboga zake, nyanya zake: Je, zinanunuliwa kwenye mgodi? Hilo ndiyo tunalishughulikia sasa hivi. Hiyo ni kwa ngazi ya Vijiji vinavyoizunguka migodi. Lakini kwa ngazi ya Kitaifa vile vile ni

kuhakikisha kwamba zile huduma ambazo zinapatikana hapa nchini, basi ile migodi izipate hapa hapa kusudi na Watanzania waanze kunufaika na hiyo migodi iliyopo hapa.

Kuna hoja ya miundombinu iliyojitokeza. Tunatambua kwamba, ili uweze kuwashawishi wawekezaji wawekeze katika nchi yako, hawawezi kuja ukawaambia wajenge barabara, waweke umeme, wafanye hili, mwishoni itachukua muda mrefu ama kulipa kodi ama wataona ile miradi haina faida hawatakuja kuwekeza. Hiyo tunaiwekea mkakati maalum. Kwa mfano, kama hata tunapoanza kuweka ile mipango ya *transmission* mgao wa umeme, tunaanza kuangalia ile migodi iko wapi na mikakati yetu ya hapo baadaye itakuwaje. Kwa mfano, kuna migodi ya kule Geita Bulyamkulu, kuna Kabanga, hamna miundombinu ya umeme.

Kwa hiyo, tunapoangalia, nimewahi kusema kwamba tutakapokuwa tunafanya uchambuzi wa kuweka ile *transmission* ya kwenda Kigoma, njia rahisi itakuwa ni kupitia Geita, Bulyanhulu, Kabanga iteremke Kigoma. Huo umeme utakuwa ni wa faida zaidi kuliko ule wa kupitisha kwenye pori. Kwa hiyo, haya yote tunayazingatia na ujenzi wa barabara vile vile unazingatiwa vile vile ili zifuate rasilimali ziko wapi.

Kuna hoja ya kwamba kumbukumbu za Kampuni ya Madini ziwekwe hapa nchini na sio nje ya nchi. Tatizo sio kumbukumbu umeziweka wapi, kwa sababu siku hizi kwa teknolojia iliyopo, sio rahisi kusema kwamba kumbukumbu zikae hapa ama hapa. Wengine wanaendesha Benki, lakini *saver* inaweza kuwa Ulaya ama kwingine. Lakini la muhimu ni kwamba Wakaguzi wetu wanapohitaji nyaraka za aina fulani zipatikane, hilo ndilo msisitizo wetu. Tunajua kwamba hili chimbuko lake linakuwa kwa ripoti ya Mkaguzi ambaye alikuwa amesema labda akitaka nyaraka wanasema hazipo, ziko nje. Nami nampongeza, wakati hili zoezi linaanza, hili lilikuwa kama tatizo, lakini nampongeza aliyekuwa Waziri wa Fedha, aliingilia, alipoliingia na wakasikiliza zikaanza kutoka.

Kwa hiyo, sasa hivi hatuna tatizo sana na hela yenyewe, ingawa hatujakuwa na uhakika wa mia kwa mia kwamba linakwenda sawa. Lakini ndiyo kazi yetu ya kufuatilia. Mahali ambapo kuna matatizo tunaambiwa, tunafuatilia.

Suala la ufumbuzi wa matatizo katika migodi, nimekwishalizungumzia. Huduma kwa migodi nimelizungumza, mahusiano ya kampuni na wananchi, nimelizungumza. Kuboresha Sheria ya Madini sasa hivi, tunaidurusu ile Sheria ya Madini, wanaitengeneza haijamalizika ili niweze kuichukua kwenye Baraza la Mawaziri baadaye kuileta hapa Bungeni. Lakini iko mbioni inakuja.

Kuna aliyechangia kusema kwamba Botswana wana asilimia 150 kwenye Kampuni ya Almasi. Nami naweza kusema kwamba lengo ni lile lile. Hizo hisa hawakuzipata bure, walizinunua. Nasi inapowezekana tunanunua. Lakini kwa sasa hivi naweza kusema kwamba, kwenye *Wilson Diamonds* tunazo asilimia 25. Kazi bado ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wanataka ku-*expand* katika mgodi ule, kazi itakuwa kwamba ni njia gani tutatumia ili tusipoteze ile asilimia 25 isipungue, isiwe *diluted.* Namna gani tutachangia ili tubaki na asilimia yetu 25? Lengo ni kubaki nazo. Njia gani tutatumia, tutakaa tuzungumze na Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kutembelea migodi na kuona utunzaji wa mazingira, tunapotembelea migodini hatuangalii hilo tu na utunzaji wa mazingira. Lakini vile vile huku

mbele imejitokeza kwamba namna gani nchi yetu inahakikisha kwamba hawa wenye migodi wamejiandaa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kutunza mazingira, lakini pili, watakapofunga migodi hawatuachii mazingira yaliyoharibika. Najua katika sheria zetu katika Kanuni ya Sheria ya Madini tuliyoitunga inahakikisha kwamba mwenye mgodi kabla haujaanza lazima atoe *plan* ya kufunga ule mgodi, inaitwa *Closure Plan.* Hiyo Sheria ilikuwa hailazimishi kisheria aweke pesa au *bonded,* lakini kwa sababu hiyo ni kanuni ambayo inaniruhusu mimi kama Waziri kuweza kuifanyia marekebisho na kwa sababu tumeona sasa hivi kuna udhaifu wa ufuatiliaji huo, ukiiacha hivi hivi tu kwamba waweke *plan* wanakupa *plan.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hiyo *plan* inatekezaje? Usipoiwekea meno mtu anaweza akafunga mgodi ukakuta hakujiandaa namna ya kurejesha mazingira kama ilivyokuwa. Kwa hiyo, tunategemea katika haya mambo ya kurudusu ile *mining development agreement review* tunazozifanya na yenyewe hiyo kuibadilisha kidogo angalau kulazimisha kuweka *bonded.*

Madini kuchangia kwenye uchumi wa nchi, nimeshaizungumzia na namna gani sasa hivi Mheshimiwa Rais anavyolishughulikia sana na bahati nzuri nilitembelea Canada, nilikuwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu alilizungumzia. Lakini jambo la kufurahisha ni kwamba, wale wenye migodi walilipokea vizuri. Tulipokuwa Canada walilipokea vizuri na tulipokuwa *South Africa* juzi wakati Mheshimiwa Rais anatoa mchango wake walilipokea vizuri na kila mmoja alikuwa analifurahia.

Kwa hiyo, nafikiri hili jambo ambalo tumelianzisha ni zuri na ni kujenga tabia tu ili hawa wenye migodi (Wawekezaji) kwa sasa hivi wasione kwamba tumewakaribisha lakini vile vile tunawapiga vita. Pale ambapo kuna matatizo tukae chini pamoja na wao na kwa kuzingatia sheria zetu ili kurekebishana kama wafanyabiashara wa aina yoyote. Lakini tusitumie nguvu sana kuwakaribisha halafu tukatumia nguvu sana kuwafukuza. Hii haitakuwa na faida na sisi.

Uboreshwaji wa huduma za jamii nimelizungumzia. *Mining Closure* nimeizungumzia sasa hivi. Nafikiri na hoja nyingi sana tutazichukua. Nafikiri tutakuwa na utaratibu tu ambao kama alivyolizungumzia Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba hoja zilizozungumzwa hapa tutaziandika halafu Wabunge wote watapewa nakala, yale majibu sahihi ambayo tumeyaweka.

Lakini siwezi nikamaliza hapa bila kuzungumzia kitu alichozungumzia Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ambacho nimekisia tu kabla sijaondoka hapa, lakini kinaleta vuguvugu tu ile taarifa isiyo rasmi iliyotolewa kwa upande wa Alex Stuwart.

Alex Stuwart ni sisi tuliwakaribisha, wanafanya kazi nzuri. Lakini kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, hili limeletwa iwe ni kama kama chombo cha Serikali cha kuisaidia katika kuhakikisha kwamba Sheria zake zinafuatwa kwa hao wenye madini. Halafu pamoja na kwamba tunapata mchango wetu ambao tunaufaidi katika Serikali na kuhakikisha kwamba maana walikuwa na vigezo vitatu, ama vinne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ilikuwa ni kuhakikisha kwamba palikuwepo na hisia nyingi tu hapo nyuma kwamba dhahabu yetu inayozalishwa hapa nchini inatoroshwa. Kuna udanganyifu mbalimbali katika mitaji wanayoleta. Kuna makampuni hayalipi kodi na mengine mambo ya mazingira kama nilivyoeleza.

Lakini hayo yote sasa hivi ndiyo wameanza ndiyo wameanza kutoa taarifa za awali. Hazijafanyiwa kazi wala hazijafika mahali popote. Kwa hiyo, nilishangaa tu nilipokuwa nimesikia kwamba zimeanza kuja kwa kasi na hili tumelipokea hata tunapokutana na hawa wenye migodi mbalimbali, wanasema kwamba taabu yao ni moja kwamba taarifa zinatolewa ambazo zinafanywa na Alex Stuwart ama na Wakaguzi wengine kabla hata wenyewe hawajazipata, hazijawa za kiofisi, *official,* tayari zimekwishaingia kwenye magazeti, tayari wamekwishazungumzwa vibaya na hiyo kwanza inawaumiza wao huko wanapokaa nchini kwao.

Maana yake wengi wako katika *stock market* na kuonyesha kwamba nchi yetu ukija kama mwekezaji ukija hapa ukikaribishwa kama Tanzania kama uko katika *stock exchange* afadhali usije Tanzania. Ukija Tanzania kabla hawajakupa nafasi ya kujitetea ya kujieleza, tayari wamekwishakuweka kwenye magazeti, tayari wamekwisha kutuhumu!

Mimi najua wanatengeneza hizi *charts* za vitu gani vizuri Tanzania, vitu gani vibaya, ili mtu aweze kuamua kuja. Hili ni mojawapo watu kuingia kwenye magazeti bila uchambuzi haujatolewa, taarifa haijawa rasmi, watu wamekwishakimbilia kwenye magazeti. Inawapa shida sana.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, kama sisi tumepewa dhamana na Watanzania wenzetu kwanza kubwa alilolizungumza, nilikuwa nasikiliza vizuri, wakati Mheshimiwa Spika alipokuwa anazungumzia dhamana yetu kama Wabunge, kubwa sana iko kwa Watanzania na kwa Watanzania sio kama tutafanya vitendo ambavyo vitawanyima Watanzania uwekezekano wa kupata faida na nchi yao, vitakuwa havitusaidii na mojawapo ni kuwakaribisha wawekezaji ambao wanatuletea teknolojia watuwekee na rasilimali ambayo tulikuwa hatuna na teknolojia na kifedha ambazo tulikuwa hatuna. Sisi tuna rasilimali.

Kwa hiyo, tunapokuja hapa pamoja na kwamba tunaangalia wakifanya vibaya tuwa-*critisize,* lakini tuhakikishe kwamba tunachokifanya tunakuwa *responsible* tusije tukafanya mambo ambayo yanaweza kuumiza wawekezaji wenyewe, lakini vile vile yakaumiza hata nchi yetu. Nami nitayasemea kidogo.

Baada ya hayo, Mheshimiwa Naibu Spika, nasema ahsante kwa kunipa nafasi na huu ndio mchango wangu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nitoe mchango kidogo kuhusiana na yaliyojitokeza Bungeni kupitia zile Kamati mbili. Lakini zaidi nitajikita kwenye Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nianze kwa kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati hii pamoja na Wajumbe wake wote kwa kazi nzuri sana ambayo kwa kweli wameifanya. Kwanza kujadili Hesabu za Serikali za Mitaa kwa kipindi cha mwaka 2004/2005 kwa Halmashauri zote 118. Lakini nimefarijika zaidi kuona kazi kubwa waliyoifanya wametembelea Mikoa 11 na wamekagua miradi mbalimbali ya maendeleo 591. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kazi kubwa na nataka nimhakikishie Mwenyekiti na Kamati yake yote kwamba maelekezo yote ambayo mmeyatoa kupitia majadiliano mliyoyafanya kuhusiana na Hesabu za Serikali za Mitaa na zaidi hasa kutokana na yale mliyoyabaini huko Mikoani nitahakikisha kabisa kwamba tunatimiza wajibu wetu kwa kuzitaka Halmashauri hizo

kutekeleza yale yote ambayo mmeagiza kwa manufaa ya Halmashauri hizo, lakini vile vile na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa yao, yako mambo ambayo ni vizuri na mimi nikayasemea kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni hili suala ambalo limekuwa ni la muda mrefu la kuzitaka Halmashauri kutenga asilimi 10 ya mapato yao kwa ajili mfuko wa akinamama pamoja na vijana. Sasa jambo hili limekuwa likizungumzwa na sisi tunajitahidi kulihimiza lakini nataka nikiri kwamba bado hatujafanikiwa kuweza kuitimiza ahadi hiyo vizuri. Sasa sababu zake ni nyingi lakini kubwa ni hasa hasa uchache wa fedha ambazo Halmashauri zetu zinakuwa nazo kutokana na vyanzo ambavyo unaweza ukasema ni vidogo ili kuweza kutimiza majukumu yao vizuri. *(Makofi)*

Lakini la pili kwa sababu mfuko huu kwa kweli tegemeo uwe ni mfuko ambao baada ya kujengwa uwe unajiendesha wenyewe, lakini ulipaji, urejeshwaji wa mikopo hiyo ambayo inatolewa kwa akinamama na vijana nalo limekuwa ni tatizo kubwa sana na mimi binafsi sasa nasubiri kwa hamu sana kuona mfuko huu au juhudi hizi mpya za kuwezesha Watanzania chini ya utaratibu wa ile bilioni moja kwa kila mkoa unavyoweza pengine kutumika vilevile tuanze kutazama uwezekano wa mfuko huu kutumia utaratibu ambao nadhani unaweza ukawa unatufaa zaidi hasa katika suala la kurejesha mikopo na ufuatiliaji na kuhakikisha kazi hiyo inafanyika.

Kwa hiyo, nitaendelea kuhimiza jambo hili kufanyika lakini nafikiri itabidi tuanze kutazama utaratibu huu mpya ambao umewekwa katika utaratibu wa uwezeshaji wananchi Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo Mwenyekiti na Kamati yake walibaini ni suala la Wenyeviti wa Vijiji pamoja na wale vitongoji kutokulipwa posho ya aina yoyote, sasa wote tutakumbuka Waheshimiwa Wabunge kwamba huko nyuma kabla ya kuondoa au kufuta vyanzo mbalimbali vya mapato, tulikuwa tunawaruhusu asilimia 20 ya mapato yanayotokana na kodi itumike kwa ajili ya kurejeshwa katika vijiji husika na ndani ya hiyo asilimia 20 kulikuwa na asilimia ambayo ilikuwa inawagusa Wenyeviti wa Vijiji pamoja na wale wa vitongoji kwa maana ya posho zao kwa ajili ya kuwasaidia kuzidi kuwapa msukumo zaidi katika eneo hili.

Sasa utaratibu huo ulisita kwa muda lakini tayari ofisi imekwishatoa maelekezo kwa Halmashauri zote kila Halmashauri inapaswa sasa kutenga asilimia 20 ya fedha ya ruzuku ambayo Serikali Kuu inarejesha kwa ajili ya vyanzo tulivyovifuta na nataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba utaratibu huu katika baadhi ya Halmashauri zilizopita nimekuta tayari unafanyakazi na kwa wastani ni karibu shilingi 200,000 mpaka 300,000 wengine mpaka 400,000 ambazo zinarejeshwa chini ya utaratibu huo. Kwa hiyo, nataka niamini kwamba jambo hili litakwisha na nahimiza Halmashauri zote kuhakisha jambo hili linatekelezwa bila kuzidi kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala ambalo lilijitokeza kwa upande wa Rufiji kwamba kuna watendaji 39 sio arobaini, wako 39 ambao bado walikuwa hawajaingizwa katika kompyuta na kwa hiyo, mishahara yao ina tatizo kidogo ya namna ya kulipwa, tunakubali tatizo hilo lipo lakini limekwisha kurekebishwa. Sasa ninalotaka kusema tu la ujumla ni kwamba kati ya watendaji wa vijiji 10,341, 9,337 wote sasa wanalipwa kupitia kwenye *payroll,* kwa hiyo, na hivi karibuni tumepata orodha ya majina mengine 180 ambao nao sasa hivi tunawashughulikia kuwaingiza katika *payroll* kupitia Wizara ya Fedha. Hawa 180 ni pamoja na wale 39 kutoka

Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji, kwa hiyo, hilo nalo litakwisha, lakini bado tutakuwa tunasubiri kukamilisha zoezi hilo kwa watendaji 824 na tumekwishatoa maelezo kwa Halmashauri zote ifikapo tarehe 1 Machi, suala hili liwe limekwisha. Kwa hiyo, naamini kabisa baada ya muda huo jambo hili litakuwa tena halina tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhususiana na suala la kuwaendeleza kielimu watendaji wa vijiji, ni kweli tulitoa kauli na bado tunasisitiza kwamba ni vizuri ikaendelea kuwepo, kwa hiyo, mwaka huu mwezi Julai, ndio mwisho wa kipindi cha miaka mitatu tuliyowapa watendaji wawe wamejiendeleza, vinginevyo itabidi kuchukua hatua kama tulivyokuwa tumedhamiria na hili tunalifanya kwa nia nzuri kwa sababu bila kuwa na watendaji katika ngazi ya vijiji wenye uwezo ni dhahiri kabisa usimamizi wa shughuli za maendeleo hauwezi kuwa mzuri sana.

Sasa mara mwisho tulisita na ilikuwa ni kutokana na rai ya Bunge, lakini vile vile upande wa chama waliona ni vizuri tukawapa hiyo fursa, madamu tumewapa wako waliojiendeleza, lakini nadhani wako wengine ambao hawaendelezeki, sasa hatutakuwa na njia nyingine, isipokuwa kutafuta watu wenye uwezo kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati vile vile imezungumza kuhusiana na suala *la value for money* kwamba kazi inayofanyika ilingane na thamani ya fedha ambazo tumepeleka, tutazingatia ushauri huu na tayari tumekwishaanza kuchukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha jambo hili linasimamiwa vizuri na tulichofanya pale ofisini tumeanzisha kitengo mahususi cha ukaguzi ndani ya ofisi ya Waziri Mkuu ambacho kazi itakuwa ni kufanya uchunguzi katika Halmashauri zetu zote, bila kungoja kuambiwa kwamba mahali fulani kuna wizi, na tayari timu hiyo imekwishaanza kufanya hiyo kazi na kwa kweli matokeo yake tumeanza kuyaona ni mazuri kwa sababu tumeanza kufahamu matatizo hata kabla jambo lenyewe halijalipuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile niseme kidogo kuhusiana na suala hili la fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya ununuzi, Kamati imetoa pendekezo zuri kwamba pengine asilimia 30 ingeenda moja kwa moja kwenye Halmashauri, ili kuziwezesha angalau kuwa na uwezo wa kununua dawa fulani ya awali, wakati asilimia nyingine ile 70 inashughulikiwa, tunalipokea kwa mikono miwili jambo hili, tutalifanyia kazi kwa kushirikiana na Wizara zinazohusika upande wa sekta ya afya lakini vile vile Wizara ya Fedha ili tuweze kuona kama linawezekana na mimi naamini mbele ya Serikali hii hakuna jambo ambalo linaweza likatushinda kwa kiasi cha kutisha, kwa hiyo, tutalichukua na tutalifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokea vile vile ushauri wa Kamati kwamba tuchunguze suala la shilingi milioni 168 ambazo zilikuwa ni kwa ajili ya mradi wa maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, tutalifanyia kazi na matokeo yake tutaripoti kwenye Kamati kuhusiana na mambo gani tuliyoyagundua katika suala hili. Kwa hiyo, kwa upande huo naomba niseme kwa maana ya taarifa ile ya Kamati, basi haya ni baadhi ya mambo, inawezekana sikuyagusa yote lakini nimeyagusa hapa na pale. Sasa naomba haraka haraka niseme mambo yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusiana na hii suala la Watumishi wanaovunja sheria, kanuni kwamba badala yake tunawahamisha, nilishawahi kulisema na narudia kulisema katika eneo hili tusaidiane, Wabunge wote kwa sababu sisi ni Madiwani na mimi naamini Madiwani *effective* kweli kweli, kwa sababu sisi uelewa wetu ni mkubwa. Maagizo ya Serikali ni kwamba kama mtu amevunja sheria, amekaidi jambo lolote ambalo linamfikisha sasa mahali ambapo inabidi achukuliwe hatua jambo hilo linafanyika pale pale kwenye Halmashauri yake na wengi mtakuwa mmeshaona jambo hili tunalifanya na tuna mifano mingi tulifanya Dodoma, tumefanya kwenye

Halmashauri ya Sumbawanga Mjini pale, Jiji la Tanga pale napo tumefanya na maeneo mengine mengi ambako tunajaribu kuhakikisha kwamba muovu hapati nafasi tu ya kutoka na kwenda sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubali kwamba wakati mwingine fedha zinachelewa kidogo kupelekwa katika Halmashauri zetu lakini ni jambo ambalo Serikali inalifahamu na tunalifanyia kazi kwa pamoja hasa na wahisani ambao nao wanachangia katika shughuli hii. Kwa hiyo, wote kwa pamoja tutaendelea kuhakikisha kwamba jambo hili linafikishwa mapema zaidi kidogo. Kwa Halmashauri sasa zinazopata hati chafu, halafu baadaye tunawanyima fedha ya maendeleo namshukuru sana Mheshimiwa Mama Zakia Meghji, kwa sababu ameliweka vizuri sana kwamba jambo hili litafanyiwa kazi ili tuone kama tunaweza tukapata *a break through* ya namna ya kulifanya, lakini nataka nisisitize jambo moja, kwa sababu ni muhimu kwetu sisi wote kama Wabunge haitawezekana kufikiria kwamba fedha hizi za Serikali zinaweza zikaenda kwenye Halmashauri ambayo haiwezi kusimamia fedha hiyo vizuri. Tutakuwa tunafanya makosa makubwa sana, kwa hiyo, ni lazima tuunganishe nguvu nyingi zaidi kidogo, usimamizi wa karibu lakini vilevile juhudi hizi ambazo Mheshimiwa Mama Zakia Meghji amezitaja, lakini tujue kwamba ni lazima fedha hizo zisimamiwe vizuri kwa sababu bila hiyo huduma pale za wananchi hazitaleta matokeo tunayotategemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watendaji iko rai hapa inasema tupunguze mzigo kwa upande wa Halmashauri kwa kuwalipa watendaji wa Kata fedha zao kutumia utaratibu wa *payroll.* Mimi kama Msaidizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu katika eneo hili watendaji wa kata hatupaswi kuwa na tatizo hilo hata kidogo, hawa wamekuwa kwenye mishahara ya Serikali na wote kwa kweli wanapaswa kuwa kwenye *payroll* kwa sasa. Tatizo lilikuwa katika watendaji wa vijiji ambao ndio tunahangaika nao sasa, kwa hiyo, kama yuko mtendaji wa kata ambaye anasema hajaingizwa kwenye *payroll* sisi tutakuwa radhi kabisa kulishughulikia jambo hilo mapema kwa sababu lilipaswa kutokuwepo kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Suala la *transparency* nalo limejitokeza na naomba niseme tumekuwa tukijitahidi sana kujaribu kutoa matangazo kwenye magazeti kupitia Wizara ya Fedha kwa fedha zote zinazopelekwa katika Halmashauri zetu, ni jambo ambalo tumekuwa tunalifanya lakini tume-*insist* vilevile kule Wilayani kubandika kwenye mbao za matangazo fedha ambazo zinakuwa zinapelekwa katika maeneo yao. Sasa Halmashauri zinafanya lakini inawezekana ziko baadhi ambazo hazifanyi na tutashukuru sana kwa ushirikiano wenu tukijua Halmashauri hizo ili tuweze kuzidhibiti inavyotakiwa kwa manufaa yetu sisi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubali tutajitahidi sana suala la kuzingatia *standard* katika maeneo yote, iwe kwenye majengo, iwe kwenye matumizi ya fedha, kwa ujumla wake kwa sababu ni wajibu wetu kama Serikali kuhakikisha jambo hilo linafanyika. Tunakubali vile vile kwamba suala la mafunzo ya Madiwani muhimu sana hasa kwa sababu wengi mnavyojua kigezo chao kikubwa ni kujua kusoma na kuandika, sasa heri Bungeni ni zaidi kidogo ya lugha hiyo, lakini kwa Waheshimiwa Madiwani ni kweli kabisa uwezo ni mdogo sana kwa hiyo, tunatakiwa kulifanya. Tayari tumeshachapisha vitini vya kutosha kwa sababu zoezi hilo karibu litaanza hivi karibuni kujaribu tena kuwa-*sensitize* Madiwani ili waweze kusimamia shughuli zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la bodi ya zabuni katika Wilaya nalo limejitokeza kwa nguvu sana kutoka kwa Wabunge wengi na naomba niseme tu kwamba kwa sasa Mwenyekiti wa Bodi hiyo sio Mkurugenzi Mtendaji, tumeondoa Mkurugenzi Mtendaji kwa lengo la kuzidi

kuendeleza usimamizi mzuri katika eneo hilo, kwa hiyo, atateuliwa mtu mwingine yeyote lakini yeye hapaswi kuwa mmoja. Sasa ni kweli katika eneo hili naweza nikasema ni kitendawili tega na sina uhakika tutafanyaje *at the end of the day,* yako mawazo kwamba pengine bodi hiyo iwe huru kwa maana ya kujumuisha hata watu wengine kutoka nje ya maeneo haya ya Serikali za mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nasema *bottom line* ni uadilifu hata kama mtasema tulianza na Madiwani, ikaonekana Madiwani ndio wala rushwa wakubwa, tukafikiri njia bora basi tuondoe kwao ili wao sasa wabakie ni watu wanaowasimamia vizuri wale watendaji na kwa kweli kwa mfano mzuri kama wa Dodoma ule ni dhahiri kabisa jambo hili linawezekana. Meya wa Manispaa ya Dodoma alikataa kusaini mkataba mpaka amepata maelezo ya namna walivyofikia maamuzi kumteua huyo mkandarasi na matokeo yake ninyi wote mnajua, ilikuwa ni kesi nzuri ikabainika dhahiri kabisa kwamba mkandarasi yule hakustahili hata kuteuliwa kuwa mkandarasi, lakini ni kwa sababu Meya aliweka mguu akasema siweki saini mpaka nipate maelezo ya mchakato mzima na hili kwa kweli ndio tunalolitegemea kutoka kwa Wenyeviti wote na Madiwani wote, tunahitaji jambo hilo lizingatiwe sana.

Lakini bado ofisi yetu imekubali kutizama tena suala zima hili la bodi tuone kama kuna namna bora zaidi ya kuimarisha utaratibu huo ili kuweze kuonekana pengine kuna nguvu na uweze kutoa matunda tunayoyategemea punde tukimaliza jambo hili basi tutakuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kulisimamia. *(Makofi)*

Ratiba ya vikao vya *RCC* na Halmashauri nimepokea ushauri nitazidi kuzihimiza Halmashauri na mikoa kuzingatia ratiba ya Bunge na vikao vyake.

Mheshimiwa Mbunge wa Mkinga nimeona hili niliseme mahususi kwa sababu anaomba Wilaya yake sasa iwe ni Halmashauri na ameomba vile vile tupate Mji Mdogo wa Muheza. Sasa kwa upande wa Halmashauri nadhani halina tatizo, Wilaya zote zile mpya ambazo Mheshimiwa Rais alizianzisha tuko katika *process* ya kuzitangaza zote kuwa ni Halmashauri pamoja na hiyo Wilaya ya Mkinga. Kwa hiyo, hili halina tatizo hata kidogo, lakini kwa upande wa Mji Mdogo naomba tu niseme mwaka 2004 tulipotoa lile tangazo la Mamlaka ya Miji Midogo, dhamira yetu ilikuwa ni kuhakikisha Makao Makuu ya kila Wilaya inakuwa ni Mamlaka ya Mji Mdogo, sasa nitajaribu tena kuchunguza na wataalamu wangu kama hili hatukulifanya kwa Muheza basi tutaona namna nzuri zaidi ya kuweza kuhakikisha hilo linafanyika. *(Makofi)*

Naomba niseme kidogo juu ya *basket funding* maana limejitokeza limetupa mawazo kwamba haieleweki, hatujui fedha hizo, ukweli ni kwamba fedha hii ni sehemu ya Bajeti ya Halmashauri. Ni fedha ambazo ziko katika miradi mbalimbali ambayo Halmashauri inakuwa imezipanga lakini tunasema zitatumia *fund* ambayo inatokana na mfuko huo wa *basket fund.* Sasa nadhani ni suala tu la kutafuta namna ya kuweka liwe wazi zaidi ili muweze kuelewa kwamba fedha hizo ni zipi na zinakwenda kufanya nini katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, niseme tu kwamba yako mambo mazuri ameyasema tutayazingatia, ingawa kwa kweli sikupenda sana kauli yake kwamba fedha za maendeleo katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha zinatumika kwenda kununua mafuta kwa ajili ya Mkuu wa Mkoa, kwa ajili ya *DC,* kidogo limenisumbua sana kichwani, nitacheki jambo hili kwa uhakika kabisa ili kama ni kweli nitaiarifu Kamati ya Bunge lako kwamba tumechukua hatua gani katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua sina muda lakini naomba basi nimalizie kwa kusema na Mheshimiwa Jacob Shibiliti, kwamba tulipeleka Tume tayari pale Misungwi na tuko katika hatua za kutoa matokeo hivi karibuni kuhusiana na madhambi mbalimbali ambayo tumeyaona pale. Lakini nataka nimhakikishie vilevile Mheshimiwa Jacob Shibiliti kwamba rai yake imesikika vizuri, tumesitisha ule uhamisho wa Mweka Hazina, kwa hiyo, ataendelea kubaki pale ili aweze kuisaidia Halmashauri ile kwa kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na muda mdogo nimeseme la posho ya Madiwani, maana hili siwezi kulikwepa, naomba tu niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Waraka wa Baraza la Mawaziri uliwasilishwa kwenye kikao, Baraza limeshatoa maamuzi tayari kwenye maeneo mbalimbali yanayohusiana na eneo hili la posho pamoja na mambo mengine yanayohusiana na jambo hili sasa siwezi katika dakika hizi nikalielezea, lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kwamba maamuzi yamekwisha patikana na baadaye baada ya muda si mrefu tukishapata muhtasari wenyewe tutatoa sasa maelezo ya namna tunavyofikiri jambo hili litaweza kusimamiwa vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, mengine yote nitajitahidi kuyaweka kwa maandishi na tutayagawa kwa Waheshimiaw Wabunge wote ili muweze kujua ni maelezo gani tulikuwa tumetarajia kuyatoa. *(Makofi)*

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. DR. BATILDA S. BURIAN):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kanuni ya 21(3) kinaeleza kwamba Bunge hili litaendelea katika sehemu yake ya asubuhi na kumaliza kusimamisha shughuli zake saa saba hadi hapo saa kumi na moja, na kwa kuwa shughuli tulizonazo, tunahitaji dakika kumi na tano za ziada, hivyo basi naomba kutumia Kanuni 124 kutengua Kanuni ya 21(3) kuweza kuongeza dakika ili kumaliza shughuli tulizonazo na kusitisha shughuli zetu kwa leo saa saba na dakika kumi na tano.

**WAZIRI USALAMA WA RAIA:** Mheshimiaw Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge ili kuongeza muda wa Kumalizika Shughuli zilizopangwa iliridhiwa na Bunge)*

**MHE. JOHN M. CHEYO - MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nataka kutoa shukrani sana kwa wale wote waliochangia kwenye hoja inayohusu Kamati ya Hesabu za Serikali, nawashukuru sana na kwa mara ya kwanza nimeona hakuna cha Chama, hakuna cha nini kila mmoja amejishughulisha na fedha ya Serikali, jamani hongereni sana na wananchi wametusikia na na nina hakika wamejua kwamba Wabunge tunajali matumizi ya fedha pamoja na mapato ya fedha za Serikali, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, basi kama ilivyokawaida naomba kuwatambua wale ambao natumaini karibu wamechangia kote kote, labda hii itarahisisha pia kwa Mheshimiwa Mgana Msindai ambaye atakuja baada ya mimi naomba kuwatambua wote ambao wamechangia kwenye

hoja ambayo zilikuwa zinagusa kote kote ambao ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Zakia Meghji Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Nazir Karamagi Waziri wa Nishati na Madini na mwisho Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia kwangu kwa njia ya maandishi ni Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa Ruth Msafiri. Kwa muda tulionao ni vigumu sana kuweza kueleza kwa kila Mbunge alilolisema, lakini nimefarijika sana kwamba haya mambo yako ndani ya *Hansard* na pia Mawaziri wamesema watajibu hoja kwa hoja na kuleta hapa Bungeni. Kwa hiyo, nafikiri nitajibu mambo mawili, matatu, kwa ajili ya ufafanuzi na zaidi nitajikita kwa hoja za Mawaziri. Lakini kwa wale waliochangia, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa mfano alitaka kwamba mikataba ya Alex Stuart iweze ikaletwa Bungeni, mimi nasema kwamba kwanza tunaishukuru sana Wizara ya Fedha na pia Benki Kuu kwamba angalau walituonyesha mikataba hiyo na kwa sababu ya unyeti wake mikataba hiyo tumerudisha, lakini tumempatia Mheshimiwa Spika dokezo linaonyesha vitu ambavyo tumeona kwamba inafaa Serikali iviangalie. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama Kamati tume-*side* kwamba kuna ripoti hizo ambazo zinaenda Serikalini na ziko katika hali ya *confidential* na kama vile alivyosema Mheshimiwa Nazir Karamagi kwamba haya mambo tunafanya biashara, *is not politics* sio siasa, kwa hiyo, hatutaki kuwa *over politicise* hizi *findings* hapa lakini hizo *findings* zitusaidie sisi kuweza kufanya maamuzi na pia kuweza kuisimamia Serikali, kwa hiyo, tumefanya hivyo na yeyote yule ambaye anataka kupata *more details,* kuna hilo dokezo la siri ambalo tumempelekea Mheshimiwa Spika, anaweza akajiridhisha na yeye kwamba baadhi ya mambo ambayo nimesema yako kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella alikuwa anatuambia vipi hamkutani na wale wezi, kwa nini hamtupi majina ya wale wezi, leo hii tulikuwa tunasikiliza Mheshimiwa Spika, alivyokuwa anasisitiza juu ya haki ya Mbunge, lakini pia na haki ya watu binafsi. Kwa hiyo, majina tuliyo nayo, yote hayo yatapelekwa kwa Mheshimiwa Spika, anaona kuwa inafaa ataweza kama inabidi kuweza kuyaweka hadharani hapa Bungeni, lakini ni vizuri ukampa mtu haki ya kujitetea kabla hajaweka hadharani ambalo natumaini ni jambo pia la kiungwana.

Nimeulizwa pia juu ya kwamba majina ya wenye nyumba zile mbili zenye utata yako wapi? Pia tumeweka dokezo kwa Mheshimiwa Spika kama alivyotuagiza, kwa yoyote yule anayetaka kujua ni nani mwenye *plot A* au *B* pia anaweza akamwendea akaweza kuangalia, kwa hiyo, haina matatizo.

Sasa nataka kutoa hisia fulani fulani ambazo wakati nasikiliza Waheshimiwa Mawaziri wamezitaja, kwanza ni jambo la Kanuni kwamba haya mambo yanayohusua Alex Stuart yametoka wapi kwamba Kamati kama vile ime-*jumping,* haimo ndani ya Kanuni. Kwanza nataka kusema kwamba Ibara 94 ya Kanuni zetu Ibara ya 1 ni kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu yanayoainishwa katika taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali kuhusu Serikali Kuu. Kama kuna Waheshimiwa Mawaziri wamesoma taarifa ambayo nimetoa nimeanzia kwa kujikita kwamba katika kifungu hiki cha madini ambayo ni Fungu 58 kwamba Mkaguzi na

Mdhibiti Mkuu kwenye hoja 415.1 amehoji uwezo wa Wizara ya Nishati na Madini kukusanya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kila wakati amekuwa anatuambia mnaomba na kuomboleza Serikali ifanye hivi na jibu inajulikana kwamba hakuna pesa. Kwa hiyo, Kamati kwa makusudi kabisa kwa jambo hili imejielekeza kuona ni sababu gani hatupati mapato ya kutosha ya kuridhika katika yatokanayo na Wizara hii na mojawapo ya mapato haya ni mrahaba, *cooperation tax* kutoka kwenye madini. Kwa hiyo, tukasema sisi tujue na tuliposema tujue tumefanya mambo mbalimbali sio *issue* ya sijui kwa nini hii imekuwa ni kubwa sana na *sensitive* kwa Serikali, hii inatupatia shida sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kitu gani ambacho Serikali ina *worry about* Alex Stuart, sisi tulianza kwanza na Gavana wa Benki Kuu kumuuliza je, tunapata dhahabu ya kutosha na fedha ya kutosha kutoka kwenye dhahabu kufuatana na hii hoja kwamba *potentiality,* uwezo wa Wizara hii kuiletea Serikali mapato ni mkubwa lakini ukiwa unapata shilingi bilioni 25 tu kwa mwaka kama mwaka 2003/2004 kufuatana na hiyo hoja tena walianza kusema watapata shilingi 16 bilioni, baadaye wamepata shilingi bilioni 22 ndio Mkaguzi akashituka kwamba ninyi kumbe mna *potential* kubwa.

Mimi naona Bunge hili linafaa lijielekeze katika kuisaidia Serikali kupata mapato, badala ya kila siku kujielekeza tu kuidai Serikali nipe nipe kutoka wapi. Kwa hiyo, mimi naona na *I think* ni *innovation* ambayo ninyi Waheshimiwa Mawaziri mnapaswa kutusifu kwenye Kamati hii ambayo angalau tumeanza, kitu kipya hiki hakijapata kutokea. Sasa tunajikita kuuliza *where can we get money,* kwenye madini tunaweza kupata fedha. Kwa hiyo, tulimwita Gavana wa Benki Kuu na tulimwita Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha watueleze ni matatizo gani. Si hivyo tu, tulimwita na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na yeye atueleze ni vipi hawapati mapato ya kutosha na baadaye tukasema kwamba kumbe kuna ripoti ya namna hiyo inayotueleza kwamba kuna matatizo moja, mbili, tatu. *Okay,* tukasema kama ni hivyo tuletee hiyo ripoti tuangalie ni matatizo ya namna gani. Kwa hiyo, hii ni kama *a way* ya kupata kuelewa ni nini ambacho kinafanya Wizara hii isipate mapato.

Kwa hili nataka kusema kweli tumepata ushirikiano mkubwa sana. Kwa mfano, hivi sasa nina ripoti ya Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha imekuwa wazi kabisa, *TRA* wamekuwa wazi kabisa, kuna *loses* moja, mbili, tatu na iko hapa. Hata ninaposema kwamba ni trilioni 1.358 hizi ni takwimu kutoka Wizara ya Fedha ambazo zinathibitisha siyo kwamba Serikali imepata hasara, inathibitisha kwamba Makampuni hayo yamepata hasara kama Mheshimiwa Nazir Karamagi anavyofahamu. Ukiwa *a corporation,* ukipata hasara ndiyo kusema huwezi ukawa *charged corporation tax*. *This is a fact* kila mmoja anafanya biashara na wengi wanajaribu kufanya hasara ziwe kubwa ili wasiweze kulipa *corporation tax. (Makofi)*

Sasa huu ni ukweli na tunasema *this what have been told by Government.* Mimi sijasema kwamba Serikali haijaweza kukusanya, hapana, tumesema *TRA,* nendeni sasa mkazungumze na hayo Makampuni kuhakikisha kwamba hizo *loses* zinapungua *this what I have said.* Mimi naona Kamati yetu imefanya kazi nzuri wala tusiseme kwamba tuwataje hao watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kabla sijamaliza muda wangu kusema kweli nataka kuisifu sana Wizara ya Fedha kwa kuwa wazi na ni vizuri ikashirikisha Bunge, ikawa wazi na Bunge hili likielewa matatizo mengi hayatakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka kuweka *in record* tumesikitishwa sana na Wizara ya Nishati na Madini kuzuia tusipate habari. Tulimwita hata Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini aje na wenye migodi wenyewe watueleze ni kwa nini hatupati faida, lakini hatukupata ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Waziri, tuliwaambia Wizara hata wamlete yule Mkaguzi tunayemlipa mabilioni wala siyo mbele ya Waandishi wa Habari aje atueleze ni matatizo gani ambayo anapata mpaka hivi sasa kwa kuwa analipwa fedha kiasi hicho. Wizara ya Nishati na Madini haikuweza kumleta huyo mtu kuweza kuzungumza nasi. *(Makofi)*

Mimi nasema kwa mambo ya mapato tuwe pamoja na Serikali tusukume mapato, Waheshimiwa Wabunge tusukume mapato kuna ubaya gani? Mtu akikwambia hapo unaibiwa, wewe unamchukia huyo mtu, *I think should run fantastic,* hebu tuone kama kuna hilo jambo ili tuweze kupata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka ku-*clarify* hilo kwamba sisi hatuku *jump in* kwa kuvunja. Kuna hoja 415 zinazohoji *potentiality,* uwezo wa Wizara hiyo kutengeneza fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nataka kutoa angalizo niko *very serious,* tumeandika kwa Mheshimiwa Spika kumwomba Katibu Mkuu ambaye ndiye Afisa Mhasibu sisi tuna *deal* na Maafisa Wahasibu, hatu-*deal* na mtu mwingine aje aieleze Kamati kwa nini amekaidi kuja kwenye vikao ambavyo tumemwita. Wengine wote wamekuja *why did not come* akaielimisha Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa jumla nimefarijika sana na mazungumzo ambayo yametokea katika Bunge hili na pia napenda kurudi kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa wewe Naibu Spika ulivyoendesha Kikao hiki na pia kwa kutoa muda wa kutosha. Sasa karibu siku mbili tunajadili Mapato na siyo tu Matumizi, Mapato na Matumizi ya Serikali na mapungufu yaliyomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba kutoa hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nifanye majumuisho kwa kifupi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa John Cheyo, Mwenyekiti wa *PAC* kwa kuwataja wale waliochangia kwa kuzungumza humu ndani ya Bunge. Sasa mimi sitarudia kuwataja majina yao, ila naomba niwataje waliochangia kwa maandishi na wengi wao wakiwa wamechangia upande wa *LAAC* wa kwanza ni Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Castor Ligallama na wa mwisho ni Mheshimiwa Gosbert Blandes. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kwa niaba ya Kamati ya *LAAC* kwanza mimi niishukuru sana Serikali kwa sababu karibu yale yote tuliyoyapendekeza wameyakubali kwamba ni mambo ya maana na wamekubali kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema jana, sisi na Wizara ya TAMISEMI hatuna ugomvi, huwa tukimaliza kukagua tunamwandikia Waziri na kwa kweli mara nyingi amekuwa anachukua hatua. Kwa hilo Wizara tunaipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado maeneo mawili ambayo yamelalamikiwa sana, la kwanza ni yule Mweka Hazina wa Misungwi aliyeanza kulalamikia hiyo ni Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, kwa sababu huyo alikuwa Mweka Hazina wa Ukerewe na akaharibu sana na Kamati yetu ikaandika barua kwa Waziri kwamba huyo mtu achukuliwe hatua, hafai akahamishwa huyo. Lakini nafikiri Wizara ilipitiwa, lakini na huko Misungwi alikokwenda ameharibu zaidi. Kwa hiyo, sisi bado tunaiomba Wizara ya TAMISEMI imchukulie hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, wa pili alikuwa *Engineer* wa Tandahimba, huyo alifanya madudu, alipewa shilingi milioni 13 za barabara, *tender* ikatangazwa siku hiyo hiyo saa nne asubuhi, *tender* ikapitishwa, *mobilization* ikafanyika, kazi ikafanyika ilipofika saa saa 7.00 mchana na mkandarasi akalipwa. Yule mtu pamoja na kuharibu hivyo alihamishwa tu na sasa bado anaendelea kuwa *Engineer* wa Wilaya fulani hapa Tanzania. Kwa hiyo, hilo tunaiomba Serikali ichukue hatua ili watu wengine waone kwamba kwa kweli Serikali imeamka na inafanya kazi kwa kasi mpya na nguvu mpya. *(Makofi)*

Lingine ni juu ya fedha za MMEM na MMES zinavyotolewa. Hizo fedha zinatolewa kwa darasa moja kwa MMEM ni milioni 3.1 Mtu wa Ilala anapata milioni 3.1, hata ile shule ilipo pale Wazo ambako mfuko mmoja wa saruji ni shilingi 11,000. Mtu wa Karagwe kule Mrongo au mtu wa Sumbawanga kule Nkasi naye anapewa fedha hizo hizo milioni 3.1. Kwa kweli sisi tungeiomba Serikali iliangalie hilo. Madarasa mengi na nyumba za walimu haziishi kujengwa kwa sababu Dar es Salaam sasa hivi bei ya saruji ni shilingi 11,000 na kule tulikotembelea mfuko wa sementi ni shilingi 20,000. Sasa hapo sisi tungeiomba Serikali iangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie kwenye ile Mikoa ambako Kamati ilitembelea madarasa ya shule za sekondari na madarasa ya shule za msingi ambako hayajakamilika tumepeana muda na wenzetu kwamba ifikapo mwezi Aprili, 2007 kabla hawajaja kwenye Kamati watakuwa wameyakamilisha. Kwa hiyo, huko tuna uhakika wataifanya hiyo kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo naomba nilizungumzie ni juu ya Kituo cha Afya cha Misungwi ambacho upasuaji unafanyika kwenye wodi ambayo wanajifungulia akinamama yaani upasuaji huo ni wa akinamama na wanaume na hicho Kituo cha Afya hakihudumii Wilaya ya Misungwi tu, kinahudumia sehemu ya Wilaya ya Kwimba, sehemu kubwa ya Wilaya ya Solwa pamoja na Misungwi yenyewe. Kwa hiyo, kwa kweli tunaiomba sana Serikali iliangalie hilo na ilichukulie kama kitu cha haraka, iwasaidie mara moja wananchi wa maeneo hayo. Lingine tunashukuru kwamba Serikali imeona kwamba kupitia kukagua hesabu, Serikali inadanganywa sana. Kwa hiyo, sasa hivi ni lazima tufanye *value for money.* Halafu lingine *quality* ya madarasa na nyumba za walimu tuseme na kazi zote zinazofanyika huko hazifikii kiwango cha Serikali kinachotakiwa. Serikali ilisema mfuko mmoja wa sementi utoe matofali 30, lakini ukienda zile kuta ukigusa tu mchanga unatoka. Kwa hiyo, na hilo ni lazima kwa kweli twende na ubora hiyo itatusaidia zaidi. Serikali ilisema watumie bati geji 28, lakini katika maeneo mengi tuliyokwenda yametumika mabati ya geji 30. Kwa hiyo, mimi ningeiomba Serikali itoe maelekezo ili hao ma-*engineer* na Wakurugenzi wajue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo na mimi ningependa kulirudia na wamelichangia Waheshimiwa Wabunge wengi sana ni pale Serikali ipomchagua mtu kuwa Mkurugenzi wa Wilaya wakati yeye kabla ya wadhifa huo alikuwa ni Mtendaji anachaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Wilaya anaachwa pale pale kwenye kituo kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona matatizo mengi sana. Wengi wanakuwa wanavurugana na wenzao. Kwa hiyo, sisi tungeshauri kabisa tunakubali kwamba huyo amepata sifa za kuwa Mkurugenzi basi aende katika kituo kingine. Mimi ningependa tujue kwamba sisi Waheshimiwa Wabunge wote ni Madiwani. Mimi ningewaomba sana Kamati ya *LAAC* inavyoendesha vikao vyake pale Dar es Salaam au Dodoma ningewaomba sana Waheshimiwa Wabunge nyie kama sehemu ya Halmashauri zenu mje na wajumbe wa hizo Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme ni Waheshimiwa Wabunge wengi sana hawaelewi yanayotendeka kwenye Halmashauri zao na wale Waheshimiwa Wabunge ambao wameshahudhuria Vikao ya Kamati ya *LAAC* kwa kweli wanafaidika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni hili la vikao vya Halmashauri kule, Waheshimiwa Wabunge wengi walilizungumzia na wakamwomba Waziri atoe agizo vikao viwe vinaitishwa wakati Waheshimiwa Wabunge wako Majimboni. Kwa sababu Halmashauri nyingi zinavizia Waheshimiwa Wabunge wako Bungeni ndiyo vikao vinaitishwa. Kwa hiyo, mimi ningeshauri hayo yatekelezwe na nirudie kusema Kamati yetu haina mgogoro na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tunafanya kazi kwa ushirikiano nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukisoma Kanuni yetu ya 94(1) na(2) ya Hesabu za Serikali na Hesabu za Serikali za Mitaa inasema hivi: "Majukumu ya Kamati ya Hesabu za Serikali yatakuwa kama ifuatavyo:- Kwanza, kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu yaliyoainishwa katika taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali kuhusu Serikali Kuu. Pili, kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishakutolewa na Kamati hiyo ya kuondoa matatizo husika ili yasionekane tena katika taarifa zifuatazo.

Kwa hiyo, napenda kuwahoji kwanza kwa Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali kwamba Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo katika Taarifa hiyo.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge**,** nitawahoji sasa kuhusu Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mitaa *(LAAC)* kwamba Bunge sasa lipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa pamoja na mapendekezo na maoni yaliyomo katika Taarifa hiyo.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali na Taarifa ya Hesabu za Serikali za Mitaa ziliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Mawaziri wakazisome tena taarifa hizi na kuchukua hatua zinazofaa ili kusudi tuweze kupata mafanikio na *value for money* ya Kamati hizi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hilo, nina matangazo machache. Kwanza, kulikuwa na Semina ya Maboresha ya Utumishi wa Umma yatakayohusua Kamati mbili. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Kamati ya Huduma za Jamii. Nimeambiwa kwamba semina itaendelea kama mlivyotangaziwa. Halafu Kamati ya Huduma za Bunge mlipewa barua wajumbe wake mkitoka hapa mwende kwenye Mkutano kule.

Sasa nasitisha Shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 jioni.

*(Saa 07.18 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

## HOJA ZA SERIKALI

## AZIMIO

### AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA MAREKEBISHO YA MKATABA WA KUANZISHWA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI YA MWAKA 2006 *(AMENDMENT TO THE TREATY FOR THE ESTABLISHMENT OF THE EAST AFRICAN COMMUNITY, 2006)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kibaha Vijijini na mimi mwenyewe napenda kutoa rambirambi kwa Mheshimiwa Rais, familia na ndugu wa marehemu Juma Jamaldini Akukweti aliyekuwa Mbunge wa Tunduru na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Masuala ya Bunge aliyefariki baada ya kupata ajali ya ndege mkoani Mbeya. Aidha, napenda kutoa rambirambi kwa ndugu na jamaa wa watumishi wote waliofariki katika ajali hiyo, Mwenyezi Mungu aweke roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Wataalam wa mambo ya diplomasia wanafahamu kwamba uteuzi kama huu, uteuzi wake, ni kigezo muhimu cha mafanikio ya sera yetu ya mambo ya nje na diplomasia yetu katika medani za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Dr. Bernard Membe, Mheshimiwa Dr. Batlida Burian, Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Gaudence Kayombo kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje ukiongozwa na Mheshimiwa Anna Abdallah na Makamu wake Mheshimiwa Mussa Zungu kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano mkubwa waliotupa wakati wote tangu Wizara ilipoanzishwa. Kwa namna ya pekee napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Mussa Zungu, Mbunge wa Ilala na Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na

Kamati nzima ya Mambo ya Nje kwa jinsi walivyoishauri Serikali katika kuboresha Azimio nitakalolisoma leo hii Bungeni. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru sana wadau wote hususan viongozi wa Chama cha Wanasheria Tanganyika *(Tanganyika Law Society)* waliokuja Dodoma na kutoa ushauri uliosaidia ukamilishaji wa Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa Serikali wa kuleta Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Afrika Mashariki umeleta mjadala kwa baadhi ya wadau wetu na ni vyema basi nikatoa maelezo kabla ya kusoma Azimio lenyewe.

Baada ya uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika mwezi Novemba, 2006 baadhi ya wananchi wa Jamhuri ya Kenya hawakuridhika na utaratibu uliotumika kuwachagua Wabunge wa kuiwakilisha Kenya. Wananchi hao walilalamika kuwa kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi kama zilivyoainishwa katika Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(Treaty for the Establishment of East African Community)* pamoja na sheria za Kenya. Kutokana na malalamiko hayo Professa Nyong na wenzake kumi walifungua kesi namba moja ya mwaka 2006 katika Mahakama ya Afrika Mashariki wakidai kuwa uchaguzi uliofanyika katika nchi ya Kenya ni batili na wakidai kwamba uchaguzi mpya ufanywe na pia wa kuitaka Mahakama itoe amri ya kuzuia kuapishwa kwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki ambao walipaswa kuapishwa tarehe 29 Novemba, 2006 mjini Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Afrika Mashariki ilikubaliana na hoja ya kuweka zuio au lalamikaji kwa kusimamisha kuapishwa kwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Uamuzi huo ambao kimsingi umesimamisha shughuli za Bunge la Afrika Mashariki ulipokelewa kwa tafsiri na mawazo na msimamo na hisia tofauti. *(Makofi)*

Aidha, palijitokeza mgogoro mkubwa na ari ya dharura juu ya heshima na ufanisi wa Jumuiya na vyombo vyake uliohitaji kushughulikiwa. Kwa mfano, kwa kawaida katika kesi za Uchaguzi katika nchi wanachama na hususan hapa kwetu Mbunge akiwa na kesi ya uchaguzi, Mbunge huyo huendelea na kazi yake ya Ubunge mpaka kesi inapomalizika na hukumu kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tafakuri ya masuala yote haya yaliashiria umuhimu wa kufanya mabadiliko madogo katika Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutoa fursa kwa upande wowote ambao hautaridhika na jambo litakalojitokeza kutumia Mahakama yenye ngazi mbili yaani sehemu ya awali na kama mtu hataridhika basi awe na fursa ya kukata rufaa katika sehemu ya pili ya Mahakama ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa fursa hiyo haipo kwa kuwa katika Muundo wa Mahakama ya Afrika Mashariki hakuna kitengo au Mahakama ya Rufaa. Mahakama iliyopo ndiyo ya mwanzo na ya mwisho. Ni kama vile Waheshimiwa Wabunge hapa nchini kwetu tungekuwa na mfumo wa Mahakama ambao ni Mahakama ya Mwanzo tu na ukishinda, ukishindwa ndiyo basi hapo hapo huna fursa ya kukata rufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati njema kabisa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeweka utaratibu wa kuufanyia marekebisho ili uendane na wakati na ili uweze

kukabiliana na changamoto zinazojitokeza. Katika Ibara ya 150 pameelezwa utaratibu wa kufuata katika kufanya marekebisho kama ifuatavyo:-

(1) Imeelezwa kwamba Mkataba wenyewe unaweza kufanyiwa marekebisho kwa makubaliano ya nchi zote wanachama wa Jumuiya.

(2) Nchi yoyote mwanachama inaweza kutoa mapendekezo ya kufanya marekebisho ya Mkataba.

(3) Mapendekezo yoyote ya kufanya marekebisho ya Mkataba yanapaswa kupelekwa kwa maandishi kwa Katibu Mkuu ambaye ndani ya kipindi cha siku 30 toka siku ya kupokea mapendekezo hayo atawasilisha kwa nchi wanachama.

(4) Nchi yoyote mwanachama inayotaka kutoa maoni juu ya mapendekezo hayo inapaswa kufanya hivyo ndani ya siku au ndani ya kipindi cha siku tisini kuanzia siku ambayo Katibu Mkuu ametuma mapendekezo.

(5) Baada ya muda ulioainishwa katika Ibara ya awali niliyoisoma au niliyoitafsiri kuisoma basi Katibu Mkuu atawasilisha mapendekezo hayo pamoja na maoni yoyote yaliyotolewa na nchi wanachama kwenye kikao cha Wakuu wa Nchi Wanachama yaani *Summit* kupitia kwenye Baraza la Mawaziri.

(6) Marekebisho yoyote ya Mkataba huu yatakubaliwa yaani yatakuwa *adopted* na Wakuu wa nchi na yataanza kutumika mara tu nchi zote wanachama zitakaporidhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoa tafsiri isiyokuwa rasmi ya vipengele vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza katika Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwa kweli kusema yale ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzingatia hali ya dharura iliyojitokeza na athari zake kwa amani, usalama, utawala bora na ufanisi kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi wanachama na kwa mujibu wa Ibara ya 11(3) ya Mkataba katika Mkutano wake wa kilele wa nane yaani *Summit,* Wakuu wa Nchi za Afrika Mashariki mjini Arusha tarehe 30 Novemba, Wakuu hao:-

(1) Waliridhia ushauri wa Baraza la Mawaziri wa Afrika Mashariki kwa kuunda upya yaani *reconstitute* Mahakama ya Afrika Mashariki ili iwe na sehemu mbili, Mahakama ya Awali na Mahakama ya Rufaa.

(2) Waliagiza pamoja na kuundwa upya kwa Mahakama hiyo utaratibu pia wa kuwaondoa Waheshimiwa Majaji wa Mahakama hiyo utazamwe upya ili kuweka sababu zote za msingi.

(3) Waliagiza pawepo na Mkutano wa Kilele Maalum yaani *Extra Ordinary Summit* haraka iwezekanavyo ili kupitia mapendekezo, kufanya uamuzi juu ya marekebisho ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maagizo ya Wakuu wa Nchi za Afrika Mashariki ambao ndio chombo cha juu kabisa cha Jumuiya ya Afrika Mashariki tarehe 8

Desemba, 2006 Mkutano Maalum wa Baraza la Mawaziri *(Extra Ordinary Meeting of the Council Ministers)* lilipitia na kuafiki mapendekezo ya Wanasheria Wakuu wa Afrika Mashariki ya kufanya marekebisho katika Mkataba wa Jumuiya. Pili, tarehe 14 Desemba, 2006 paliitishwa Mkutano Maalum wa Wakuu wa Nchi za Afrika Mashariki yaani *Extra Ordinary Summit* na Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki mjini Nairobi kwani Wakuu walikubali marekebisho yaliyofanywa yafanywe katika mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema awali baada ya uamuzi huu wa kufanya marekebisho ya Mkataba pamejitokeza hoja mbalimbali nitataja chache:-

(1) Kwamba taratibu za kurekebisha Mkataba kama ilivyo katika Ibara ya 150 zilikiukwa yaani *Monitory procedure of amendment a stipulated in article 150 of the treaty was not followed.*

(2) Kwamba mapendekezo ya marekebisho yanalenga kupunguza Mamlaka, uhuru na hadhi ya Mahakama ya Afrika Mashariki kwa lugha ya Kiingereza yaani *The proposal amendments sake to undermined the authority integrity and independence of the East African Court of Justice.*

(3) Mapendekezo ya marekebisho yana dhamira mbaya ya kutaka kukwepa maamuzi ya Mahakama yaani *proposed amendments are premised and improper motive namely to circumvent to the decision of the court.*

(4) Marekebisho ya Mkataba hayakuzingatia dhana ya utawala bora na utawala wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kuwashukuru wadau wote kama nilivyosema awali kwa michango yao na hususan Chama cha Wanasheria Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba marekebisho yanayowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii kwa nia ya kuomba kuridhiwa yanalenga kuunda upya Mahakama ya Afrika Mashariki iwe na vitengo viwili kikiwemo Kitengo cha ngazi ya kwanza (ya awali) na pia kitengo cha rufaa au Mahakama ya Rufaa. Lengo ni kutoa nafasi, uhuru na haki ya kukata rufaa kwa mtu yoyote au asasi itakayohitaji fursa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inatambulika duniani kwa kuzingatia haki na kutoa fursa kwa wananchi wake kutumia Mahakama kutafuta haki na huu ndio msingi wa utawala bora na msingi wa utawala wa sheria. Sera hii inatokana na sera ya Chama chetu cha Mapinduzi na Ilani yetu ya Uchaguzi. Ndiyo maana basi na ndiyo sera hiyo hiyo inayofanya Serikali yetu kuunga mkono hatua hii ya kufanya marekebisho katika Mkataba wa Afrika Mashariki. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inaheshimu sana utawala bora, inaheshimu sana utawala wa sheria, kinga za Majaji, hadhi na uhuru wa Mahakama. Taratibu za kufanyia marekebisho zilifuatwa hususan kwa tafsiri kwa muda uliowekwa kwenye Mkataba ni wa ukomo. *(Makofi)*

Aidha, kama ambavyo nimeeleza hapo awali kwamba palikuwa na mchakato wa vikao mbalimbali ambavyo vilifuata taratibu ya kupitia mapendekezo na mpaka kufikia maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Mkataba hayana dhamira mbaya na hayaingilii au kuathiri kesi zilizopo Mahakamani. Kama Waheshimiwa Wabunge watakavyoona katika marekebisho ameweka kipindi cha mpito katika Ibara ya 140, hii ina maana kuwa kesi zilizoko Mahakamani kwa sasa zitachukuliwa kama zipo katika Mahakama ya Awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya kikao cha Wakuu wa Nchi wanachama yalilenga kutatua tatizo ambalo mfumo wa Mahakama kama ulivyo hivi sasa haukidhi, ukosefu wa Mahakama ya Rufaa una maana kuwa ikiwa mwanachama au mdau yoyote hakuridhika basi hana mahali pa kukimbilia pa kukata rufaa, hii ni kinyume kabisa na mfumo ambao tunao hapa nchini ni kinyume kabisa na Katiba yetu na sheria zetu mila na desturi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi naomba Waheshimiwa Wabunge tufanye kazi yetu kama viongozi kwa kuridhia azimio nitakalolisoma hivi punde. Wenzetu wa Kenya na Uganda wamefanya kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nilisome Azimio la Bunge Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2006 *(The Amendment to the Treaty for the Establishment of the East African Community 2006).*

KWA KUWA Tanzania ni nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

NA KWA KUWA Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ulisainiwa na Wakuu wa Nchi za Tanzania, Kenya na Uganda mwaka 1999 na kisha Mkataba huo kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vile vile Bunge lilitunga Sheria ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mwaka 2000;

NA KWA KUWA Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ulifanyiwa marekebisho na kusainiwa na Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki akiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 14 Desemba, 2006 mjini Nairobi;

NA KWA KUWA lengo na marekebisho katika Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kuunda upya Mahakama ya Afrika Mashariki kwa kuanzisha vitengo viwili yaani Kitengo cha Mahakama ya Awali na Kitengo cha Mahakama ya Rufani ambapo Mahakama ya Awali itakuwa ni Mahakama ya kuhakikisha Sheria inafuatwa katika kutoa tafsiri, maamuzi na utekelezaji wa Mkataba wa Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Mahakama ya Rufani itashughulikia mashauri ya rufaani kutokana na uamuzi wa Mahakama ya Awali. Pia Kitengo cha Mahakama ya Rufani kitatoa fursa ya rufaa kwa mtu ambaye hataridhika na uamuzi wa Mahakama ya Awali kuainisha sababu nyingine zinazoweza kutumika kuwachukulia hatua ya kinidhamu Majaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa Ibara ya 150 sehemu ya 6 ya Mkataba wa Kuanzishwa Jumuiya ya Afrika Mashariki marekebisho haya yatakubalika na kuanza kutumika tu baada ya kuridhiwa na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

HIVYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na manufaa yatokanayo na marekebisho yaliyofanywa katika Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Tanzania na kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Na kwa mujibu wa Ibara ya 63 sehemu ya 3(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Bunge hili katika Mkutano wa Sita sasa litaazimia Kuridhia Marekebisho katika Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liliridhie marekebisho haya ya Mkataba wa Jumuiya wa Afrika Mashariki kama yalivyosainiwa na Wakuu wa Nchi zetu. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na kuungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati aliyoshughulikia Azimio hili, Mheshimiwa Mussa Zungu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni namna 88 (11) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004 naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Masharikiya mwaka 2006 *(Amendment to the Treaty for the Establishment of the East African Community 2006). (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha maoni haya kwa niaba ya Kamati, naomba kutoa salaam za rambirambi kwako binafsi, Bunge hili, wananchi wa Jimbo la Tunduru na Taifa kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Bunge na wengine waliofariki kutokana na ajali ya ndege Jijini Mbeya. Ndugu zetu hawa walikuwa wazalendo na wachapakazi na mauti yao yamewafika wakiwa katika ujenzi wa Taifa hili. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salaam za rambirambi pia kwa niaba ya Kamati yangu napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dr.Asha-Rose Migiro, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Uteuzi huu umeliletea heshima kubwa Bunge lako Tukufu, Taifa letu na Bara la Afrika kwa ujumla. Aidha, kuteuliwa kwake kumeipa nchi hii heshima kubwa katika medani ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nampongeza Mheshimiwa Bernard Membe, Mbunge wa Mtama kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia masuala ya Bunge na Mheshimiwa William Ngeleja, Mbunge wa Sengerema na Mheshimiwa Gaudence Kayombo kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri. Nawatakia kila heri katika kutekeleza majukumu yao mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salaam hizo napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kwa kunipa heshima ya kuwasilisha maoni haya mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo Mheshimiwa Anna Abdallah, Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa Zungu, Makamu Mwenyekiti na wajumbe ambao ni Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimiwa Balozi Khamis Kagasheki, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mheshimiwa Yono

Kevela, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa John Shibuda, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Mohamed Dewji, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama na Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa marekebisho haya ambayo tayari yamekwishatiwa saini na Wakuu wa Nchi wanachama yanalenga kuunda Kitengo cha Rufaa, sio Mahakama ya Rufaa *(Appelate Court)* cha Afrika Mashariki kitakachoshughulikia mashauri ya rufani kutokana na uamuzi wa Mahakama ya Awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki msingi wake ni wananchi *(people centred)* na kwa kuwa Kanuni 88(6) ya Kanuni za Bunge wadau mbalimbali walishiriki mjadala katika Kamati. Kamati inapenda kutoa shukrani za dhati kwa wadau waliotoa maoni yao mbele ya Kamati wakati wa kujadili Azimio hili. Wadau hawa ni pamoja na Wabunge kutoka Kambi ya Upinzani Bungeni na Chama cha Wanasheria cha Tanganyika *(Tanganyika Law Society).*

Mheshimiwa Naibu Spika**,** wadau walioshiriki mjadala walikuwa na hisia zifuatazo kuhusu Azimio hili endapo litaridhiwa:-

(1) Kwamba utaratibu wa kurekebisha Mkataba *(procedure)* huo kwa mujibu wa Ibara 150 (4) utakuwa umekiukwa.

(2) Kwamba utahatarisha uhuru wa Mahakama na usalama wa ajira ya majaji *(Independence of Judiciary and Security of Tenure).*

(3) Kwamba marekebisho haya yanaweza kuwa na msukumo usio na nia njema *(improper motives).*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kujadili Azimio hili kwa kina ikiwemo kuzingatia maoni ya wadau waliofika mbele ya Kamati, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatayo:-

Kamati inawapongeza Wakuu wa Nchi wanachama kuleta marekebisho haya kwa kuwa yanazingatia haki ya msingi ya mtu, taasisi au Serikali ya kukataa rufaa pale inapoona kuwa haijaridhika na maamuzi yaliyotolewa na Mahakama ya awali. *(Makofi)*

Kamati iliona kuwa pamoja na kwamba Ibara ya 150 (4) ya Mkataba inasema kuwa Mwanachama anayetaka kupeleka maoni kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya juu ya mapendekezo ya mabadiliko anapaswa kupeleka maoni hayo ndani ya siku 90. Kamati imeridhika na muda uliotumika kupeleka mapendekezo ya mabadiliko mbele ya Bunge lako Tukufu kwa kuwa wanachama wote walikuwa tayari wameshakamilisha zoezi la kupeleka maoni husika. *(Makofi)*

Aidha Ibara hiyo haizuii wanachama kukamilisha kupeleka maoni na kuanza kufanya marekebisho yanayokusudiwa iwapo upelekaji huo umefanyika mapema zaidi ya siku 90 na kama hakuna mwanachama mwenye maoni tofauti kutokana na maoni hayo. Kwa mantiki hiyo Kamati imeona hakuna utata wowote utakaozuia Bunge lako Tukufu kuridhia mapendekezo ya haya yaliyoletwa na Wakuu wa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Kamati pia ilijadili kwa kina kuhusu athari za kuridhi Azimio hili kwa Uhuru wa Mahakama na Usalama wa Ajira ya Majaji. Mapendekezo haya yamezingatia uhuru wa Mahakama kwa kuwa Ibara ya 26 ya Mkataba bado imezingatiwa. Aidha, Jaji hawezi kufukuzwa kazi mpaka Tume maalum iundwe ili kuchunguza tuhuma zinazomkabili na kisha itoe mapendekezo kwa Wakuu wa Nchi Wanachama kwa mujibu Ibara ya 26 1(a) ya marekebisho hayo. Hivyo Kamati imeridhika kuwa marekebisho yanayopendekezwa hayatahatarisha uhuru wa Mahakama na Usalama wa Ajira ya Majaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wasiwasi pia kuwa Mahakama ya Rufaa inayopendekezwa itakosa kazi za kufanya. Kwa mujibu wa marekebisho Ibara ya 35A Mahakama ya Rufaa *(Appelate Division)* itafanya kazi ya kupitia rufaa itakayoletwa kwake kutoka Mahakama ya Awali *(First Instance Division of the Court).*

Aidha, Wakuu wa Nchi wanachama wanaweza kutengeneza kanuni za kuiongezea kazi Mahakama hii inayopendekezwa. *(Makofi)*

Aidha Kamati ilichunguza hoja kuwa marekebisho haya yana msukumo usio mzuri *(improper motives)* na kuona kuwa kila jambo lina wakati wake. Wakuu wa Nchi baada ya kuona kuwa ipo haja ya kupanua wigo wa kutoa haki kwa wananchi wa Afrika Mashariki waliamua kuanzisha Kitengo cha Rufaa cha Mahakama ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba marekebisho yanayopendekezwa na Azimio hili hayana uhusiano na kutokuapishwa kwa Wabunge wa Kenya waliochaguliwakuingia Bunge la Afrika Mashariki mwezi Novenba, 2006. Umuhimu wa kuwepo kwa Kitengo cha Rufaa katika Mahakama ya Afrika Mashariki unaonekana wazi. Kwa kutokuapishwa kwa Wabunge hao kunawanyima haki Wabunge wa Bunge hilo kutoka Tanzania na Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, shughuli zote zinazohitaji kupitishwa na Bunge ikiwemo Bajeti ya Jumuiya Afrika Mashariki haitakuwepo na kama kutakuwa na matumizi yoyote yanayoendelea yatakuwa ni kinyume cha sheria.

Baada ya kuanza utekelezaji wa Mkataba huu mapungufu kadhaa yameanza kujitokeza na Kamati inashauri iundwe Tume maalum ili kuangalia vipengele vingine vinavyohitaji marekebisho kama haya yanayoletwa sasa ili mapungufu hayo yaondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine naomba kuwapongeza Wakuu wa Nchi wanachama kwa busara na hekima kwa kuona umuhimu wa marekebisho haya kwa manufaa nchi zetu na Jumuiya kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Katibu Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na maofisa wengine kwa kuwasilisa Azimio hili mbele ya Kamati kwa ufanisi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maoni hayo Kamati katika ujumla wake haina pingamizi juu ya kuridhiwa kwa Azimio hili na inaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuliridhia Azimio hili kwa manufaa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika**,** napenda kuwashukuru tena Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kwa maoni na ushauri waliotoa kwa maslahi ya nchi yetu na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ujumla katika vigezo vya *standards and speed*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maoni haya Kamati inaunga mkono hoja. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maoni kuhusu mapendekezo ya kuridhia marekebisho ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu cha 43(5) (b) (c) na 70(2) Toleo la 2004, napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba nilioutaja hapo juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha mimi kusimama hapa kutoa maoni haya. Pili, sina haja ya kukumbusha yale tulioambiwa katika vitabu vyetu vya dini, *Quran* Takatifu na Biblia kwamba kila mtu atayaonja mauti. Lakini ni wajibu wetu pale yanapo mpata mmoja wetu, sisi tuliobaki tuoneshe huzuni zetu kwa msiba huo.

Hivyo basi, naomba na mimi nimuombee rafiki yetu mpendwa na Mbunge mwenzetu Marehemu Juma Jamaldin Akukweti, pamoja na wenzake waliokuwemo katika ajali hiyo. Tunawaombea malazi mema peponi. *Amin.* Naomba pia niwape mkono wa pole familia za marehemu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii vile vile kuwapongeza Waheshimiwa wote waliopata nyadhifa mpya na ninawahakikishia ushirikiano wetu katika kuzitekeleza shughuli ambazo tumekabidhiwa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Bunge la Jamhuri ya Muungano, tunaombwa turidhie marekebisho ya Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki katika nyanja ya Mahakama ya Jumuiya hiyo. Lengo ni kuunda upya Mahakama ya Afrika ya Mashariki kwa kuanzisha Mahakama ya Awali na Mahakama ya Rufaa ya Mahakama hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, maoni yetu sisi ni kuwa marekebisho haya hayakuzingatia utaratibu uliowekwa na Mkataba wa kuanzisha Jumuiya hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuziorodhesha baadhi ya taratibu hizo amabazo hazikuzingatiwa:-

Kwanza, Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki una matatizo mengi ambayo yangehitaji marekebisho. Matatizo haya yamejitokeza zamani sana kuliko linaloambiwa ni tatizo la Mahakama ambalo limejitokeza hivi karibuni tu baada ya mahakama hiyo kuamua kuwa Wabunge wateule wa Afrika ya Mashariki kutoka Kenya wasiapishwe. Kwanza mgogoro huu ni wa Kenya pekee na haungepaswa kufanyiwa marekebisho haya kabla ya Kenya wenyewe kurekebisha tatizo hilo. *(Makofi)*

Pili, ni kuwa kwa nini tunashughulikia tatizo moja tu na hatufanyi marekebisho kwa mambo yote ambayo tunahisi yana matatizo na ni tishio kwa Jumuiya yetu. Suala la kusema hili ni muhimu si kweli kwa sababu na hayo mengine pia ni muhimu na yamejitokeza mwanzo kuliko hili. Mambo haya nitayaelezea baadae kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi mwingine muhimu wa kulitazama Azimio hili ni kwamba Serikali imekiuka Ibara 150(4) na (5) ya Mkataba huo ambazo zinataka nchi wanachama watoe mapendekezo yao ndani ya siku 90 *(with in 90 days)* na kwamba baada ya kumalizika *(after the expiration)* ya siku 90 ambazo wadau wanatakiwa kutoa maoni yao, Katibu Mkuu apeleke maoni hayo kwa wakuu wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha hii ni nyepesi na rahisi na haihitaji maelezo yoyote ya kutilia mwega kwamba ni lazima siku 90 zipite ndio Katibu Mkuu wa Jumuiya apelike mapendekezo aliyoyapata kutoka nchi wanachama kwenda kwa viongozi wa nchi hizo *(Summit)* kwa kupitia kikao cha Mawaziri. Kufanya vingine vyovyote ni kwenda kinyume na Mkataba huo na hivi ni kuvunja Mkataba huo. Vile vile Mkataba huo unasisitiza hata katika utangulizi wake *(preamble)* kwamba ni lazima wadau (wananchi) washirikishwe ipasavyo. Hatukuyafanya hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi yetu inasikitishwa sana kwa Serikali kukiuka matakwa ya Mkataba huo na ndio maana Kambi yetu tukaona kuwa mapendekezo hayo yanakwenda kinyume na matakwa ya Mkataba huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine kubwa ya kukataa mapendekezo haya ni kuwa mabadiliko haya yanaathiri uhuru wa Mahakama na kwa maana hiyo kutokuheshimu utawala wa sheria *(Rule of Law).*

Ibara ya 43(2) ya Mkataba inatoa maelekezo ya kuwa Jaji wa Mahakama hiyo hatoshika nafasi za Kiserikali au Jumuiya na hatojiingiza katika biashara ya aina yoyote ile ambayo italeta mgongano na shughuli zake za mahakamani. Mapendekezo ya Azimio lililopo mbele ya Bunge lako Tukufu ni kuziondoa kinga hizo na kuweka mambo mawili makubwa:-

Kwanza, Jaji wa Mahakama hizi sasa anaweza kushika nafasi ya aina yoyote ile katika nchi mwanachama.

Pili, Jaji wa Mahakama ya Afrika Mashariki sasa anaweza kuchukuliwa hatua na hata kuondolewa na nchi yake wakati wowote na kwa kosa lolote lile.Inaonesha, iwapo nchi mwanachama imemchoka Jaji waliompendekeza inaweza tu kutoa visingizio vya aina yoyote ile na kumwondoa Jaji huyo wakati wowote ule. Hivi ni kupunguza uhuru wa Jaji huyo kwa kuhofia kuondolewa tu kwa sababu uamuzi wake haukumfurahisha mkubwa mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi yetu inaamini kuwa mapendekezo haya yametokana na shinikizo la nchi moja wanachama ambayo haikufurahishwa na maamuzi ya chombo cha Jumuiya, wakati Ibara ya 38(2) ya Mkataba wa Jumuiya inasisitiza kuheshimu maamuzi ya chombo cha Jumuiya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni muhimu sana na tusiwe laini na kukubali mara moja na kwamba pale ambapo nchi moja wanachama haikufurahishwa na uamuzi fulani uliotolewa na chombo kimoja cha Mahakama, basi nchi hiyo iharakishe kufanya marekebisho ya

Mkataba wa Jumuiya. Utaratibu huu haufai  na sio utaratibu mzuri ambao utarutubisha Jumuiya yetu. *(Makofi)*

Kambi yetu ya Upinzani inajua na kufahamu kwamba Rais wa nchi yetu pamoja na Marais wa Kenya na Uganda wameshaweka sahihi zao kukubali mapendekezo ya marekebisho hayo na kwamba tayari Kenya na Uganda wamesharidhia kwa njia zao zisizokuwa za Bunge. Sasa mtego huo ni wa Tanzania kukubali marekebisho hayo ya Jumuiya au kukataa na hivyo kufanya kutetereka tena kwa Jumuiya hii ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumebakiwa na masuala mawili muhimu ya sisi Wabunge kujiuliza, kwanza, je, tuyakubali na kuyaridhia mapendekezo haya hata kama hayakufuata utaratibu wa kimkataba na kufanywa kwa mara ya kwanza sheria muhimu ya Jumuiya kutungwa bila ya kupata ridhaa za wadau (wananchi) wa Afrika ya Mashariki?

Pili tuyakate mapendekezo haya huku tukijua athari zake kwa Tanzania na hatimaye kuutetemesha umoja huu ambao bado ni mchanga sana? Jibu hapa ni lazima tuwe wazi kwa sababu Wabunge siku zote tunatakiwa tuwe imara kulinda Katiba na sheria na hata kiapo chetu Bungeni kinataka hivyo. Ikiwa Katiba (mkataba) imevunjwa lazima tuseme hivyo na tusikubali kufumbia macho. Hapa Mkataba umevunjwa na Kambi ya Upinzani hatukubaliani na uvunjwaji huu, haitawezekana kutoa baraka zetu za kuridhia Mkataba huo. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inaamini kuwa marekebisho hayo yangekuja pamoja na kero nyingine ambazo nazo zingeweza kuiboresha Jumuiya yetu, kwa maana hiyo ni lazima tujaribu sana kuepuka kufanya marekebisho ya Mkataba huu pale yanapotokea matatizo *(crisis)* yaliyoikumba nchi moja wanachama. Pili, Serikali ichukue hatua za haraka katika kupendekeza kufanywa kwa marekebisho mengine muhimu kama vile hatua za kuchukuliwa nchi wanachama pale inaposhindwa kulipa ada yake au pale inaposhindwa kutekeleza yale yaliyokubaliwa; kuwepo kwa utaratibu mzuri na wa aina moja katika nchi wanachama wa kuchagua wabunge wa Bunge la Jumuiya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuwepo kwa mikakati mizuri ya matumizi ya fedha, michango na hata kushirikishwa kwa jamii ya watu wa Afrika Mashariki katika uchangiaji huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuwepo kwa utaratibu wa aina moja wa kufanya mabadiliko ya Mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya na mengine mengi yatasaidia sana kuimarisha zaidi Jumuiya yetu. Tuyafanyeni kwa pamoja, tusifanye udoho udoho *(in piecemeal).*

Jambo lingine amabalo marekebisho hayo yanalenga ni kupunguza nguvu za mahakama kutafsiri mambo yote yanayohusiana na Jumuiya kama ilivyotaka Ibara ya 28 ya Mkataba huo wa Jumuiya. Kwa maana hiyo ni dhahiri kuwa pana mgongano mkubwa baina ya ibara hiyo ya 28, ukisoma pamoja na Ibara ya 30 inayotaka mtu yeyote mwananchi wa Jumuiya kuomba maamuzi kutoka kwa Mahakama hiyo pamoja na kutaka uhalali wa jambo fulani au maamuzi fulani ya chombo kimojawapo cha Jumuiya. Ibara ya 26 inayopendekeza marekebisho ya mahakama hizo ndiyo iliyopunguza nguvu hizo na kwa maana hiyo kugongana na Ibara za 28 na 30 za Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vigumu kutokana na kasoro hizi zote kukubali kwamba Azimio hili liridhiwe. Tunahisi hatutowatendea haki Watanzania wenzetu na hata wananchi wa nchi wanachama wa Jumuiya hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, Kambi ya Upinzani, haiungi mkono kuridhiwa kwa marekebisho haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani na kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ningependa Waheshimiwa Wabunge wenzangu watambue kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati wa Mambo ya Nje. Kwa hivyo, nilipata nafasi ya kulipitia pitia hili Azimio toka kwenye vikao vya Kamati. Niungane na Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Zungu kuwapongeza viongozi wa *Tanganyila Law Society* ambayo kwa kweli maoni yao yaliweza kutufanya kulifahamu vizuri Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaolipinga Azimio hili kwa ujumla wanajenga hoja zao katika misingi mikubwa mitatu. Msingi wa kwanza ni hii *Article 150,* vifungu vidogo vya (2), (3)na (4) kwamba tunakiuka taratibu za kuleta mabadiliko kwa mujibu wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wanasheria wanapokuwa wanaangalia Sheria hawaangalii kwa jicho la kuku kwamba jicho moja linaangalia huku basi linalopita huku halioni mpaka litumike lingine. Wana uwezo wa kutumia jicho la kinyonga wakaangalia pande zote mbili za shilingi. *Article 150,* kifungu kidogo cha (2) kinazungumzia ndani ya siku 30. Maana ni kutoka siku moja mpaka siku hiyo 30. Namba tatu akishaipata hiyo *Secretary General* basi ndani ya siku 90 ahakikishe *Partner States* wanapata hizo *proposals* na namba nne inayopigiwa kelele sana inamwambia ikishafika siku 90 ni lazima *(shall)* ahakikishe kwamba anapeleka hiyo juu.

Sasa ukiangalia hapa kwa jicho moja basi unang'ang'ania wewe siku 90 baada siku 90. Lakini ukiamua kuangalia kwa jicho la kisheria. Panapotokea utata wa tafsiri zaidi ya moja maana kwa tafsiri hii haisemi kwamba kama mambo yenyewe yamekamilika chini ya siku 90. Basi ni haramu kupeleka, hakuna la kukatiza. Maana yake hii ni *ambiguity* na katika maamuzi ya kisheria inapotokea hali kama hii, wanahama kwenye *written rule* na kwenda kwenye *intension of legislatures*. Hivi madhumuni ya sheria hii ilikuwa ni nini? Ndiyo maana hata Miswada ya Waheshimiwa hapa inavyokuja wanakuwa na madhumuni kwanza. Sasa ninapoangalia madhumuni hivyo ni kweli kwamba hata kama wameshamaliza mambo yao ndani ya siku 30, ndani ya siku 15, basi tunafungwa tu kama ng'ombe mpaka zimalizike siku 90. Ndiyo madhumuni ya kutunga sheria hii kweli? *(Makofi)*

Sasa mimi nilifikiria wenzetu wanapoangalia upande huu wa siku 90 waangalie na upande wa pili, je, madhumuni ya kutungwa hii ilikuwa ni kuchelewesha mambo yetu au kufanya mambo yetu au kufanya mambo yaende kwa *spirit* ile ile ya mshikamano, umoja na amani? Kwa kigezo hicho mimi naona hakuna *procedure* tuliyoikiuka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini msingi wa pili ambao wenzetu wanausimamia katika kulipinga hili ni kwamba maamuzi ya kutengeneza kitengo cha Mahakama ya Rufaa basi kina wanyang'anya mamlaka, uhuru na kujiamini Majaji. Kwa maneno yao wenyewe

inawanyang'anya *Authority, Independence* na *Integrity* na wanakimbilia sana kuitaja hiyo *Article 26* kuifananisha na 27. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinga ya Majaji imejieleza wazi katika *Article* na katika marekebisho yanayotakiwa kufanywa kwamba haitatokea tu kwamba *summit* imekaa wacha Rais mmoja hata wenyewe watatu hawawezi wakakaa kule juu wakasema Jaji fulani na fulani *out*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawawezi mpaka kwanza kuwe na *ad' hook Tribunal* itakayopitia kwa utaratibu ule ule wanaoshughulikiwa Majaji katika kuajiriwa na kufukuzwa au kuachishwa ambao unatumika katika Jumuiya ya Madola. Sijui wasiwasi huu umetengenezwa? Maana mimi niliuangalia kwa siku tatu najadili hii, sioni mahali panapoonyesha wasiwasi wa namna hii. *(Makofi)*

Lakini hivi kwa nini tumefikia hapo kwa Jumuiya yoyote ya kiungwana, fursa yoyote ya kiungwana ni haki ya msingi. Humu ndani ya Bunge mtu akibamizwa bamizwa hapa ana haki ya kukata rufani. Kuna wanaokwenda kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, kuna wanaokwenda kwenye Kamati za Kanuni. Lakini hata katika utaratibu wa nchi yetu ukitoka kwenye Mahakama ya Mwanzo kule unakwenda mpaka unafikia *Court of Appeal.* Haiwezekani tu kwamba mimi nimeamuliwa *ABC* hapa halafu kuna kuwa ndiyo mwisho nasubiri Mwenyezi Mungu ataamua nini. Si uungwana hata kidogo na haya yapo ndani hata ya familia zetu. Mnagombana, mnasuruhishana na marafiki mkishindwa mnakwenda kwa wazee ndiyo utaratibu. Sijui kwa nini haki ya kukata rufaa katika suala hili la Afrika Mashariki linaonekana gumu mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitajaribu kutoa sababu baadaye lakini kuna sababu ya tatu inatolewa kwamba eti mabadiliko haya yanafanywa kwa dhamira isiyokuwa njema. Hili nalo halimo kwenye marekebisho yenyewe. Ni hisia za watu ambao hawalipendi Azimio lenyewe lakini ndani ya marekebisho hii dhamira isiyo njema haionekani. Inasikitisha sana kuonekana kwamba eti Watanzania tukiridhia jambo hili tunaburuzwa na Wakenya.

Mimi nalifikiri kinyume chake, kama haturidhii Azimio hili maana yake tunakubali kuburuzwa na Wakenya na sababu ni hizi zifuatazo, mtu ambaye anaadhibiwa ni yule ambaye amefanya kosa. Mtu ambaye hajafanya kosa hapaswi kuadhibiwa kwa kosa la mwingine. Uchaguzi huu tulioufanya wa Wabunge wa Afrika Mashariki tulitumia Kanuni na ukiangalia Kanuni kwenye *Annex III* pale. Tumefanya hii kwa mujibu wa *Article 50* ya *Treaty* yenyewe na katika *Annex* hiyo ukienda kwenye Ibara ya 15 na 16 naomba ninukuu. "*Person to the provisions of article 52 (1) of the Treaty. The election of the candidate as a member of the East African Legislative Assembly may be declared void only on an election petition."*

Namba 16: *"The procedure, jurisdiction and grounds for declaring void the election of such member shall be the same as provided by Law for election petition in respect of members of the National Parliament."*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua taratibu zetu hapa, watu wakiwa na kesi, hata wewe Naibu Spika ulikuwa unaendelea ukiwa Mbunge mpaka hiyo Mahakama itakapotoa uamuzi wake ndiyo Ubunge wako unakoma. Katika mazingira haya kwa sababu eti ya mgogoro wa huko Kenya, Wabunge wetu ambao wamechaguliwa kwa njia halali kwa mujibu wa Kanuni, leo

wanazuiwa kuapishwa, wanazuiwa kufanya kazi zao kwa sababu tu nchi jirani wana matatizo. Tukikataa kulipitisha Azimio hili maana yake ndiyo tunakubali kuburuzwa na Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukikubali kulipitisha maana yake tunasema sisi ni nchi lakini kwa kweli anayekosa ndiye anayeadhibiwa. Hawa wanasheria wanamsemo wao na mimi napenda kuunukuu: *"It is quiet Law that only the guilty parties face the race* of *the Law but not the innocent."* Katika suala hili Wabunge wa Uganda ni *innocent* hawapaswi hata kidogo kuangukiwa na rungu hilo. Kwa hivyo, habari hiyo ya *improper motive* haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tukiwa kwenye Kamati tarehe 5, wenzetu viongozi wa Upinzani walikuja kama *observers* na kiongozi wa Upinzani Bungeni alitahadharisha kwenye Kamati: "Tunakwambieni hata kama mtakaa kwenye Kamati ya chama sisi hatutapitisha." Kauli ile siku ya tarehe 6, mimi niliirudia kwamba haikuwa ya kiungwana. Ni jambo halipendezi kutufikiria Wabunge wa CCM tunapotoa maamuzi hapa tunafanya maamuzi kama *rubber ink* kwamba hatuna hoja eti tunaburuzwa. Sisi ndani ya CCM maamuzi yetu hayatokani na wingi, yanatokana na thamani na uzito wa hoja yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni kinyume ya wanavyofikiria wenzetu kwamba wanaburuzwa kama ng'ombe aliyetogwa shimere, hata kidogo. Wala hatuyumbi kama bendera kufuata upepo hata kidogo. Ndiyo maana tukiwa na msimamo tunakuwa na msimamo wa kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wasiwasi kwamba hapa tunakusudia kuchanganya kuchanganya suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki na Azimio hili. Haya ni mambo mawili tofauti. Tunafahamu msimamo wa wenzetu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walikutana wakaita vyombo vya habari na wakatoa msimamo wao kwamba kuanzishwa kwa Jumuiya hiyo ni jambo *illegal,* halikufuata taratibu kwa sababu tunawajua wanatuambia wenyewe. Lakini kwa suala hili la Mahakama la Bunge la Afrika Mashariki hawawezi hapa wakasimama wakatuambia kwamba hilo hawalitaki. Huko ni kutafuna muwa na kupiga mruzi wakati huo huo. Haiwezekani. Kwa sababu Bunge la kwanza lilipoanza wenzetu walishiriki na walipata mwakilishi wao. Hata juzi hapa tulipofanya uchaguzi huu na wao walileta viongozi wao humu ndani na wengine kwa sababu walikiuka tu utaratibu ikawa haiwezekani waendelee walilipuka humu ndani.

Kwa hiyo, suala la Bunge wanajua umuhimu wake kwamba linatakiwa lifanye kazi. Nashangaa kwamba leo wanatuambia isije hii peke yake yaje na masuala mengine yote ya Afrika Mashariki tuyajadili kwa pamoja. Hakuna duniani mtu anapofanya kila jambo kwa wakati mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata matatizo yetu ndani ya familia hatuwezi kuyashughulikia kwa siku mmoja yakaisha na kama tunasubiri hivyo hatuendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya ya Afrika inawahusu raia wa Afrika Mashariki, sisi ni watu na kwa kawaida si *static,* ni *dynamic*. Linaloonekana leo sio tatizo, kesho lazima litakuwa tatizo tu. Kwa hiyo, mambo hayafanani kwamba tumalize matatizo yetu yote ndiyo tuyalete humu ndani tukifikiria kwamba ndiyo mwisho wa matatizo. Mwisho wa matatizo kwa mwanadamu ni pale anapoingia kaburini, basi. Mradi upo hai matatizo yanaendelea tu. Kwa hivyo, nafikiri huko si mahali kuzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa imani yangu kabisa napenda niwaombe Waheshimiwa Wabunge wezangu tuliunge Azimio hili kwa sababu moja tu Wabunge tuliwachagua waweze kuapishwa na kufanya kazi zao. Lakini mbili haki ya Kikatiba na haki ya kibinadamu ya msingi kwamba nikionewa hapa nikakate rufaa pale. Lakini tatu kwa sababu tu ya kuamini kwamba katika maisha ya mwanadamu hakuna anayemaliza kila kitu siku moja. Leo unaweza kuona si muhimu keshokutwa likawa muhimu. Kwa hivyo, si dhambi kufanya mabadiliko haya leo kwamba kwa nini hayakuanza toka mwanzo, leo hapa lazima kuna nia ambayo si njema. Mwanzoni tuliona hakuna sababu hiyo na ndiyo maana unaweza kutoka nyumbani umevaa shati mikono mirefu ukisikia joto unakunja. Maana ile baridi uliyotokanayo kule haipo tena. Lakini ukavaa shati koti umelitundika hapa baadaye baridi ikaja ukalivaa. Ndiyo mwanadamu anavyokwenda hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele ya Bunge lako Tukufu. Lakini kabla sijasema la msingi nianze kwa kutoa masikitiko yangu kwamba kwa kawaida Bunge linapaswa kufanya maamuzi kwenye taarifa iliyo kamili. Kwa bahati mbaya kama *documents* zilizogawanywa leo asubuhi, ndio hizi tu ambazo mimi nipewa hapa ndani ya ukumbi na kama wenzangu waliopewa ndio hivi na tunatakiwa kufanya maamuzi, basi kuna tatizo la msingi katika maamuzi ndani ya Bunge ya hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepewa Azimio lakini hakuna vipengele vya *Treaty* vinavyofanyiwa *amendment,* hata vile vilivyotolewa kwenye Kamati ambako mimi nilihudhuria kama *observer* navyo pia havipo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanajadili kitu ambacho hakipo isipokuwa Azimio tu. Ninaliona jambo hili ni la hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, wataalamu wanasema usipofanya utafiti si vema ukaongea, na usiposoma si vema pia ukazungumza, kwa sababu unaweza ukazungumza maneno yasiyo ya msingi, lakini ukawa hodari kwa kuongea na ku-*convince* lakini msingi hautokuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina tatizo la msingi sana hapa nianze kwa kukubaliana na yale aliyosema msemaji wa upinzani, nayaunga yote mkono, sasa niseme yale ambayo hakuyakazia niyakazie na muda ukitosha nitarudia kufafanua aliyoyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza kabisa, nia ya njema ya Serikali kwamba mabadiliko haya yana nia ya kuanzisha mahakama ya rufani ili tupate haki, na mimi nakubali mahakam ya rufani ni muhimu. Lakini naomba kusema kwamba katika hili si kweli kwamba nia ni kuanzisha mahakama ya rufani ili kupata hiyo haki, kwa nini nasema hivi, nia hiyo ingekuwa kweli, la kwanza kabisa lingefanyika hapa ni kuleta marekebisho ya Ibara ya 27 yanayozungumzia *jurisdiction* ya mahakama yenyewe. Ibara ya 27 imebakia ilivyokuwa, kwa hiyo, hata mahakama inayoundwa haikupewa *jurisdiction* tena na hivyo hata leo mkipitisha haitafanya kazi na msingi wake ni kutengeneza mgogoro katika jumuiya na kutengeneza mgogoro mbaya zaidi katika shirikisho ambalo tunaliendea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si vema masuala ya kisheria yakajadiliwa kwa msingi wa kisiasa, ninaelewa kwamba sheria inaanza kwenye siasa na siasa na sheria si rahisi kutenga. Lakini ukijadili misingi ya kisheria kwa misingi ya kisiasa tu basi unapotea na utafika mahali

tena sio nchi ya *Good Governance* wala *rule of law* ambayo ni misingi ya nchi yoyote ambayo ni ya utawala wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili wala si kweli kama tulivyosema kwamba sasa hivi mahakama *East Africa* ilivyokaa haki isingetendeka kwa sababu hakuna mfumo wa *appeal* (wa rufani). Ibara ya 27 kama ingefanyiwa kazi na vyombo vyetu vya Serikali inatoa nafasi ya rufani baada ya hukumu moja kutolewa taratibu za rufani zingetolewa, sina muda wa kusoma, naomba kila mmoja mwenye *Treaty* asome. Bahati mbaya hata Wabunge hapa ndani sidhani kama *Treaty* yenyewe wanayo, wanaamua kitu ambacho hawana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka ili muda wangu usiishe, naomba turejee, labda niseme kabla sijaenda huko, niseme kwamba kwa bahati mbaya, mwenzetu ameeleza hapa vizuri Waziri, kwamba kuna mgogoro ndani, kulikuwa na mgogoro uliotokana na uchaguzi wa Wabunge wa Afrika Mashariki na utaratibu wa sheria ambao ni *Good Governance* na *rule of law*. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge umesema Naibu Waziri au Waziri?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alitamka hivyo. Tayari tuna hukumu ambayo imekuwa mahakamani na imetolewa tarehe nadhani ni juzi ni *ruling* kwa *application* namba tano ya mwaka 2007 na naomba kwa ruksa yako ni nukuu. Kuna wanaofikiri ni Wapinzani wamepata hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alisema hivyo, tayari tuna hukumu ambayo imekuwa mahakamani na imetolewa nadhani ni juzi. Ni *Ruling* kwa *Application* Namba 5 ya 2007. Kuna wanaofikiri Wapinzani wamepata hizi *documents* kwa sababu wanataka kupinga, naomba kusema, Wapinzani tunafanya kazi yetu, tunatafiti, tunatafuta *records* na hizi ni *Public Records*. Kwa hiyo, tunapoongea hapa, tunaongea kitu tulichokifanyia kazi, hatuongei tu kwa sababu tunapiga *blah blah,* tumetumwa na watanzania tufanye kazi kwa vitu vilivyo na uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Majaji wanasema, naomba kunukuu: "*While we are anxious to refrain from the merits and the process of amending the Treaty and reaction to an interim court order, we are constrain to say that any reasonable court will conclude as we are inclined to do that this application was brought more out of a desire to delay the hearing, the reference, than a desire to ensure that the applicant receives a fair hearing. In our view, this is tantamount to abuse of court process ...*" Sasa ni ndefu, sitaendelea. Popote pale unapoingilia taratibu za mahakama zinazoendelea mahakamani, ni *abuse of court process*. Nchi inayojali sheria, haiwezi kuingilia taratibu za mahakama, itangojea mahakama imalize, halafu itachukua hatua ambayo inafikiri inafaa. Hapa hatukufuata utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende Kanuni ya *Treaty* ibara ya 38. Ibara ya 38(2) inasema, iwapo kuna mgogoro umepelekwa mahakamani, yaani Mahakama ya *East Africa*, inakataza kabisa na ninaomba nitumie maneno yaliyotumika *"Shall refrain; the Partner State, shall refrain from any action." Any action* ni sawa na hii tunayofanya ya kukimbia Bungeni kupeleka marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Treaty* tuliyoipitisha ndani ya Bunge, inatukataza kuchukua hatua yoyote. Tumefanya kazi hiyo, tunapeleka Bungeni kwenda kuchukua hatua eti tutafute haki. Taratibu zote za *court* zinasema kwamba, kuna mgogoro utatatuliwa kwa misingi ya

Mkataba ulioko na kama kuna tatizo, taratibu nyingine zitafuata baada ya mgogoro ule kumalizika mahakamani.

Tumekwenda kinyume na ibara ya 38 na nchi yoyote inayokuwa tayari kupindisha taratibu hizo, basi nchi hiyo unaweza kujiuliza; je, kwa mambo mengine makubwa, baadae tukiingia kwenye Shirikisho kutatokea nini? Naomba tujiulize na tufikirie mara mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, *background* ya namna tunavyotaka kupitisha hili, naweza kuzifahamu. Ninaelewa kwamba, tulitaka ku-*salvage situation*, ni *situation* ya kisiasa. Lakini hatuwezi ku-*salvage situation* ya kisiasa, kwa kuingia kwenye mgogoro wa kisheria. Kama tunahitaji ku-*salvage*, basi tutafute njia ya kisiasa, ambayo haina mgogoro wa kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme pia kwamba, imegusiwa hapa kwamba, wenzetu wa Kenya na Uganda nao wamekwisha kupitisha. Mheshimiwa Waziri, ameisema. Naomba niseme kwamba, kwa taarifa tuliyonayo, kama ni ya kweli au si ya kweli, sijui, lakini taarifa tuliyonayo ni kwamba, Kenya imepitisha bila kupita Bungeni na sasa hivi kuna mgogoro wameshaupeleka mahakamani, kwa sababu ni kinyume cha Katiba ya Kenya, ibara ya 135 na 145. Kilichopelekwa Arusha, kimepelekwa kwa kupitia Baraza la Mawaziri, lakini Katiba ya Kenya inataka ipitishwe. Sasa, Kenya wana matatizo yao, sisi Tanzania si lazima tufuate matatizo ya Kenya. Sisi ni nchi iliyo na heshima, imepata heshima Duniani kwa kuwa nchi inayofuata utaratibu wa sheria, ni lazima tubaki na utawala wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uganda, kwa taarifa tuliyonayo mpaka jana usiku, labda imefanyika leo, sijui. Lakini kwa taarifa tuliyonayo mpaka jana usiku, Bunge lao limeanza kuketi baada yetu sisi hapa. Hakuna kitu kilichofanana na *amendment* ya *Treaty* katika *Business* ya *Session* hii, kwa hiyo, haijapelekwa kwenye Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekwenda pamoja na wenzangu wa Kamati Ndogo ya Spika, tumekwenda Uganda, tumerudi na Katiba ya Uganda. Mikataba yote kwa sheria ya Uganda ni lazima ipite Bungeni, tena ni yote siyo kama sisi, mengine yanakuja hapa, mengine hayaji, haijaenda kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa hii kama ni kweli, tunajiingiza kwenye mgogoro mkubwa. Tunafikiria kwamba, tuna-*salvage*, lakini tutaingia kwenye mgogoro mkubwa na kuhatarisha hii tunayoiita ni Jumuiya. Tunadhani tunajaribu kuiunda Jumuiya, tunaipenda sana Jumuiya, lakini hatutaisaidia Jumuiya kwa kwenda kinyume na taratibu tulizojiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie kwenye Ibara ya 150 iliyotajwa na mwenzangu, kwa bahati mbaya, ameeleza kwamba, wale wanaopinga, wanakazia ibara vifungu vya tatu na nne, akaishia hapo. Naomba, hii siyo ukweli, ukweli sahihi ni kwamba, ibara yenye mgogoro mkubwa ni ibara ya 150(5) na naomba kunukuu. Sasa kama mwenzangu aliacha kwa makusudi au kwa bahati mbaya, sijui. Ibara hii haitoi uhuru kwa mtu yeyote kurudisha hizi *documents* kabla ya siku 90. Mtu yeyote ambaye ana elimu ndogo ya sheria, ataelewa kinachosemwa hapa. Inasema hivi: *"After the expiration of the period prescribed under paragraph four of this article, the Secretary General shall submit."*

*Prescribed period* ni siku 90, ni sawa na inaposema Sheria yetu ya Uchaguzi, utarudisha fomu ya uchaguzi saa 10.00 jioni tarehe fulani. Wewe umepokea fomu kutoka kwa watu watatu kabla ya saa 10.00, ukafunga milango kabla ya saa 10.00, kitendo kile ni batili. Kitendo

kinachofanywa hapa Tanzania, Serikali ilipeleka kabla ya kupata maoni ya wadau. Kwa kadri ya *Article 7* ya Mkataba huu, wadau wanapaswa kushirikishwa kwa sababu Mkataba unasema, *East African Community* ni *people centered*. Kama ni *people centered*, maoni yetu yalipaswa kuchukuliwa na nchi yetu ndio yawasilishwe. Lakini kabla hawajapata, Serikali ikawasilisha yenyewe na yenyewe ndio inayotakiwa kuwasilisha kwa kweli, lakini imewasilisha kabla ya muda. Kwa hiyo, kama imewasilisha kabla ya muda, *prescribed time* haijaisha, kwa maana hiyo utaratibu umekiukwa na ndiyo maana tunasema kwa msingi wa kukiukwa utaratibu huu, hatuwezi kukubaliana na ibara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki nigongewe kengele, kwa msingi huo na kwa misingi ya *documents* zote tulizonazo, hizi hapa ni za Mkutano wa *Attorney Generals* wote, ninazo hizi *records*. Kenya ndiyo ili-*initiate*, ika-*chair*, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wetu alikuwepo. Nina *Minutes* hapa za Mkutano wa Mawaziri, bahati mbaya Tanzania iliwakilishwa na Naibu Waziri na akasaini. Tena kwa *technicality*, NaibuWaziri haruhusiwi kusaini Mkutano wa Baraza la Mawaziri, *unless* kuna *instrument* inayomteua, kwa sababu *Treaty* inasema Mawaziri. Lakini hakuna *instrument* inayoteua kwa taarifa tuliyonayo, *unless* watuoneshe kwamba, kuna Naibu Waziri, aliteuliwa na Waziri, kuna *instrument* iliyomteua. Kwa misingi hiyo, tuna *records* zote hizi na hizi ni *public documents* ziko mahakamani. Hizi *documents* zimetolewa kwenye Mahakama ya *East Africa*.

Kwa hiyo, Mbunge yeyote anapaswa kuwa na *access*, ili tunapofanya uamuzi, uwe ni uamuzi ambao wataalam wanauita *informed decision*. Hatuwezi kufanya *informed decision* kwenye *page* moja iliyowasilishwa ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ndio mara yangu ya kwanza kuzungumza leo, napenda nitume salamu zangu za rambi rambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti na vile vile kwa Watanzania wengine wote, ambao walipata msiba kipindi kile, sitaweza kutaja majina.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba nitoe pongezi zangu za dhati, kwa Mheshimiwa William M. Ngeleja, pamoja na Mheshimiwa Dr. Batilda S. Burian, kwa kuteuliwa kwao kuwa Mawaziri. Ninaamini kama alivyosema Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, watavaa vile viatu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kwamba aliyetangulia ni mtaalam vibaya sana, nisingependa kurudia vile alivyovizungumza. Ninaamini kwamba, Watanzania wamemuelewa na ninaamini kwamba, Wabunge hapa wamemuelewa, tukiachilia mbali dhana za kisiasa, tukiwa tunaangalia *facts*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nitaanza kwa *statement* ya ujumla, ambayo aliitoa Mheshimiwa Waziri. Nafurahi anasema kwamba, Serikali ya CCM inaheshimu sana Utawala wa Sheria na Katiba. Kwa kweli amenifurahisha sana alivyozungumza hicho kitu. Vile vile ninapenda waiondoe hiyo dhana ya kuonesha kwamba, upande wa huku hatukubaliani na kutengenezwa Mahakama ya Rufaa, hiyo siyo kweli.

Kwa hiyo, tusitake kupotosha umma kwa kuonesha kwamba, sisi tunapingana na mlolongo mzima wa haki. Tukimaanaisha kwamba, haki ikizuiwa sehemu moja, inaweza

ikasuluhishwa sehemu nyingine. Kwa hiyo, naomba tufute hapo, watu wasielewe hivyo, kitu kinachogomba hapa ni utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukiwa kama Bunge, tunakuwa sehemu ya kuvunja Katiba ama sehemu ya kuvunja Mikataba ya Kimataifa, tunakuwa hatuleti picha yoyote nzuri kwa wananchi na kwa Watanzania na kwao hao watu wa nje, ambao tunafikiria tunawabeba, kumbe baadae wanatubeza kwa nyuma, wanatuona hatuna msimamo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile dhana yetu nzima ya kupingana na hiki kitu, hatutaki mambo yaliyotokea mwaka 1977 wakati Jumuiya ya Afrika Mashariki inakufa yatokee. Tunataka vitu viende kwa utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nije moja kwa moja kwenye hoja. Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, alianzia ibara ya 150(5), mimi naomba nianzie ibara ya 150(3), inayozungumzia nafasi ya *Secretary General*. Inasema kwamba, atapokea *Proposal*, naye ndani ya siku 30 baada ya kupokesa *Proposal* anatakiwa aipeleke *Partner States*. Sasa, *Partner States* baada ya kupewa hiyo *Proposal,* ambaye atataka ku-*comment,* anatakiwa afanye hivyo ndani ya siku 90. Hiyo ni ibara ya 150(4). Ibara ya 150(5) inasema, baada ya ku-*expire period* ambayo imekuwa *prescribed above,* ambayo imeelezwa juu ni siku 90 na siyo siku saba, kama Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, anavyotaka tuamini, imesema siku 90. Kwa hiyo, tusitake kutumia njia za kupindisha pindisha sheria ili kuweza ku-*justify* tunachokifanya. Mkubali kwamba, hii ni siasa basi, lakini si vinginevyo, Mkataba uko *clear*, mpaka siku 90 zikiisha.

Tena dhana hiyo ya siku 90 ni wadau, kwa sababu ndani ya Mkataba inaeleza wazi kabisa, lazima kuwe na *consultation* ya wadau. Sasa huwezi kusema ndani ya siku saba ambazo wakubwa walizifanya, wadau waliweza kuwa *consulted*. Huo si ukweli, ni uwongo na wao wanalijua hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika *Article* 26(1)(a), inahusiana na kuadhibiwa kwa Majaji au ni kwa jinsi gani Majaji wanaweza kutolewa katika ofisi. Ukiangalia Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano, ibara ya 107(a), inazungumzia kuwa mamlaka yenye kauli ya mwisho kutoa haki katika Jamhuri ya Muungano ni Mahakama. Mihimili Mitatu iliundwa kwa kujua kwamba, kuwe kuna *checks and balances*, wale watu wanaangaliana, mmoja asimzidi mwenzie. Mahakama kwa kuwa ndiyo mamlaka ya mwisho ya kutoa haki, sisi kabisa tukaona katika hayo marekebisho, ambayo yalikataliwa tuliyofanya 2005, tukijua fika kwamba, Jaji anateuliwa na Rais, itakuwa ngumu sana kwa huyu Jaji kufanya kitu kinyume na Rais anayemteua.

Kwa kufahamu hilo na kwa kuwa tuko mbele ya Kenya na Uganda, ambavyo kama Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, alivyokuwa akieleza juzi kwamba, Mahakama ya Juu inatoa amri lakini hawatekelezi. Sisi tukaenda mbele zaidi kwamba, Jaji hawezi kuondolewa hivi hivi tu na *Committee* itakayoundwa na Rais. Jaji anaondolewa na Kamati itakayoundwa na Rais, pamoja na Wajumbe kutoka *Commonwealth*. Iko kwenye ibara ya 110(a), mabadiliko 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kwamba, kuna wajumbe ambao lazima wawe nusu kutoka nchi nyingine za *Commonwealth* na wengine kutoka Tanzania, itakuwa ngumu kabisa kwa maamuzi hayo kuwa kuna upendeleo. Vile vile Katiba inajieleza wazi kabisa kwamba, maamuzi ya Kamati, pasipokujali Rais anasema nini, kama Rais Rais amesema

wafukuzwe, Kamati ambayo inajumuisha Majaji kutoka nchi nyingine, ikiona huyu hajatenda kosa, inasema kwamba, huyu aachiliwe na mamalaka ya Rais yanakuwa hayapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ambao tuliliona hili na tukaliweka kwenye Katiba yetu, ndio tunataka sasa hivi kubariki hiki kitu katika *East African Treaty*. Hili ni kosa na ninajua mnajua kuwa ni kosa na mnajua kwamba, tunavunja Katiba ya nchi yetu, achilia mbali hiyo *Treaty* yenyewe tunayoizungumzia hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuja katika suala la jinsi ambavyo Majaji sasa wanaweza kuondolewa kwa mujibu wa *Treaty* yetu, ambayo mmetuletea hapa. Wanasema kwamba, *Summit* itapendekeza *Tribunal* na hiyo *Tribunal* itakuwa na uwezo wa kumfukuza Jaji, pamoja na yale makosa mengine waliyoyaonesha, kwa kosa lingine lolote. Sasa sisi tunahoji, hilo kosa lingine lolote ni nini; kwa sababu kosa lingine lolote maana yake ni makosa zaidi ya yale yaliyokuwa-*mentioned*? Sasa tuambie uhuru wa Jaji utatokeaje, kwa sababu tujue hapo kuna ubinadamu. Mimi huwezi kuniambia leo umeniteua kuwa Jaji, ninajua kabisa mimi huu ndio mkate wangu, halafu ninajua kabisa kuna kitu kingine ambacho kinaweza kikaja kikaniondoa bila sababu ya msingi, kwa nini nisifanye jinsi ambavyo *Head of States* watakavyotaka. Ndiyo hicho hicho Kibaki alichoonesha na bahati nzuri kwa kudra za Mwenyezi Mungu, ameshindwa kesi *East African Court of Appeal*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hatutegemei sisi kwa ufahamu wetu, kufanya vitu vya kuburuzwa buruzwa na Wakenya, lazima tutumie akili, tuangalie sheria inasema nini. Kama tulikuwa hatutaki, tungefanya vile *from the first place,* kwa nini tuwe kama Uganda wasiozingatia utawala wa sheria na vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua kwamba Mkataba utapita, ninajua vizuri kuwa utapita, lakini *at the end of the day,* mnajua kwamba mnachokifanya mtahukumiwa wenyewe na wapiga kura na Watanzania wote, mtajijua wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kitu kilichonishangaza zaidi kwa kuonesha kabisa kwamba hiki kitu kilifanywa *intentionally*, nilibahatika kuingia kwenye Kamati, sasa ikawa kwamba, hii sheria itakayopitishwa, ambayo itapelekea kuundwa kwa Mahakama ya Rufaa, itakuwa inasikiliza hata kesi ambazo zimeamuliwa sasa hivi na hii Mahakama iliyopo. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu hayupo hapa, lakini yule wa zamani yupo, nadhani anajua *principles* za Sheria kwamba, sheria hai-*apply retrospectively* au haifai kabisa kutunga sheria ambayo madhumuni yake ni kuondoa haki ambayo sasa hivi ipo, yaani unajua mimi leo nina haki ya kula ugali, kesho unatunga sheria unasema, Halima jana haukuwa na haki ya kula ugali na leo ugali ni kinyume cha sheria, unanifunga; hiyo siyo sahihi. Kwa hiyo, ninajua tutapitisha vile vile lakini tunaenda kinyume na taratibu, wakati huo huo tunajisifu tukisema kwamba, nchi yetu inafuata Utawala wa Sheria na Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, kwa sababu sitataka kuzungumzia hiki kipengele cha 32, ambacho kinazuia, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, amekielezea vizuri sana. Nimalizie kwa kusema kwamba, kama kweli tunasema tunajali maoni ya wananchi na kama ambavyo tulijifanya tunawa-*praise Tanganyika Law Society,* ambao walikuwa wanakuja kutusaidia, lakini mmepuuza mawazo yao, hapa tunafanya kuwabeza tu, kila mtu anayezungumza anawasifu, wakati mkijua kabisa walichokisema hamjakifanya. Kwa hiyo, kama kweli tunasema tunajali maoni ya watu, hatutapitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikiliza kwa makini sana mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na wachangiaji wengine waliofuatia baadae.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukaongea muda mrefu sana hapa, tukichambua maudhui ya mabadiliko yaliyoko mbele yetu, tukichambua utaratibu uliotumika, lakini kuna ukweli mmoja ambao ningependa niusisitize hapa kwamba, suala tulilonalo mbele yetu sasa hivi ni *fée accompli* (nikitumia neno la Kifaransa). Limeshafanyika, hatuwezi kulirejesha tena. Nalisema hilo kwa kuangalia utaratibu uliopo chini ya ibara ya 150 ya Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sihitaji kuisoma, nimeipitia mara nyingi mno hii, nitaeleza tu. Chini ya Ibara hiyo ya 150, mabadaliko ya Mkataba huu, yanaweza yakaletwa na nchi mwanachama au Baraza la Mawaziri, ndiyo hatua ya kwanza. Hatua ya pili, hayo mabadiliko yanapelekwa kwa Katibu Mkuu, Katibu Mkuu anayapeleka kwa nchi wanachama kutoa maoni. Baada ya nchi wanachama kumaliza mchakato wa maoni, wanarudisha kwa Katibu Mkuu, ambaye kupitia Baraza la Mawaziri, yanakwenda kwa Marais wetu watatu, ambao wakishaweka mikono yao, basi inafuatia sasa *process* ya *ratification,* kama ambavyo leo hii *document* iko mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hatuna nafasi ya kufanya mabadiliko kwenye maudhui ya hii hoja iliyoko mbele yetu hapa. Hatuna nafasi kwa sababu Marais wameshasaini, sisi ni kuridhia ama kutokuridhia, ndilo lililoko mbele yetu hapa. Nasema hivyo kwa sababu lazima tutambue, chini ya ibara ya 150, tuna vitu viwili muhimu; cha kwanza ni hatua za kufuatwa na hilo halibishaniwi hapa. Nimewasikiliza sana hata ndugu zangu upande wa upinzani, hawalibishanii hili la hatua za kufuatwa, ina maana hatua zilifuatwa. Ila ni muda kati ya hatua moja na nyingine, ambao unapendekezwa kwenye ibara ya 150, huo ndio unaobishaniwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi pengine niende mbele kidogo; kwa nini hatua zilizofuatwa hazibishaniwi ? Hazibishaniwi kwa sababu chini ya ibara ya 150 ya Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki, hatua hizo zimeainishwa kwa uwazi kweli kweli; utaanza hapa, utakwenda hapa, utarudi hapa. Lakini tatizo la muda uliowekwa kati ya hatua moja na nyingine, unaruhusu tafsiri mbali mbali, ndilo tatizo moja kubwa la msingi na naomba wenzangu Wanasheria muelewe. Unaposema *within 30 days,* kama ndugu yangu Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir alivyosema mwanzoni, una maana gani? Una maana ndani ya siku 30 au siku 30 zenyewe. Sasa kama ulitaka ziwe siku 30, kwa nini usiseme siku 30 tu; unaposema *within,* ina maana toka siku ya kwanza mpaka ya 30, ndiyo *within* yenyewe? Sasa siyo kwamba nasema ndiyo *position* nzuri sana, lakini ndiyo hivyo ni kwamba, ibara ya 150 imeruhusu tafsiri tofauti tofauti na kwa hiyo ndugu zangu, Serikali za Afrika Mashariki, zimetumia hiyo *loophole* na kwa sababu tafsiri ni pana, zimetumia hiyo na kuleta mabadiliko katika kipindi ambacho kiko *within* hizo siku 30 na *within* hizo siku 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mambo mawili ya kuyafanya hapa na yote yatakuwa ni kwa manufaa yetu wote, upande wa Upinzani na wa Chama Tawala humu ndani, kwa sababu wote tunajenga nchi moja, tunajenga Afrika Mashariki moja. La kwanza, ni hatua ambayo inatakiwa ifanyike ya haraka, ya pili *long term*. Ya kwanza ni kuridhia haya mabadiliko. Tumeambiwa na Mheshimiwa Waziri muhusika kwamba, wenzetu Wakenya na Waganda

wameridhia. Mimi naomba nisijiingize kwenye swali la wameridhia vipi? Hilo mimi nafikiri halituhusu. Wameridhia vipi, kama kuna maswali, ni Waganda wenyewe wayashughulikie, kama ni Wakenya washughulikie mambo ya kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la msingi hapa ni kwamba, Rais Mwai Kibaki, ameweka mkono kwenye haya mabadiliko, Wakenya wameridhia, Rais Yoweri Museveni kaweka mkono, Waganda wameridhia. Sasa Rais wetu sisi vile vile ameweka mkono, tena siyo Rais tu hivi hivi, huyu ni Rais mwenye ridhaa kubwa kupita Marais wote wa Afrika Mashariki. Mtu aliyechaguliwa na zaidi ya asilimia 80 ya wapiga kura, siyo utani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema tu jamani, haitakuwa sahihi kisiasa, sisi si Wanasheria hapa. Tukianza mambo ya malumbano ya sheria hapa, haitusaidii chochote, sisi ni wanasiasa. *After all,* kama nilivyosema, ibara ya 150 imekaa vibaya, inaruhusu *interpretation* ya kila aina. Unaposema *within*, kwa nini useme hivyo? Nikitaka siku 90, nasema *ninety days*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kaka yangu hapa Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, amesema hata Sheria ya Uchaguzi inasema saa fulani, uwe umeleta fomu zako, ukizidisha imekuwa batili. Ni sahihi kabisa hiyo *interpretation*, lakini Sheria inasema nini?

Imetaja kabisa *at 4.00 p.m.* Hii haisemi, inasema *within*. Sasa na hii ya Uchaguzi ingesema urudishe *within seven days*, wewe Jumatatu unarudisha, Jumanne unarudisha, Jumatano, Alhamis, mradi tu uko katika zile siku. Kwa hiyo, tunasema hii ibara ya 150 ina matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa la pili, napendekeza nini? La kwanza nimeshasema naomba Waheshimiwa Wabunge kwanza, nilisema kwamba ni suala la kuamua sasa hivi. Nawaombeni wote pamoja na kaka yangu Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, ambaye najua anajua Sheria sana, kuna hitilafu kwenye ibara ya 150, hiyo hitilafu inaruhusu *interpretation*. Wote hebu turidhie kwanza hili, halafu sasa tuitatue hii hitilafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa pili, hoja inayolalamikiwa ni ya muda kati ya hatua moja na nyingine. Inalalamikiwa siyo na watu wa kuwapuuzia, hoja ikitolewa na mtu anayeitwa Jaji Warioba, ni mtu ambaye sisi Watanzania wenyewe, tunajivunia kama Jabari la Sheria, siyo hapa Tanzania, Duniani kote. Waliokuja hapa, *Tanganyika Law Society* ndiyo *cream* ya Wanasheria ya Tanzania. Kwa hiyo, hoja zao siyo za kuzipuuzia, ni za msingi kweli kweli. Lakini ninachosema hizo hoja bado hatujazitupa nje, tuna nafasi ya kuzi-*take into account,* kwa sababu kuna mambo ya kufanya sasa hivi na ya kufanya baadae.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachopendekeza ni kwamba, hoja ya wenzetu kwamba, Msingi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni msingi wa *Consultation* na hata ibara ya 150 ukiisoma, siyo moja kwa moja, mpaka utumie tunaita sisi kwenye Sheria, *the doctrine of harmonious interpretation*, ndiyo unapata hiyo kwamba ziwe siku 90 ili kuruhusu wananchi kushiriki. Sasa, badala ya sisi kutumia hizo dhana za kisheria na za tafsiri kuweza kupata hiyo maana, hapana. Ndio maana nasema Mchakato umeshaanza na nafikiri hata Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, atatusaidia hapa. Nafikiri mchakato wa kuibadilisha *Treaty,* wamesharuhusu uanze. Hebu tushiriki kwenye huo mchakato, tuweze kui-*improve* hiyo ibara ya 150, iweze sasa kusema moja kwa moja, wananchi wa Afrika Mashariki kwenye mabadiliko wawe na sauti zaidi kuliko Serikali zao kutumia siku saba au kumi, wakafanya mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalisema hilo kwa sababu moja kubwa; nakumbuka mwishoni mwa mwaka 2001, Rais Mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Tatu ya Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alikuja kuongea na Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, tulikuwa Manyara. Kitu ambacho sitaweza kukisahau tena, alisema historia ina sura mbili; sura ya kwanza, ni mwalimu mzuri sana na historia inakuwa mwalimu mzuri pale ambapo wewe uko tayari kuiangalia na uko tayari kujifunza kutokana na yaliyotokea nyuma ili pale ulipoteleza, uweze kuchukua tahadhari. Lakini sura ya pili ya historia, ni hakimu katili kweli kweli; anakuwa katili kwa sababu historia hiyo kama wewe hutaki kuangalia ulikotoka, kwa sababu yale yaliyokuangusha yatakuangusha tena na madhara yake yatakuwa mara mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki hapa, ikavunjika kwa kishindo kikubwa kweli mwaka 1977 na ilivunjika kwa sababu tunazozijua. Hatua ya kuifufua ilianza mwaka 1993 na tunamshukuru sana mzee wetu, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, ndiye alikuwa mwanzo kabisa wa *efforts* za kuirudisha *Community*. Wameirudisha mwaka 1999, ndiyo tunapata huo Mkataba na kuanza Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mimi naweza kusema, tumeanza vizuri, kwa sababu tumeonesha kwamba, tunajali historia na tuko tayari kujifunza kutokana yaliyotokea nyuma. Tumejifunza mawili na yako ndani, ukisoma huu Mkataba unasema kwamba, Jumuiya ya Kudumu haijengwi toka juu kuja chini, inajengwa toka chini kwenda juu. Pili, ili uwe na Jumuiya imara, lazima iwepo *constant consultation* na watu wa kawaida, ndiyo maana kwenye *Treaty* hii kuna vipengele vingi vinavyosisitiza kwamba, hii Jumuiya ni *people centered*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwenye dibaji ya huu Mkataba, tunasema kwamba, Jumuiya ya 1977, ilivunjika kwa sababu kadhaa na sababu mojawapo ni kutokuwahusisha Wana-Afrika Mashariki kwenye masuala ya Jumuiya. Kwa hiyo, nasema tuna ulazima wa kuiangalia upya katika mchakato wa kuangalia, huu siyo *immediate long term,* kuangalia ibara ya 150 iseme *categorically* kwamba, kuna umuhimu kwenye mabadiliko ya *Treaty* yoyote, wananchi wawe *involved* na uwepo muda mrefu wa kujadiliana. Kwa sababu *Treaty* yenyewe hii haikutokana na Serikali zenyewe, tuliujadili hapa mwaka mzima, Afrika Mashariki nzima, nafikiri Waheshimiwa Wabunge, mnakumbuka.

Nimalizie kwa kusema, Tanzania ina nafasi ya pekee katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuzionesha njia nchi nyingine. Sisi tumekomaa zaidi kwa demokrasia. Mimi nakumbuka miaka ya 1960 kwa sababu ninapenda sana *constitutional history,* mwaka 1964 alitokea mtu aliyemwomba Baba wa Taifa, Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, awe Rais wa maisha. Kipindi hicho kilikuwa ndiyo kipindi ambacho kila mtu Afrika anataka kuwa Rais wa maisha, Banda alishakubali, Mwalimu alikataa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi nishiriki katika mjadala juu ya hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri, mwenye dhamana ya Ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kaka yangu Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, juu ya marekebisho ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, wenye malengo ambayo yameainishwa kwenye azimio.

Napenda nimhakikishie kaka yangu, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, mimi nina azimio na kiambatisho cha marekebisho yaliyopendekezwa katika kurekebisha Mkataba huo, ninayo

hapa. Sasa ametuambia kama hujafanya utafiti, hurusiwi kuzungumza. Mimi nilimtarajia angeachia hapo hapo, kwa sababu ana kiambatisho, asitoe *criticism,* yeye alikuwa na Mkataba tunaourekebisha. Mimi nilidhani angesema sasa naomba tuahirishe Bunge, makabrasha yakamilike ili mjadala unoge. Akaendelea na Mkataba wa zamani ule, sasa wa zamani unaweza ukaubeba. *(Makofi)*

Lakini hoja yetu nianzie pale ambapo rafiki yangu, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, alipokazia. Hapa Bungeni sisi tuko kama Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kila mtu hapa ana *professional background* yake. Kuna walimu, kuna *engineers*, kuna wanasheria, madaktari na kadhalika, sasa wengine wanaweza wakadhani nimesimama hapa kama *advocate*. Nimesimama kama Mbunge wa Muleba Kusini na kilichoko mbele yetu ni Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambao mapendekezo yake, yamefuata taratibu chini ya Mkataba ambao tunataka kuurekebisha kwa *speed* mno. *(Makofi)*

Lakini taratibu kama alivyosisitiza Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe na walionitangulia kuunga mkono hoja, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, hatimaye ilifika kwenye chombo *(organ)*, ambacho kinaheshimika chini ya Mkataba *(Summit).* Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Mashirikiano ya Afrika Mashariki na Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ameelezwa ameweka sahihi kwenye marekebisho hayo kwenye *Summit*. Baada ya kutoka Baraza la Mawaziri na Afrika Mashariki, wakawapelekea kwenye *Summit* na hayo chimbuko lake, naipongeza Serikali yetu kwa kuwa wawazi. Mheshimiwa Waziri, ametueleza bayana kabisa chimbuko lake nini, ni Kenya wamepeleka mapendekezo, Tanzania haijapeleka yanakataliwa na Kenya, Uganda haijapeleka yanakataliwa na Tanzania. Kenya wameanza changamoto, tuna haya na wakajenga hoja kuna dharura. Marais wetu wakasema kweli dharura tunaiona wakaweka saini. *(Makofi)*

Sasa Bunge letu hili la sehemu mbili, Rais na sisi Wabunge, tukijadili Miswada yetu ya Sheria na tumeshapitisha mingi Awamu ya Nne hii, Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, hachelewi kuridhia yale ambayo wakati tunajadili anakuwa hayupo, lakini ana namna ya kutufuatilia, ana *machinery*. Sasa yeye katuwakilisha, naye Rais amechaguliwa na wananchi na wa Kenya pia na wa Uganda, dhamana ya uwakilishi siyo ya Wabunge tu, Marais tena wana dhamana kubwa kuliko yeye. Wao wamefanya tathmini ya mambo mengi sana na wanao Wanasheria Wakuu kutoka nchi zao na wao wakawaambia kisheria mambo yanakuaje na hawa Marais wetu wakasema kwa mazingira haya tuende hivi. *(Makofi)*

Mimi nampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kukubali kuweka sahihi kwenye mambo haya. Nafurahia wale wote wanaokubali kwamba, tukubaliane na Rais turidhie uwakilishi wake na siyo kuhamisha matatizo ya migogoro, tukaanza kuonesha hatuna imani hata na Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, amesema aliyeweka saini kule ni Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Jamani, Mheshimiwa Rais kafika pale kaweka sahihi kwa jambo ambalo liko mbele yetu, unamhoji hata Naibu aliyemteua? Mimi nadhani tungekuwa tunahoji kwamba, aliyeweka sahihi siyo Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, siyo sasa unalishusha tena unaweka mpaka kwa aliyeweka saini kwenye Baraza la Mawaziri. Hapa tunajadili yaliyoletwa na *Summit* siyo ya Baraza la Mawaziri, sisi kiwango chetu ni mambo ya *Summit*, tusije tukaipotosha jamii. *(Makofi)*

Mimi nitafurahia mtu kama unajenga hoja za nia njema, ningefurahi kama hoja za ndugu zetu Wapinzani, zingesema dhamira ya marekebisho haya tuna mashaka nayo. Kwa sababu hiyo ni huru kila mtu unaweza kumtilia mashaka yeyote, ni haki yako hasa ukisema nina ushahidi umekwenda kwa *speed* mno kunikubalia, mimi nimekuomba mkopo wewe unanipa haraka haraka unasema hizi hapa, utashangaa mbona wewe unanipa haraka. Dhamira yako nini sasa, lakini nimeshakupa nilichoomba, sasa ulichokuwa unataka nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa najaribu kusikiliza kwa makini hapa Katiba gani imevunjwa nikaikosa, nikawa nasema hivi nisiseme nilianza kufikiria kutosimama kuchangia nikasema hivi ni Katiba gani imevunjwa? Maana yake inatumika maneno mawili Katiba, Mkataba, sasa nikasema Katiba gani; Katiba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki sijawahi kuiona, ninaujua Mkataba! *This Treaty,* siyo Katiba ni Mkataba. Katiba ziko kwenye nchi wanachama na mimi ninayo hapa. Nilikuwa nasoma ya kwetu, maana mnaweza mkasema nasema bila kusoma, hata hii aliyosema Rais na sisi Wabunge kuwa sehemu moja ya Bunge ni ibara ya 62. Sasa ile ibara ya 110 (a) aliyoisoma Mheshimiwa Halima J. Mdee kwamba, kumtoa Jaji kwa sababu yoyote ile, inakiuka Katiba yetu. Mimi niliposoma Katiba, nikakuta maneno hayo hayo kwenye Katiba na mkitaka nitawasomea ili nianze kusema maneno mengine, nisije nikapoteza muda mwingi, maana wanaweza kusema tunazusha, wananchi wanaweza wakatushangaa. *(Kicheko/Makofi)*

Mbunge unapaswa useme ulichokuwa na uhakika nacho, tumekumbushwa asubuhi. Ibara ya 110(a)(4) inasema: "Ikiwa Tume iliyoteuliwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (3), itamshauri Rais kwamba, Jaji ambaye habari zake zimechunguzwa na hiyo Tume, aondolewe kazini kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya, basi Rais atamwondoa kazini Jaji huyo anayehusika na utumishi wa Jaji huyo utakuwa umekoma." *(Kicheko/Makofi)*

Sasa ukiyasoma kwa Kingereza ndiyo hayo hayo yamo kwenye mapendekezo ya marekebisho, ambayo ni kiambatisho alichonacho Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa. Ngoja niwaambie kitu kimoja, kwa sababu hii ni katika kuweka misingi, kwa nini mimi nimekubali. Mheshimwia Naibu Spika, *Speed* kweli huwa inaleta mashaka, huu mchakato wa *fast track* hata na mimi huwa sipendi mambo ya haraka haraka. Wanasema haraka haraka haina baraka, ingawa hizi methali huwa zinatuchanganya sana, wengine wanasema chelewa chelewa utakuta mtoto siyo wako, sasa ina-*nullify almost* hata ile ya kwanza ya haraka haraka. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa nataka kutafuta, hivi kwa nini Marais wetu wanatambua kwamba, chini ya ibara ya 13(6)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haki ya rufaa ambayo haina mjadala, hata ndugu zetu wa Upinzani, bahati nzuri wameikubali hiyo kwamba, haki ya rufaa ni ya Kikatiba katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kwenye Mahakama ya Afrika Mashariki, ilikuwa haipo. Sasa hiyo, si *credit* kweli kwa Marais kwamba, wameona mapungufu haya na haki ya kukata rufaa ni jambo la dharura, isipopatikana hivi kweli wewe umenyimwa haki yako, mtu anakuambia haki ya rufaa ni ya Kikatiba, lakini umechelewa kwenye sheria tuliyonayo hapa haipo, kwa mujibu wa mazingira ya Kitanzania, tutasema hiyo sheria ni batili kwa sababu haikuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo, haki inabaki. *(Makofi)*

Kwa hiyo, suala la *concept* ya *retrospective aspect,* ambayo anaisema Mheshimiwa Halima J. Mdee, kwa haki ya kula ugali ni sawa na rufaa. Huwezi ukamwambia sasa mtu unasema aliyeona ameathirika jana, umnyime haki ya kukata rufaa kama taratibu inawezekana

kwamba, sasa tutakuwa tumerudi sasa *retrospective* kwanza humpigi *penalty,* unampa haki. Mimi nimeshindwa kumwelewa, amesema unachukua haki yake unakwenda kumfidia, wewe rufaa ipo. *(Makofi)*

Halafu kitu kingine kinachonistaajabisha, hapa hatupitishi hukumu ya kutengua maamuzi ya Mahakama ya Afrika Mashariki. Mimi nimesikiliza hapa tusije tukapeleka hisia kwa wananchi wetu kwamba, Bunge la Afrika Mashariki, tumekaa kutengua maamuzi ya Mahakama ya Afrika Mashariki, si kweli. Mimi najua jana hukumu imetoka, wamekataa maombi ya *Attorney General* wa Kenya, ni mazingira yanayosikitisha. Lazima tuwe wakweli, anayemwambia mtu ukweli, anampenda zaidi. Chimbuko lake ni kukataa kuapisha Wabunge wa Kenya, wakaathiri hata wa kwetu, ni mgogoro upo lazima tukiri. *(Makofi)*

Sasa namna ya kulitafutia dawa, mimi vile vile sifurahii, mtu anaweza akasema ukimpa mtu haki ya rufaa, umemshushia hadhi aliyetoa hukumu. Mimi nadhani ninamwongezea heshima na *confidence* kwamba, mimi nimeamua leo weka rufaa tutaona, kwa nini huyu ana mashaka na rufaa, kwa nini uwe unataka hukumu yako iwe *final*, hiyo *integrity* ya maamuzi hayo, mimi naamini hakuna jaji anayeweza akaifurahia sana kwa heshima zote, lazima useme nenda popote pale. Mimi niwahi kuwa Hakimu, nenda Mahakama ya Rufaa, wakitengua basi, kwa sababu huna *interest* kwenye mambo, wewe unachagua *facts,* sheria na kanuni, Jaji huwezi kuwa na *interest* kwenye maamuzi, acha iende kwenye rufaa, wakitengua basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nisipoteze muda mwingi sana, nataka kusema kwamba, tukubali kuridhia na tumpongeze Mheshimiwa Rais wetu, alichofikiria ndicho dhamana yetu. Hatima ya nchi yetu iko kwenye Bunge hili, tukishirikiana na Rais na hatima ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, iko chini ya Mabunge yetu matatu. Walioko nje wanachostahili ni kutuletea habari na Tanzania tumefanya vizuri, *Tanganyika Law Society,* ambayo na mimi ni mwanachama, wamesikilizwa na Kamati.

Sasa unaweza kusema, mawazo yao hayakubaliki lakini yamesikilizwa. Tutaendelea kuyafanyia kazi, kurekebisha Mkataba wa Afrika Mashariki, mwisho siyo leo. Leteni hata mtu, anaweza akaenda, sasa tukijifanya Mahakama hapa ya Afrika Mashariki, tukaanza kutafsiri hata Mkataba ni vichekesho, kwa sababu Mkataba wenyewe unasema mwenye uwezo wa kutafsiri Mkataba huu ni Mahakama hiyo ya Afrika Mashariki, siyo Mabunge. Unaona hilo tena ni mtego mwingine, tunataka kuingia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi ningependa kushukuru, kama Mwanasheria na Mbunge, hatima ya nchi yetu, iko kwenye hiki kitu, kwa kushirikiana na Mheshimiwa Rais. Sisi tukiweka hapa, atajua na sisi tunamwani. Sisi Miswada yetu akiweka sahihi, tunagonga baada ya taarifa ya Spika. Yeye anatuletea sahihi yake, kwamba na mimi ni Rais, najua maslahi ya nchi, najua maslahi ya Afrika Mashariki, tusonge mbele, tutasahihishana mbele, sisi hatukatai kwanza hamfurahishi Rais, tufurahishe wa Kenya kwamba, tunajua kukataa. Hasira za mkizi hazitatusaidia. Tukiikimbia Jumuiya ya Afrika ya Mashariki tutairekebishaje, tuwemo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hii ndiyo maana ya Bunge, mwingine anasema na wengine wanasikiliza, halafu mwishoni tunaamua.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukamilisha hoja yangu. Kwanza, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia, kwa kuzungumza na waliochangia kwa maandishi. Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe na Mheshimiwa Wilson M. Masilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aliyechangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa. *(Makofi)*

Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, yote waliyoyasema, tumeyatilia maanani na kwa kweli lazima niwashukuru sana wote. Lakini kwa namna ya pekee, nawashukuru Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe na Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, kwa sababu wamenifanyia kazi, ambayo pengine ningechukua muda mrefu hapa kuifanya. Wamejibu katika michango yao, hoja karibu zote ambazo zilitolewa, ambao waliamua kulikataa azimio hili na wametoa ufafanuzi ambao kwa kweli nawashukuru. Napenda niseme tu kwamba, haya ambayo yamesemwa, sisi tutayatilia maanani na tutayafanyia kazi. Nataka nitoe mfano mmoja tu ambao Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, aliuliza swali kama kuna mchakacho. Nadhani kuna mchakato umeanza wa kurekebisha Mkataba. Napenda nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba, ni kweli mchakato wa kurekebisha Mkataba wa Afrika Mashariki, umeanza na mambo mengine baadaye yatatiliwa maanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo napenda niliseme kwa ufupi pia katika muda ambao nimepewa ni hili la Mheshimiwa Halima J. Mdee. Ilikuwa bayana kwamba, Msemaji wa Upinzani alisema kwamba, wao hawaungi mkono hili, kwa hiyo si kusingizia kwamba wameona kwamba hawaungi mkono. Inanisikitisha kwa sababu kwa upande mmoja, hoja walizozitoa nimezielewa, lakini pia hawakutoa kitu kipya na wala hawakutoa suluhisho lolote kwa mujibu wa matatizo ambayo yalikuwepo. Lakini ndiyo Bunge letu na ndiyo uzuri wa Tanzania, tunabishana, tunabadilishana mawazo na hatimaye tunafanya uamuzi. Kwa hiyo, mimi nawashukuru kwa yale yote ambayo wameyasema.

La tatu, nataka nitoe ufafanuzi, kumetolewa maneno hapa kwamba, Kenya ndiyo walioleta ushauri na Kenya ndiyo walitoa mapendekezo na Kenya ndiyo walio-*chair* mkutano. Inatoa picha kama vile Kenya imekuwa ikiziburuza nchi nyingine. Sasa kama huelewi kinachotokea, hii ndiyo inaweza kueleweka. Nataka niseme kwamba, Kenya sasa hivi ndiyo Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo, kwa maana hiyo, panapokuwa na vikao vya ngazi za maafisa, afisa wao ndiyo Mwenyekiti, panapokuja kwenye ngazi ya Makatibu Wakuu, Katibu Mkuu wao ndiyo anakuwa Mwenyekiti wa Kikao. Kwa Mawaziri pia, Waziri ndiyo anakuwa Mwenyekiti. Hivyo hivyo kwenye ngazi ya Marais. Sasa nadhani niliona hili nilieleze ili lisitoe taswira mbaya.

Mwisho, nataka niseme kama nilivyosema awali kwamba, ukweli ni kwamba, nchi yetu ina historia ya kutukuka juu ya Utawala Bora na Utawala wa Sheria. Katika haya tuliyoyafanya, kama ambavyo Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe na wengine walivyosema, kwa kweli ni mwendelezo wa sera na mfumo wetu wa ndani katika sera yetu ya mambo ya nje. Tunaunga mkono na tunasimamia yale ambayo kwa hakika ndiyo tunayafanya hapa ndani. Mimi nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tena kwa kumalizia

kwamba, mlipitishe azimio hili, mliunge mkono na tuunge mkono maamuzi ya wakuu wetu wa nchi, ili marekebisho haya yaweze kuanza rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kuanzishwa Jumuiya ya Afrika Mashariki liliridhiwa na Bunge)*

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**(Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo Tanzania wa Mwaka 2007**
***(The Law School of Tanzania Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

*(Muswada wa Sheria uliotajwa hapo juu, ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza)*

**(Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo Tanzania wa Mwaka 2007**
***(The Law School of Tanzania Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuchukua fursa hii, kuwashukuru kwa dhati, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora, Mheshimiwa George Malima Lubeleje na Wajumbe wote wa Kamati, kwa ushauri, maoni na mapendekezo, ambayo yametuwezesha kukamilisha mchakato wa kuwasilisha Muswada mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupitia Muswada, Kamati ilitoa mapendekezo ya kufanya marekebisho katika ibara kadhaa za Muswada. Baada ya kutafakari mapendekezo ya Kamati, Serikali imekubali kufanya marekebisho katika baadhi ya ibara za Muswada kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Marekebisho *(Shedule of Amendment)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kwanza, kutoa maelezo mafupi kuhusu dhana ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo, kwa kutambua kuwa uelewa wenu utasaidia kwa kiasi kikubwa, kujadili na kisha kupitisha Muswada huu. Dhana ya mafunzo ya sheria kwa vitendo ni utaratibu unaotumika katika nchi nyingi za Jumuiya ya Madola, zinazofuata mfumo wa sheria unaojulikana kama *Common Law*. Mfano wa nchi hizo ni Kenya, Uganda, Zambia, Malaysia, Malawi na Uingereza. Mafunzo hayo hutolewa baada ya wanafunzi wa Shahada ya Kwanza ya Sheria, kuhitimu mafunzo ya nadharia.

Lengo la utaratibu huu ni kuwapa nafasi wahitimu, kufanya mafunzo ili kuimarisha uelewa na kupata ujuzi wa kazi katika fani ya sheria. Aidha, mafunzo hayo hutolewa kupitia taasisi zinazoitwa *Law Schools*. Mafunzo ya aina hii, hutolewa kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Baada ya kipindi hicho, wahitimu hufanya mitihani ya uwakili ili kuwawezesha kusajiliwa na kisha kuingia kwenye soko la ajira moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa mafunzo ya aina hiyo uliopo hivi sasa, unaojulikana kama *Internship Programme,* ulianzishwa mwaka 1974. Mafunzo hayo yamekuwa yakitolewa na kuratibiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Wakati wakiwa mafunzoni, wahitimu au wanafunzi, walikuwa wanahesabiwa kuwa waajiriwa. Hii ni sababu wahitimu wote walikuwa wanapata ajira katika Utumishi wa Umma. Kati ya mwaka 1974 na 2002, idadi ya wahitimu wa Shahada ya Sheria, ilikuwa ndogo na kutokana na idadi hiyo kuwa ndogo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliweza kusimamia mafunzo hayo kwa ukamilifu.

Kutokana na ongezeko la idadi ya wanasheria waliohitimu katika Vyuo Vikuu mbalimbali, pamoja na ongezeko la vyuo vinavyotoa mafunzo ya taaluma ya Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imepata ugumu wa kusimamia ipasavyo, mafunzo hayo. Aidha, wahitimu wanapaswa kusimamiwa na Wanasheria Waandamizi. Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko la wahitimu, imekuwa vigumu kuwapata Wanasheria Waandamizi, wanaoweza kuwasimamia wanasheria wote wahitimu kikamilifu. Vile vile imekuwa ni vigumu kupata nafasi za ofisi za kutosha za kuwaweka wahitimu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kwamba ni lazima kutimiza matakwa ya Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 *(The Advocates Act, 341)* na masharti ya Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali *(The Attorney General Discharge of Duties Act, 2005),* zinazoelekeza kwamba, wahitimu wa mafunzo ya sheria sharti wapate ujuzi unaotakiwa ili kuweza kumudu kazi za uwakili, Serikali imeona umuhimu wa kuanzisha Taasisi ya Mafunzo ya Sheria, ili kuwezesha wahitimu wa Shahada ya Sheria kupata ujuzi unaohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maudhui ya Muswada, taasisi inayopendekezwa itakuwa ni chombo cha umma, kama vile kilivyo Chuo cha Mahakama cha Lushoto, yaani *The Institute of Judicial Administration Lushoto* na kitasimamiwa na Baraza la Taaluma ya Sheria, ambalo limeundwa na Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 *(Council for Legal Education)*. Kazi za kila siku zitasimamiwa na Bodi ya Wakurugenzi, kama ilivyoainishwa katika Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unapendekeza kuwepo kwa kipindi cha mpito. Katika kipindi hicho, vyuo vinavyotoa mafunzo ya Shahada ya Sheria kwa hivi sasa, vitatoa mafunzo hayo kwa kusimamiwa na Baraza. Ili kulipatia Baraza uwezo wa kisheria wa kusimamia mafunzo hayo, inapendekezwa Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 ifanyiwe marekebisho yatakayowezesha kukidhi azma hiyo. Hivi sasa Baraza la Taaluma ya Sheria lipo na kiutawala, linasimamiwa na Jaji Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu sita. Sehemu ya Kwanza ya Muswada yenye ibara ya kwanza, ya pili na ya tatu, inapendekeza masharti juu ya mambo ya utangulizi, kama vile jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria, watumiaji wa sheria na tafsiri ya maneno mbali mbali yaliyotumika katika sheria.

Sehemu ya Pili ya Muswada yenye ibara ya 4 hadi ya 12, inapendekeza kuanzishwa kwa Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo, Taasisi nyingine na Idara za Chuo, kuundwa kwa Kamati ya Mafunzo kwa Vitendo na Mitihani na kuainisha majukumu yake. Vile vile inahusu namna ya kujiunga na Taasisi, malipo ya ada na mafunzo ya sheria kwa vitendo na uteuzi wa

Mkuu wa Chuo. Vile vile inapendekeza majukumu mbalimbali ya kiutawala na uteuzi wa watendaji chini ya sheria hii; kuanzishwa kwa Baraza la Chuo, pamoja na madaraka na majukumu yake.

Sehemu ya Tatu yenye ibara ya 13 hadi ya 20, inapendekeza uteuzi wa Mkuu wa Chuo, kuanzisha Bodi ya Utawala, mamlaka na majukumu ya Bodi. Aidha, yapo mapendekezo yanayoweka utaratibu wa malipo ya posho kwa Wajumbe wa Baraza la Chuo, Madaraka ya Baraza la Chuo, kukasimu majukumu yake na kutoa madaraka kwa Baraza la Chuo kutengeneza kanuni mbalimbali. Sehemu ya Nne inayohusu ibara ya 21 hadi ya 25, inapendekeza masharti yanayohusu masuala ya fedha, makadirio ya Bajeti ya mwaka, mahesabu na ukaguzi wa fedha, ripoti ya fedha na uwekezaji wa mapato ya chuo.

Sehemu ya Tano inahusu masuala ya jumla na uwezo wa Waziri, kufanya marekebisho katika Jedwali. Vile vile inatoa uwezo kwa Baraza la Chuo, kutunga sheria ndogo na masharti ya mpito.

Sehemu ya Sita inapendekeza kuifanyia marekebisho Sheria ya Mawakili, Sura ya 341, kwa lengo la kuunda Sekretarieti, ambayo itafanya kazi za kila siku za Baraza la Elimu ya Sheria, ambalo limeanzishwa na Sheria ya Mawakili. Sekretarieti hiyo, itasimamia kwa karibu, uendeshaji wa elimu ya taaluma ya sheria kwa vitendo katika kipindi cha mpito, yaani kabla majengo ya shule hayajakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, nakushukuru wewe na kupitia kwako, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. RAMADHANI A. MANENO – (k.n.y. MHE. GEORGE M. LUBELEJE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, naomba kusoma maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo ya Tanzania mwaka 2007 *(The Law School of Tanzania, Bill 2007).* Kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo ya Tanzania wa Mwaka 2007, inafahamika kwa (*The Law School of Tanzania Bill, 2007).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu iliujadili Muswada huu tarehe 30 Januari, 2007 katika kikao kilichofanyika katika Ofisi ya Bunge, Dodoma. Katika kikao hicho, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali, kuhusu mapendekezo yaliyokusudiwa katika Muswada huu kama alivyoeleza na mtoa hoja. Maelezo hayo yaliwasilishwa na Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, Waziri wa Katiba na Sheria, akisaidiwa na Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mheshimiwa Johnson P. M. Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na wataalamu wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali ya kuwa na Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo nchini, kwa kuzingatia kuwa hivi sasa kumekuwepo na idadi kubwa ya wahitimu wa sheria, hali ambayo imesababisha kutokuwepo kwa wasimamizi *(supervisors)* wa kutosha, kuwasimamia wahitimu hao wanapokuwa kwenye mafunzo ya vitendo *(internship),* kwa upande mmoja. Kwa upande mwingine, idadi hiyo imesababisha kukosekana kwa asasi, mashirika au taasasisi za kutosha za kuwapatia mafunzo hayo. Kamati inaamini kuwa, utaratibu huu mpya utaweka chombo kimoja kitakacho wawezesha wahitimu mbalimbali kukusanyika, pamoja na kupata taaluma ya sheria kwa vitendo kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kukubaliana na mapendekezo hayo, ningependa kugusia maeneo machache, ambayo Kamati yangu ilitaka ufafanuzi na kutoa ushauri. Kwanza, ni kuhusu ibara ya 11(2) ya Muswada, inayoweka sharti la lazima kwa wanafunzi wote watakaojiunga na Taasisi, kulipa ada itakayowekwa na Bodi ya Taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilitafakari kwa kina kipengele hiki. Kwanza, iliona kwamba, mafunzo ya vitendo ni sehemu muhimu katika kukamilisha sifa za kuwa mwanasheria. Zaidi ya hayo, ibara ya 12(3) ya Muswada, inaweka sharti la lazima kwa mhitimu wa Diploma ya Uzamili ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo *(Post-graduate Diploma in Legal Practice)* kuwa na sifa ya kuwa Wakili wa Kujitegemea au kuajiriwa katika utumishi wa umma.

Hata hivyo, kwa kuwa mafunzo hayo ni ya lazima kwa wahitimu wa sheria na kwa kuwa sharti la kulipa ada kwa ajili ya kujiunga na mafunzo hayo ni la lazima, kwa kuzingatia hali halisi ya maisha ya Watanzania walio wengi, ilionekana kwamba, si wahitimu wote watakaoweza kulipa ada hiyo. Hivyo, Kamati inashauri kuwa ni vizuri Serikali iangalie uwezekano wa kuwakopesha wanafunzi, watakaosajiliwa katika Taasisi hii katika utaratibu unaofanana na mikopo inayotolewa kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu nchini, kuwawezesha wahitimu wote kujiunga na mafunzo hayo muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ibara ya 13(1), inayompa mamlaka Waziri, kumteua Mkuu wa Taasisi, baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ingawa Bodi ya Taasisi imehusishwa kwa kiwango fulani katika mchakato wa kumpata Mkuu wa Taasisi, Kamati inaona kwamba, kuhusishwa huko hakuipi mamlaka ya kutosha, ikilinganishwa na Taasisi au Vyuo vingine vya elimu ya juu, ambapo Makamu Mkuu wa Chuo, huteuliwa na Baraza la *Senate.* Kwa sababu hiyo, pamoja na mamlaka ya Waziri, Kamati inashauri kuwa, Bodi ihusishwe kikamilifu katika mchakato huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda nimalizie kwa kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Aidha, nawashukuru Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Johnson P. M. Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalamu wao wote, kwa maelezo yao ya ufasaha mbele ya Kamati. *(Makofi)*

Vile vile napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati, kwa michango yao mizuri, waliyoitoa wakati wa kuujadili Muswada huu. Naomba niwatambue kama ifuatavyo: Mheshimiwa George M. Lubeleje, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Athumani S. M. Janguo, Mheshimiwa Rajab Ahmad Juma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa

Fatma Mussa Maghimbi, Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa na Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Emanuel Mpanda, Ndugu Ernest Zulu na Ndugu Charles Mloka, kwa kuihudumia Kamati na kutayarisha maoni mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani, kwa niaba ya Kununi ya 43(5)(c) na Kanuni ya 70(2). Nashukuru kwa hilo na ninaanza kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani.

Mhehismiwa Naibu Spika, napenda kusisitiza juu ya kifungu cha *interpretion.* Kifungu hiki nilikizungumzia wakati nikitoa mchango wangu katika mjadala wa Muswada wa Marupurupu ya Majaji. Kwa hiyo, nategemea kuwa ikija tena Miswada, Wizara itatoa jina sahihi la Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 9(4) kinapendekeza kuwa, Baraza la Chuo ndilo litaweka muda wa Wajumbe wa Kamati ya Mafunzo kwa Vitendo na Mitihani kuhudumia Kamati hii. Kambi ya Upinzani inaona kuwa, Baraza limepewa mamlaka makubwa sana, ambayo linaweza kuyatumia vibaya. Sheria nyingi zinazoanzisha Bodi, Mabaraza na Kamati mbalimbali, huwa zinaainisha bayana, muda na vipindi vya Wajumbe kuhudumia vyombo hivyo. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, muda na vipindi vya Wajumbe kuhudumia Kamati hii, vitajwe bayana kwenye sheria mama, badala ya kulipa Baraza mamlaka haya makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 11(2), kinapendekeza kuwa, wanafunzi wote ambao wamekubaliwa kujiunga na chuo hiki, lazima walipe ada ya mafunzo. Hivi sasa wanafunzi wengi wa taasisi za elimu ya juu, wanapata mikopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi. Hata hivyo, Sheria inayohusika na mikopo ya wanafunzi, haitoi fursa ya kuwapa mikopo kwa wanafunzi watakaojiunga na chuo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mafunzo yatakayotolewa na chuo hiki, yatakuwa ni mwendelezo wa mafunzo ya shahada ya kwanza ya sheria, ambayo ni mbadala wa mafunzo ya Sheria kwa vitendo *(intenship),* yanayotolewa sasa kwa wanafunzi waliomaliza shahada ya kwanza ya sheria. Kwa kuwa mafunzo hayo yatakuwa ndiyo sharti la kuweza kufanya kazi za uanasheria na kwa kuwa wanafunzi watakaomaliza shahada ya kwanza ya sheria watalazimika kujiunga na chuo hiki ili waweze kukubaliwa kufanya kazi za uanasheria.

Pia kwa kuwa wengi wao walikuwa wanasoma shahada ya kwanza kwa mkopo wa Serikali, ambao unatolewa tu kwa wanafunzi wa shahada ya kwanza. Kwa kuwa utaratibu wa sasa wa kuwapatia mkopo wanafunzi wa shahada ya kwanza, unaishia kwenye ngazi hiyo tu na siyo kwenye mafunzo mengine baada ya shahada ya kwanza, hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaona kuwa, wanafunzi wengi watashindwa kumudu gharama za mafunzo hivyo, watakosa sifa

za kuruhusiwa kufanya kazi za uanasheria. Kwa sharti hili, itasababisha watu wa kipato cha chini wasisome fani ya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii inapingana na dhana ya kuanzisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi, ambayo inalenga kutoa fursa kwa wanafunzi kupata mikopo kwa ajili ya kugharamia mafunzo yao ya shahada ya kwanza. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa, chuo hiki kisianze kufanya kazi mpaka utakapowekwa utaratibu mzuri wa kuwakopesha wanafunzi fedha za kugharamia mafunzo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mapendekezo hayo machache, nawashukuru kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe mchango wangu kidogo. Awali ya yote, napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ili kuweka utaratibu wa kudumu, ambao utakuwa mwepesi kuweza kuufuatilia. Mimi nitakwenda kwenye Muswada moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nipate maelezo zaidi katika *clause* ya nane, kumetumika neno *by-laws*, *clause 27(1)* na *clause* hiyo hiyo kifungu kidogo cha pili, *by-laws.* Halafu katika *clause* ya 16(2) na *clause* ya 20(1), imetumika *rules.* Sasa nilitaka tu kuelewa hizi zitakavyotumika, kwa sababu Mheshimiwa Waziri, wakati anatoa hoja yake alisema, Bodi itatunga Sheria Ndogo *(By-Laws).* Mimi ninavyoelewa, Waziri ndiye mwenye madaraka ya kutunga *by-laws.* Sasa hapa ninataka tu kuelewa, je, ni kwa sababu ile Bodi imejawa na Sheria, kwa hiyo, wana madaraka ya kutunga *by-laws?* Hiyo ni moja ya ufafanuzi.

Eneo lingine kwa kweli ni masahihisho tu, ambayo ungesema Mheshimiwa Waziri akubali. Katika *clause* ya 10(d), pale kuna neno limeandikwa *candidates who has,* nadhani mmeiona hiyo*, page* ya *51 clause* ya *10(d). Candidates who has,* nadhani ibadilike hiyo, iwe *candidates who have.* Halafu katika *clause* ya 16 ukurasa wa 54, *clause* ndogo ya kwanza, pale kuna *powers give directions* nadhani pale kuna *to* inakosekana *(powers to give directions)*. Mimi kama mmoja wapo niliyehusika kutunga hizi, nadhani yangefanyika marekebisho hapo. Nimeangalia katika karatasi ya marekebisho hamna. Ndiyo nimeyataja haya ili tusichukue muda mrefu wakati wa Kamati ya Bunge Zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *clause* ya 23, kuhusu Ukaguzi wa Hesabu, kifungu kidogo cha pili, Mkaguzi Mkuu *(Controller and Auditor General),* amepewa kazi ya kuangalia hesabu za Taasisi hii. Mimi ninavyojua, hii ni *Public Corporation,* sasa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ana kazi kubwa sana kwenye Wizara za Serikali na Halmashauri.

Kwa hiyo, nadhani tusimfunge yeye peke yake tu kukagua Hesabu za Taasisi hii, nadhani tumpe nafasi yeye mwenyewe au Mkaguzi ambaye atamchagua. Tumpe hiyo nafasi ili tusimfunge kwamba, lazima aende kwenye hizi *Public Corporations,* huku kwenye Serikali lazima yeye mwenyewe afanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, nasema kwamba, naunga mkono hoja hii, pamoja na haya maangalizo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii, nikushukuru tena kwa kuendesha Bunge lako vizuri, wakati nawasilisha Muswada huu. Naomba vile vile niwashukuru sana Wabunge wote, waliochangia ikiwemo Kamati yangu

na hasa Mheshimiwa Ramadhani Athumani Maneno, Mbunge wa Chalinze, aliyewasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

Napenda vile vile kumshukuru Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mbunge wa Chakechake na Msemaji wa Upande wa Upinzani, kwa maoni yake aliyoyatoa kwa niaba ya Upinzani. Pia napenda kumshukuru Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, Msemaji peke yake kutoka kwa Wabunge kuhusu Muswada huu. *(Makofi)*

Nimefurahi kupata mchango wa maandishi kutoka kwa Mheshimiwa Gosbert B. Blandes na kwa Mheshimiwa Profesa Peter M. Msolla. Nawashukuru wote kwa maoni yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe ufafanuzi au maelezo, kuhusu hoja ambayo imetolewa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora, vile vile na Kambi ya Upinzani kuhusu malipo ya ada kutoka kwa wanafunzi ambao watapitia chuo hiki cha sheria. Kwa kutambua kwamba, zipo gharama zitakazotakiwa kulipwa na wanafunzi watakaojiunga na Taasisi ya Mafunzo ya Sheria na kwa kutambua kwamba, hiyo ni sifa ambayo inatakiwa ili mtu awe amehitimu sheria na kwa kutambua vile vile kwamba, hawawezi kuwa Mawakili bila kupitia chuoni hapo, mimi ninaona hoja hiyo ni muhimu na kwa hivyo, endapo italazimu basi Sheria ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya mwaka 2004, itatumika kwa ajili ya mikopo husika na tutaangalia ni namna gani tutaona kwamba, hao vijana wananufaika au wanapata fursa ya kupata mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati ilihoji au ilitaka kuboresha kuhusu uteuzi wa Mkuu wa Chuo, jambo ambalo vile vile Mheshimiwa Profesa Peter M. Msolla, aliligusia kwenye mchango wake. Kamati imesema kwamba, Bodi ihusishwe kikamilifu katika mchakato wa uteuzi. Nakubaliana na hilo na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atatoa *Amendment* wakati wa Kamati.

Kwa sababu ile ambayo ilitoka mwanzo, haikukidhi hii haja. Kwa hivyo, nawashukuru sana kwa maoni haya. Namshukuru sana Mheshimiwa William H. Shellukindo, ambaye yeye ameonesha kwamba, kuna makosa ya uandishi na vile vile ushauri wake tutauchukua, kwa sababu kwa kweli hakuna ambao unaleta mabadiliko makubwa ndani ya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya kutoa maelezo haya, narudia tena kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe, kwa Kamati yangu, kwa Kambi ya Upinzani na Wabunge kwa ujumla, kwa maoni ambayo nimeyapata ya kuboresha Muswada huu. Ninawahakikishia kwamba, nitauboresha na kwa kuanzisha chuo hiki, sasa Tanzania itakwenda kwa kasi ambayo inatakiwa hasa tukizingatia kwamba, tunaingia kwenye Afrika ya Mashiriki. Kwa sababu upande ule mwingine, kuna Wanasheria wengi, ambao kila mwaka wanatoka kuwa Mawakili, nafasi ya vijana wetu isichukuliwe na Wanasheria wa Kenya au wa Uganda. Chuo hiki kitafanya Mawakili wawe wengi kila mwaka na waweze kujiajiri kama inavyotegemewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo Tanzania wa Mwaka 2007**
***(The Law School of Tanzania Bill, 2007)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutapitia *section by section* kutokana na muda.

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 13

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kufanya marekebisho kwenye *Clause* ya 13, sasa hivi isomeke kama ifuatavyo: *"The Minister shall, upon recommandation of the governing board, appoint a person who is suitable to be a Principal of the School."*

Ibara ndogo ya pili inasema: *"Before making recommandations, the governing board, shall consult the Attorney General."* *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21

Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 28

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 29

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 30

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Mafunzo ya Sheria kwa Vitendo Tanzania wa Mwaka 2007**
***(The Law School of Tanzania Bill, 2007)***
*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima, imepitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Taasisi ya Mafunzo ya Sheria Tanzania *(The Law School of Tanzania Act ya 2007),* pamoja na marekebisho yake na kuukubali. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada huu, pamoja na marekebisho yake, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKIA:** Kwa faida ya watoto wetu wa shule waliopo sasa, Muswada ukishakuwa umesomwa mara ya tatu, kwa upande wa Bunge umeshamaliza safari yake, tunasubiri sasa Rais aweke mkono wake, ndipo itakuwa sheria ya nchi hii.

## KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI WAKE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 21(6), naomba Bunge lako liahirishwe hivi sasa hadi kesho saa tatu asubuhi, ili kwa mujibu wa kanuni hiyo hiyo ya 21(9), kuweza kutoa nafasi kwa Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, aweze kutoa maelezo yake binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

## MAELEZO BINAFSI YA WABUNGE

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Napenda kutoa maelezo binafsi ya kuitaka Serikali, kutoa tamko juu ya hatima ya Shirika la Reli Tanzania *(TRC),* chini ya Kanuni ya 21(6), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mpanda ni miongoni mwa wilaya ambazo hazina barabara za uhakika za kuunganisha wilaya hiyo na maeneo mengine. Kutokana na kukosekana kwa barabara zenye uhakika wa kupitika mara zote, wananchi wa Mpanda wanategemea sana usafiri wa Reli ya Kati. Usafiri huu umekuwa wa matatizo sana miaka ya hivi karibuni.

Aidha, usafiri wa reli bado ni wa gharama nafuu duniani ikilinganishwa na njia nyinginezo za usafiri kama vile barabara, anga. Kutokana na sababu hizo kuu mbili, umuhimu wa reli zetu bado upo palepale, kama yalivyokuwa makusudio yake ya kujengwa kwa reli hizo wakati huo.

Aidha, itakumbukwa pia reli hii ilitoa mchango mkubwa katika Vita vya Kagera vya mwaka 1978/79. Sote tunafahamu umuhimu wake katika ulinzi na usalama wa nchi hii, si wa kupuuzwa. Zaidi ya hayo, reli hii imekuwa ikisafirisha mizigo kwa nchi jirani zisizo na bandari za *DRC,* Rwanda, Burundi na Uganda kwa miaka mingi na bado nchi hizo zinategemea reli hii, kama njia rahisi fupi na ya haraka, kusafirisha mizigo yao kwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam. Kwa njia hiyo, reli hii imekuwa kianzio kikubwa na cha uhakika cha kuipatia nchi yetu fedha za kigeni, vile vile ilitumika kupeleka msaada wa chakula, madawa na mahitaji mengine ya Wakimbizi na pengine hata usambazaji wa chakula nchini, usafiri wa reli ulitumika sana.

Kama nilivyoeleza hapo awali kwamba, ufanisi wa Shirika la Reli kwa sasa unatia mashaka na ni dhahiri shirika lipo katika hali mbaya ya kifedha, kuweza kujiendesha kwa faida. Hali hii iliyakumba Mashirika mengi ya Umma, baadhi yake yamebinafsishwa au kuuzwa na hasa mashirika yaliyokuwa yakijiendesha kwa faida, yaliweza kubinafsishwa mapema, zoezi hili lilipoanza miaka ya 1996.

Kuchelewa kuchukua hatua na maamuzi ya haraka ama kubinafsisha, kuuza au kukodisha na kutoliwezesha shirika kujiendesha lenyewe, kumesababisha hali kuwa mbaya zaidi, katika shirika hilo, kuliko ilivyokuwa wakati dhana ya ubinafsishaji imeanza kujichomoza au dhana ya

kuuza Mashirika ya Umma yaliyokuwa yakijiendesha kwa hasara. Hali ya *engine* za treni, mabehewa ya abiria na ya mizigo na huduma nyingine kwa sasa ni mbaya zaidi kuliko wakati wowote ule. Kuendelea kushindwa kufikia maamuzi angalau ya kukodisha, kumesababisha mambo kadhaa kujitokeza:-

(a) Kupunguza safari za abiria za kila siku kutoka na kurudi Dar es Salaam kuwa chache kwa wiki. afari kati ya Dar es Salaam na Bara na Bara - Dar es Salaam, sio tu zimepunguzwa lakini hata hizo chache zilizobaki wala hazianzi na kumalizika Dar es Salaam tena, kama ilivyokuwa awali, bali huanzia na kuishia Dodoma. Jambo ambalo limekuwa likileta usumbufu mkubwa kwa abiria na hata kusababisha wengi wao, kupoteza mizigo yao katika kuhamishia kwenye mabasi, ambayo nayo hayakuandaliwa kwa mpangilio makini. Hatua hii pia imeongeza gharama kubwa sana kwa abiria.

(b) Wafanyakazi kwa kutokujua hatima shirika na maslahi yao, ari ya kufanya kazi imepungua sana.

(c) Kitendo cha Serikali kutofikia maamuzi sahihi na kwa haraka, kunatoa mwanya wa kufanyika hujuma au ubadhirifu katika usimamizi, uendeshaji na ukusanyaji wa mapato na matumizi ya shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua hali hii itaendelea hadi lini? Natoa maelezo yangu binafsi ili wananchi waelezwe ukweli juu ya shirika. Wakati Serikali imekuwa ikilisaidia Shirika la Ndege, kwa kutoa ruzuku, pamoja na kuwa *ATC* bado ipo kwenye ubia na Shirika la Ndege la Afrika Kusini. Japo vyombo vya habari vimetoa taarifa kuwa ubia huo umekufa na wala hatuajelezwa kuwa ruzuku hiyo ni ongezeko la hisa yetu. Serikali imekaa kimya na wala hakuna hatua yoyote inayochuliwa, kuhusu Shirika la Reli, ambalo bado ni mali ya Serikali (Shirika la Umma). Reli inagusa maisha ya Watanzania walio wengi, ndio usafiri wa walala hoi, ninashindwa kufahamu na Watanzania walio wengi wanataka kufahamu vigezo vinavyotumika kuweka vipaumbele vyetu.

Pamoja na hayo basi, napenda kupata maelezo juu ya yafuatayo:-

(a) Mpango wa ubinafsishaji au ukodishaji wa *TRC* umefikia au umekwamia wapi? Ningependa Serikali itoe mchanganuo wa gharama na faida ya mpango huo, kujua manufaa yake kwa taifa letu.

(b) Serikali itoe kauli kuhusu usumbufu mkubwa unaosababishwa na hali ya kukatisha safari kutoka Bara na kushia Dodoma na safari ya Dar es Salaam kwenda Bara kuanzia Dodoma; lini utaratibu wa kawaida utarudishwa kuondoa usumbufu huo kwa abiria?

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo sababu na haja kama taifa, tuangalie njia bora na sahihi za kuendesha Shirika letu la Reli. Kwa kuangalia mtaji wake, muundo, menejimenti na ikama ya watumishi. Kama kuna vikwazo, ni vema tukaelezwa ili kama taifa, tushirikiane kutafuta mbinu za kuondoa vikwazo au kurekebisha panapowezekana. Kama taifa, ni kitu gani kinatushindwa kuliendesha Shirika letu la Reli kwa ufanisi na tija, ili liweze kuchangia maendeleo ya nchi yetu? Kama nchi yoyote duniani reli ni uti wa mgongo wa huduma za kijamii na kiuchumi, hata kwetu inawezekana tukiamua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja hii haihitaji kuungwa mkono na mtu yeyote, haya ni maelezo yake binafsi, Serikali inaweza kujibu sasa ama inaweza kujibu siku nyingine.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Nimesimama sio kutoa jibu kwa maelezo binafsi ya Mheshimiwa Said A. Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati, tunamshukuru aliyoyasema si mageni kwetu, lakini kwa sababu ya rekodi tu, kwa wakati muafaka Serikai itampa maelezo. Lakini kwa wananchi Watanzania na hasa ambao wanaitegemea reli hii, tunataka kuendelea kuwapa matumaini, reli yetu ni rasilimali muhimu sana, tutafanya kila lililo ndani ya uwezo wa Serikali, kukamilisha kile kizuri ambacho tunataka kukifanya. Tuwe na subira tu, lakini mambo mazuri hayahitaji haraka, hasa kwa suala kama hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda nikushukuru kwa kunipatia fursa hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawahoji kuhusu hoja ya Waziri wa Nchi ya kuomba Bunge liahirishwe mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 01.41 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa, Tarehe 9 Februari, 2007 saa tatu asubuhi)*